# MAKOSA YA KIMOFOSINTAKSIA KATIKA LUGHA YA KIMAONGEZI DHIDI YA KANUNI ZA LUGHA YA KISWAHILI SANIFU

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

KIRABI JULIUS MWANGI

TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

NOVEMBA, 2015

*1500556*
UoN Thesis

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya M.A katika Chuo Kikuu kingine chochote.

______________________ 09/11/2015

Kirabi Julius Mwangi Tarehe

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu sisi wasimamizi wafuatao:-

Daktari Jefwa Mweri Tarehe

Sahihi ______________________ 09/11/15

Daktari Ayub Mukhwana Tarehe

Sahihi ______________________ 21/11/2015

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa ambao ni mwenda zake Joel Kirabi Ngoti na Teresa Wanjiku Kirabi kwa kunizaa, kunilea na kunihimiza bila kuchoka abadan katan kuendelea na masomo yangu hadi katika kiwango cha juu. Pia namtabarukia mke wangu Alice Wambui Mwangi kwa uvumilivu wake wa kiwango cha juu na kwa kunipa moyo mambo yaliponiwia magumu. Mwishowe nawakumbuka watoto wangu Kelvin Kirabi, Teresa Wanjiku na Martin Muchori kwa kunihimiza nisome hadi nichukue nafasi ya kwanza.

**SHUKRANI**

Nampa shukurani za dhati Maulana kwa kunipa na kuniweka uhai na kunipa nguvu za kuikamilisha kazi hii. Kwa kweli nisingaliikamilisha kazi hii kama si kwa neema zake Mwenyezi Mungu. Kwake nasema utukufu na sifa zote ni zake.

Pili, kamwe siwezi kuwasahau wahadhiri wangu wa idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi kwa welekezi wao wa kitaaluma walionipa. Walinipa mwongozo nilipoonekana kukosa mwelekeo. Walinivumilia na kunisaidia bila kinyongo nilipowaendea nikitaka usaidizi. Wahadhiri hao ni pamoja na Prof. Zaja, Prof. Kineene, Bw. Mungania, Prof. Habwe, Prof. Mbatia, Dkt. Mbuthia, Dkt. Iribemwangi na Dkt. Swale. Nachukua nafasi hii vilevile kuwashukuru wasimamizi wangu ambao ni Dkt. Mukhwana na Dkt. Mweri. Uelekezi mlionipa sitausahau daima dawamu.

Aidha nawatolea shukrani wanafunzi wenzangu tulioabiri chombo kimoja na kutiana moyo kila mara. Wanafunzi hawa ni Otieno, Furaha, Jane, Regina, Scholar, Doris, Ruth, Magdalene, Nahashon, Beatrice, Mariam, Samwel, Margaret K., Margaret M, Sis. Teresa, Grace na Duncan. Kwao wote nawatakia maisha yenye fanaka.

Nawashukuru pia walimu wa shule yangu ya Watuha kwa kunipa fursa ya kufanya utafiti katika mazingira ya utulivu. Siwezi kamwe kuwasahau walimu wakuu wa shule za Muguru, Mukarara, Watuha, Kiangunyi na Kanyenya-ini kwa kuniruhusu kufanya utafiti katika shule zao.

Shukrani za dhati zimwendee mke wangu Bi. Alice Wambui Mwangi kwa kunitia moyo. Kwa kweli alikuwa karibu nilipomhitaji kwa ushauri na kwa kunifaa kwa mambo maridhawa. Alivumilia upweke nilipokuwa nakimbia hapa na pale nikijaribu kufanikisha kazi hii.

Kwa wote walioshiriki kufanikisha kazi hii naomba Mungu awabariki sasa na milele. Asanteni.

## IKISIRI

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kutathmini na kuchanganua makosa ya kimofosintasia katika lugha ya kimaongezi kwa wanafunzi na walimu katika kaunti ndogo ya Kangema. Walimu na wanafunzi tuliojihusisha nao walikuwa ni wakazi wa eneo hilo na lugha yao ya kwanza ilikuwa ni Kikuyu. Tulitumia mtazamo wa Uchanganuzi Makosa. Nadharia ya uchanganuzi Makosa iliasisiwa na corder na wenzake mnamo mwaka wa 1960. Kwa mujibu wa nadharia hii makosa husababishwa na visababishi vingi mbali na athari ya lugha ya kwanza. Nadharia hii vilevile inachangia katika kubaini mikakati ambayo hutumiwa na wanafunzi katika harakati za ujifunzaji wa lugha ya pili na aidha kutambua visababishi vya makosa na hata chanzo cha makosa mengi katika kazi za wanafunzi. Kwa kuongozwa na nadharia hii basi, katika utafiti wetu, tuliyasikiliza makosa na kuyaandika, kisha tuliyapanga kulingana na aina na hatimaye kuelezea kilichosababisha makosa hayo. Kabla ya kuingia nyanjani na kufanya utafiti wetu tulikisia kwamba makosa mengi ya kimofosintaksia yanayofanyika ni makosa ya kimatamshi. Tulikuwa pia tumetabiri kuwa, makosa mengi ya kimofosintaksia hutokana na mazingira na athari za lugha ya kwanza za wazungumzaji wa Kiswahili katika kaunti ndogo ya Kangema. Vile vile tulikisia kwamba ukiushi wa kimofosintaksia katika matumizi ya lugha hujitokeza pale walimu wanapowahutubia wanafunzi katika vikao rasmi na kwamba kuna uwezekano wa kuyarekebisha makosa hayo. Tulichagua vikundi viwili vya watafitiwa ambao ni walimu na wanafunzi. Tulichukua sampuli rahisi bila kufuata utaratibu wowote. Baada ya kuyakusanya makosa kutoka kwa watafitiwa wetu, kuyaweka katika kategoria kulingana na aina, tuliweza kudhibitisha makisio ya nadharia tete zetu. Tulifanyia utafiti wetu katika shule za upili na za msingi katika kaunti ndogo ya Kangema. Tulishughulikia mokosa ya kimofosintaksia pekee ingawa katika shughuli za kufanya hivyo tulijadili makosa ya kimofolojia. Hii ni kwa sababu makosa ya kimofosintaksia yanaweza kusababishwa na makosa ya kimofolojia. Tuliushughulikia ukiushi wa kimaongezi. Hatukuchunguza ukiushi wa kimaandishi. Wahusika wetu wa utafiti walikuwa ni wale wanaozungumza lugha ya Kikuyu kama lugha yao ya kwanza.Tulikuja kugudua kuwa mengi ya makosa hayo yalisababishwa na athari za lugha ya kwanza ambayo ni Kikuyu. Makosa hayo yalionekana yakiwa mengi sana katika viwango vya chini vya elimu na kupungua kadri mwanafunzi alivyoendelea na masomo ya kiwango cha juu. Umilisi

ulionekana kuongezeka kadri kiwango cha elimu kilivyoongezeka. Ilikuwa dhahiri kuwa walimu waliongea kwa ufasaha zaidi kuliko wanafunzi ingawa hata wao walifanya makosa hapa na pale.

## YALIYOMO

**UNGAMO** .......... iii

**TABARUKU** .......... iv

**SHUKRANI** .......... iv

**IKISIRI** .......... vi

**YALIYOMO** .......... vii

**SURA YA KWANZA** .......... 1

1.0 UTANGULIZI .......... 1

1.1 USULI WA MADA .......... 1

1.2 TATIZO LA UTAFITI .......... 3

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI .......... 4

1.4 NADHARIA TETE .......... 5

1.5 UMUHIMU WA UTAFITI .......... 5

1.6 UPEO NA MIPAKA .......... 6

1.7 MSINGI WA KINADHARIA .......... 8

1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI .......... 10

1.9 MBINU ZA UTAFITI .......... 14

1.9.1 UTEUZI WA WATAFITIWA .......... 14

1.9.2 UKUSANYAJI DATA .......... 15

1.9.3 UCHANGANUZI WA DATA .......... 15

**SURA YA PILI** .......... 16

**KANUNI ZA LUGHA YA KISWAHILI KIMOFOSINTAKSIA** .......... 16

2.0 UTANGULIZI .......... 16

2.1 LUGHA .......... 16

2.2 KISWAHILI SANIFU .......... 18

2.3 DHANA YA UKIUSHI .......... 20

2.4 NGELI ZA NOMINO ZA KISWAHILI .......... 21

2.4.1 UTANGULIZI .......... 21

2.5 UAINISHAJI WA NGELI KISINTAKSIA .......... 22

2.5.1 Ngeli ya A –WA ........ 23
2.5.2 Ngeli ya U-I ........ 23
2.5.3 Ngeli ya LI-YA ........ 23
2.5.4. Ngeli ya KI- VI ........ 24
2.5.5 Ngeli ya I-ZI ........ 24
2.5.6 Ngeli ya U – U ........ 24
2.5.7 Ngeli ya U- YA ........ 25
2.5.8 Ngeli ya U- ZI ........ 25
2.5.9 Ngeli ya YA-YA ........ 26
2.5.10 Ngeli ya I- I ........ 27
2.5.11 Ngeli ya KU ........ 27
2.5.12 Ngeli ya PA- KU – MU ........ 27
2.5.13 Ngeli nyinginezo ........ 28
2.5.13.1 Ngeli ya ZI-ZI. ........ 28
2.5.13.2 Ngeli ya VI-VI ........ 28
2.5.13.3 Ngeli ya LI-LI ........ 28
2.6 HITIMISHO ........ 28
2.7 AINA ZA MANENO ........ 29
2.7.1 UTANGULIZI ........ 29
2.7.2 NOMINO ........ 29
2.7.2.1 Nomino za pekee/nomino halisi. ........ 29
2.7.2.2 Nomino za kawaida ........ 30
2.7.2.3 Nomino za dhahania ........ 30
2.7.2.4 Nomino za wingi (vitu visivyohesabika) ........ 30
2.7.2.5 Nomino za vitenzi–jina ........ 30
2.7.2.6 Nomino za jamii ........ 31
2.7.2.7 Nomino za mguso ........ 31
2.7.2.8 Nomino ambatano ........ 31
2.7.3. VIVUMISHI ........ 31
2.7.3.1 Vivumishi vya sifa. ........ 31
2.7.3.2 Vivumishi vionyeshi (viashiria). ........ 31

2.7.3.3 Vivumishi viulizi. 32
2.7.3.4 Vivumishi virejeshi. 32
2.7.3.5 Vivumishi vya "a" unganifu. 32
2.7.3.6 Vivumishi vimilikishi. 32
2.7.3.7 Vivumishi vya idadi. 32
2.7.3.8 Vivumishi visisitizi 33
2.7.3.9 Vivumishi vya majina 33
2.7.3.10 Vivumishi vya pekee 33
2.7.4 VIWAKILISHI 33
2.7.4.1 Viwakilishi nafsi 36
2.7.4.2 Viwakilishi nafsi viambata/vitegemezi 36
2.7.4.3 Viwakilishi vya sifa 37
2.7.4.4 Viwakilishi vionyeshi/ viashiria 37
2.7.4.5. Viwakilishi vimilikishi 38
2.7.4.6 Viwakilishi vya pekee 38
2.7.4.7 Viwakilishi visisitizi 38
2.7.4.8 Viwakilishi viulizi 39
2.7.4.9 Viwakilishi virejeshi 39
2.7.4.10 Viwakilishi vya 'a' – unganifu 39
2.7.4.11 Viwakilishi vya idadi 40
2.7.4.12 Viwakilishi vya ngeli 40
2.7.5 VIELEZI 40
2.7.5.1 Vielezi vya namna 43
2.7.5.1.1 Vielezi vya namna halisi 44
2.7.5.1.2 Vielezi vya namna hali 44
2.7.5.1.3 Vielezi vya namna mfanano 44
2.7.5.1.4 Vielezi vya namna viigizi 45
2.7.5.1.5 Vielezi vya namna ala/kitumizi 45
2.7.5.1.6 Vielezi vya namna vinavyoonyesha mtenda /kitenda 45
2.7.5.1.7 Vielezi vya namna vinavyoonyesha mbinu/mikakati iliyotumiwa kufanikisha kitendo.. 45

2.7.5.1.8 Vielezi vya namna vikariri ..... 45
2.7.5.2 Vielezi vya wakati ..... 45
2.7.5.3 Vielezi vya mahali ..... 46
2.7.5.4 Vielezi vya idadi/kiasi ..... 46
2.7.5.4.1 Vielezi vya idadi ya jumla ..... 46
2.7.5.4.2 Vielezi vya idadi kamili ..... 47
2.7.6 VITENZI ..... 47
2.7.6.1 Aina za vitenzi ..... 48
2.7.6.1.1 Vitenzi halisi ..... 48
2.7.6.1.2 Vitenzi elekezi ..... 48
2.7.6.1.3 Vitenzi visoelekezi ..... 49
2.7.6.1.4 Vitenzi vikuu ..... 49
2.7.6.1.5 Vitenzi visaidizi ..... 49
2.7.6.2 Vitenzi vya hali/dhamira ..... 49
2.7.6.3 Vitenzi vishirikishi ..... 50
2.7.6.4Vitenzi sambamba ..... 51
2.7.7 VIHUSISHI ..... 51
2.7.7.1 AINA YA VIHUSISHI ..... 52
2.7.7.1.1 Vihushi vya wakati ..... 52
2.7.7.1.2 Vihusishi vya mahali ..... 52
2.7.7.1.3 Vihusishi vilinganishi/vya kulinganisha ..... 52
2.7.7.1.4 Kihusishi cha 'a'- unganifu ..... 53
2.7.7.1.5 Kihusishi 'na' cha mtenda ..... 53
2.7.7.1.6 Kihusishi 'kwa' cha kitenda/kifaa/jinsi ..... 53
2.7.7.1.7 Vihusishi vya sababu ..... 53
2.7.7.2 Matumizi zaidi ya kihusishi 'kwa' ..... 53
2.7.8 VIUNGANISHI ..... 54
2.7.8.1 Viunganishi ambatani/ambatishi ..... 54
2.7.8.2 Viunganishi vitegemezi ..... 54
2.7.8.3 Aina za viunganishi ..... 54
2.7.8.3.1 Viunganishi viongezi/vya kuongeza ..... 55

2.7.8.3.2 Viunganishi visababishi/vya sababu ........ 55
2.7.8.3.3 Viunganishi vya nia/dhamira/matokeo ........ 55
2.7.8.3.4 Viunganishi vya kinyume ........ 55
2.7.8.3.5 Viunganishi vya wakati ........ 55
2.7.8.3.6 Viunganishi vya masharti ........ 56
2.7.8.3.7 Viunganishi vya uteuzi ........ 56
2.7.8.3.8 Viunganishi vitegemezi ........ 56

**SURA YA TATU ........ 58**
3.0 MAKOSA YA KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA ........ **58**
3.1 UTANGULIZI. ........ 58
3.2 Makosa ya kifonolojia ........ 58
3.3 Makosa ya kimofolojia ........ 60
3.3.1 Dhana ya mofolojia ........ 60
3.3.2 Ukiushi wa kiwango cha kimofolojia ........ 60
3.4 Hitimisho ........ 64

**SURA YA NNE ........** 66
4.0 Makosa ya kimaongezi ya kiwango cha kimofosintaksia ........ 66
4.1 utangulizi ........ 66
4.2 KATEGORIA ZA MAKOSA ........ 67
4.2.1 Makosa yanayohusu ukosefu wa upatanifu katika ngeli za nomino. ........ 67
4.2.1.1 NGELI YA A-WA ........ 67
4.2.1.2 Ngeli ya U-I ........ 71
4.2.1.3 Ngeli ya LI-YA ........ 72
3.2.1.4 Ngeli ya KI-VI ........ 74
4.2.1.5 Ngeli ya I-ZI ........ 76
4.2.1.6 Ngeli ya U-ZI ........ 78
7.2.1.7 Ngeli ya YA-YA ........ 79
4.2.1.8 Ngeli ya PA-KU-MU ........ 79
4.3 HITIMISHO ........ 80

**SURA YA TANO** .......... **82**
5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 82
5.1 MUHTASARI .......... 82
5.2 HITIMISHO .......... 83
5.3 Mapendekezo .......... 84
MAREJELEO .......... 87
KIAMBATISHO .......... 89

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 USULI WA MADA

Lugha ya Kiswahili ni lugha muhimu sana nchini Kenya na katika nchi zingine kama vile Tanzania, Rwanda, Msumbiji, Uganda, Afrika Kusini, Burudi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa kuwa ni Lingua Franka katika eneo hili. Nchini Kenya, lugha ya Kiswahili imepewa majukumu mawili muhimu ambayo ni kuwa lugha rasmi na lugha ya kitaifa.

Kiswahili kama lugha rasmi hutumika katika shughuli rasmi za kiserikali kama vile mikutano rasmi, katika ofisi za serikali na hata katika uandishi wa barua rasmi nchini Kenya. Kama lugha ya kitaifa, Kiswahili kimetwikwa jukumu la kuwaunganisha Wakenya wote kwani ndiyo lugha inayotumika katika maeneo yote nchini Kenya.

Kando na kuunganisha Wakenya, lugha ya Kiswahili pia huleta umoja wa kimataifa kwa sababu wananchi mbalimbali kutoka nchi zingine kama vile Tanzania na Unguja wanaozungumza lugha ya Kiswahili wameweza kushirikiana kufanya mambo pamoja kama vile biashara kwani wanaweza kuelewana kwa urahisi.

Kwa mujibu wa Massamba (1999), Kiswahili ni lugha inayotumiwa na watu wanaokadiriwa kuwa milioni 60 kote ulimwenguni. Katika orodha ya lugha zinazozungumzwa na watu wengi zaidi duniani, Kiswahili huchukua nafasi ya pili baada ya lugha ya Kiarabu. Kiswahili kwa hivi sasa ni somo la lazima katika shule za msingi na zile za sekondari nchini Kenya. Aidha ni somo linalofunzwa pia katika vyuo vikuu vyote nchini Kenya isipokuwa vile vinavyofunza kosi za Sayansi na Teknolojia. Vyuo hivyo ni vile vya umma na hata vya kibinafsi. Mifano ya vyuo vinavyofunza lugha ya Kiswahili nchini Kenya ni kama vile Chuo Kikuu cha Nairobi, Chuo Kikuu cha Moi, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Chuo Kikuu cha Mount Kenya, Chuo Kikuu cha Maseno, Chuo Kikuu cha Egerton, Chuo Kikuu cha Karatina na vyuo vingine vya elimu ya juu vinavyofunza sanaa na kosi ya ualimu.

Hata nje ya mipaka ya Kenya, kunavyo vyuo vikuu vinavyofunza lugha ya Kiswahili kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nchini Tanzania na Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini Uganda. Vile vile karibu vyuo vikuu vyote ulimwenguni vina idara ya Kiswahili. Lugha hii hutumika katika vyombo vya habari kama vile radio, televisheni, majarida na magazeti. Katika burudani, lugha hii haijaachwa nyuma kwani wataalam wa kutunga mashairi na nyimbo huitumia lugha hii.

Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kama vile Kimvita, Kivumba, Kimtangata, Kitukuu, Kipemba na Kiunguja. Utafiti wetu ulijikita katika Kiswahili sanifu ambacho kimetokana na lahaja ya Kiunguja iliyosanifishwa na kuwa msingi wa kufunzia Kiswahili sanifu.

Kama tulivyotaja, lugha ya Kiswahili kama somo hutahiniwa katika viwango vyote vya elimu nchini Kenya. Katika shule ya msingi, Kiswahili hutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa Kenya Certificate of Primary Education (K.C.P.E) na husaidia kuamua gredi ya kumwezesha mwanafunzi kujiunga na shule ya sekondari.

Mwanafunzi anapojiunga na shule ya sekondari anaendelea kujifunza lugha hii kwa miaka yote minne na hatimaye hufanya mtihani wa Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E). Mtihani katika kiwango hiki huhusu sarufi, ufahamu, uandishi wa insha na fasihi ya Kiswahili. Insha na sarufi hutumiwa kutahini umilisi wa lugha ya mwanafunzi na stadi za kujieleza na kufupisha ambapo makosa tofauti tofauti hubainishwa na kuainishwa. Mwanafunzi anapofanya vizuri katika somo hili, husaidika sana kwani gredi anayoipata katika somo la Kiswahili huchangia katika gredi ya wastani inayomwezesha kujiunga na Chuo Kikuu na hata vyuo vingine vya elimu ya juu.

Katika Vyuo Vikuu, mwanafunzi anayechukua Kiswahili hupitia viwango vyote vya lugha kama vile fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmantiki. Anapobobea katika lugha na kuwa mwanaisimu, huchangia katika ufunzaji wa lugha, uhariri wa makala na hata uandishi wa vitabu na majarida.

Silabasi ya Kiswahili huwa na malengo ambayo huoana na mambo ambayo wanafunzi hupaswa kujifunza. Malengo haya hudhamiriwa kuwaelekeza walimu katika kuwafunza wanafunzi na kuwapa stadi za kimsingi katika kujifunza Kiswahili sanifu.

Stadi hizi ni kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Baada ya kufunzwa basi, wanafunzi wanatarajiwa wawe na uwezo wa kutumia Kiswahili sanifu katika mazungumzo, matamshi, uandishi na vile vile waweze kuyatambua makosa ya kisarufi yanayofanywa na wazungumzaji wengine.

Uelewa wa mambo haya hurahisisha mawasiliano. Kutokuelewa kwa stadi hizi huyatatiza mawasiliano kwa sababu ya makosa yanayojitokeza. Hivyo basi pana haja ya utafiti kufanywa kuhusu makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika lugha ya kimaongezi ili yabainishwe na hatua mwafaka kuchukuliwa ili lugha ya Kiswahili ipate kuboreshwa zaidi.

Utafiti wetu ulishughulikia swala la makosa yanayotokea katika lugha ya kimaongezi. Makosa haya ni yale yanayotokea kwa sababu ya kutofuata kanuni za matumizi ya lugha fulani kimaongezi au kimaandishi. Makosa katika lugha ya kimaongezi unahusu hoja mbalimbali. Kuna makosa ya kifonetiki, makosa ya kifonolojia, ya kimofolojia, ya kisintaksia, ya kimofosintaksia na ya kisemantiki. Sisi tulijikita katika mambo machache kati ya nyanja zote zinazohusu matumizi ya lugha. Tuliangalia makosa yanayojitokeza katika kiwango cha kimofosintaksia.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Mawasiliano ni muhimu sana katika jamii yoyote ile. Iwapo mawasiliano hayatadumishwa, basi mambo mengi yatakwama. Mawasiliano katika jamii huwezeshwa na lugha kwani lugha ndicho chombo muhimu zaidi kinachowezesha mawasiliano. Aidha, Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya kwa hivyo hatuna budi kuhakikisha kuwa imetumika vizuri kwa kufuata kanuni zake. Njia mwafaka ya kufanya hivi ni kubaini makosa ni yapi, yanatokezea wapi, vipi na kwa sababu gani ili tuweze kuyashughulikia.

Utafiti huu unatokana na imani kwamba makosa katika lugha ya kimaongezi ni tukio halisi na dhahiri katika matumizi ya lugha yoyote ile.

Kuifahamu lugha na kuielewa kikamilifu kunahusu pia ufahamu wa makosa na sababu za kutokea kwa makosa hayo. Utafiti wetu ulichunguza na kuonyesha baadhi ya makosa yanayotokea katika hali halisi ya maongezi ya walimu na wanafunzi kutoka katika kaunti ndogo ya Kangema katika kauti ya Murang'a.

Utafiti wetu ulishughulikia swala la makosa ya kimofosintaksia katika maongezi ya kawaida na katika yale yaliyo katika vikao rasmi dhidi ya kanuni au kaida za lugha sanifu ya Kiswahili. Tulijikita katika mazungumzo ya walimu wanapowahutubia wanafunzi katika vikao rasmi na vilevile katika mazungumzo ya walimu yaliyo rasmi na yasiyo rasmi. Tuliwahusisha pia wanafunzi wakiwa nje na ndani ya darasa.

Ni makosa kudai kwamba uongeaji wa lugha yoyote unaweza kufanywa kwa ufasaha kikamilifu. Hata hivyo pana viwango tofauti vya ufasaha. Tunatumia istilahi ufasaha kwa maana ya ukubaliano fulani katika kanuni za kimatamshi, kisintaksia na kisemantiki. Ukubaliano huu ni muhimu katika maongezi ya lugha, (Max Black, 1968).

Kaunti ndogo ya Kangema hupatikana katikati mwa nchi ya Kenya. Inazingirwa na wazungumzaji wa lugha ya Kikuyu kila upande. Wakaazi wengi wa kaunti ndogo hii huongea Kikuyu kama lugha yao ya kwanza. Kutokana na haya, utafiti wetu uliongozwa na maswali yafuatayo;

(i) Je, ni makosa gani yanayotokea katika hali halisi ya maongezi ya walimu na wanafunzi kutoka katika kaunti ndogo ya Kangema katika kaunti ya Murang'a?

(ii) Je, makosa katika kiwango cha kimofosintaksia hujitokeza kutokana na nini?

(iii) Je, waalimu wanapohutubia wanafunzi kirasmi makosa hujitokeza?

(iv) Je, kuna uwezekano wa kuyapunguza au kuyarekebisha makosa hayo?

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika utafiti wetu tulinuia:-

(i) Kuorodhesha aina zote za makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika hali halisi ya mazungumzo ya walimu na wanafunzi dhidi ya kanuni za lugha ya Kiswahili sanifu.

(ii) Kubainisha chanzo cha ukiushi wa kimofosintaksia.

(iii) Kubaini iwapo ukiushi wa kimofosintaksia hujitokeza walimu wanapowahutubia wanafunzi.

(iv) Kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuyarekebisha au kuyapunguza makosa hayo.

## 1.4 NADHARIA TETE

Katika utafiti wetu, tulikisia kwamba:-

(i) Makosa mengi ya kimofosintaksia yanayofanyika ni makosa ya kimatamshi na yanaweza kuorodheshwa.

(ii) Makosa mengi ya kimofosintaksia hutokana na athari za lugha ya kwanza ya wazungumzaji wa Kiswahili katika kaunti ndogo ya Kangema.

(iii) Ukiushi wa kimofosintaksia katika matumizi ya lugha hujitokeza pale ambapo walimu wanawahutubia wanafunzi katika vikao rasmi.

(iv) Kuna uwezekano wa kuyarekebisha au kuyapunguza kwa kiwango kikubwa makosa hayo.

## 1.5 UMUHIMU WA UTAFITI

Umuhimu wa utafiti huu unatokana na nafasi teule ya Kiswahili katika nchi ya Kenya na haja ya kukiendeleza na kuhimiza matumizi bora ya Kiswahili. Mtu asiyeweza kuteua viambishi-ngeli sahihi katika matumizi ya Kiswahili huishia kukiuka kanuni zake kwa kuiboronga lugha hiyo.

Makosa ya lugha ya Kiswahili yanaathiri maendeleo na ukuaji wa Kiswahili sanifu. Ukiushi huu wa lugha unaipa lugha sanifu mwelekeo ambao ni hasi na kuwa pingamizi kwa kutimiza malengo ya kupita mitihani hasa miongoni mwa wanafunzi ambao wanahitaji msingi imara wa Kiswahili sanifu.

Uchunguzi wa matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii hulenga kuainisha matumizi ya lugha katika maisha ya kila siku na wala sio jinsi watu wanavyozungumza wakati mazungumzo yanapokuwa yakirekodiwa. Matumizi haya yanapoainishwa, makosa kugunduliwa na chanzo cha makosa hayo kubainishwa, mapendekezo hutolewa nao washikadau wote watashirikishwa ili kuupiga vita ukiushi dhidi ya Kiswahili sanifu shuleni na hata vyuoni. Washikadau hawa ni kama vile walimu, wanafunzi, watangazaji katika vituo vya redio na televisheni, waandishi wa majarida na magazeti, viongozi na wahubiri. Hawa wote wakishirikishwa katika jukumu hili la kupiga vita makosa katika Kiswahili sanifu tutakuwa tumepiga hatua kudhibiti Kiswahili sanifu na kukilinda kutokana na kuborongwa. Jambo hili litakuwa na manufaa kwa maendeleo ya nchi yetu kwa jumla kwani litaleta umoja wa Wakenya na kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Utafiti huu vilevile utakuwa ni mchango kwa tafiti zingine zilizowahi kufanywa katika maeneo mengine nchini Kenya. Utakuwa umeongezea utajiri wa ujuzi wa ni kwa nini makosa dhidi ya kanuni za Kiswahili sanifu yanakuwa tofauti katika maeneo tofauti. Kwa hivyo mbinu mwafaka za kukabiliana na makosa haya zitaweza kubuniwa kulingana na aina za makosa katika eneo mahsusi. Hii ina maana kwamba jinsi ya kukabiliana na aina tofauti za makosa zinaweza kuwa tofauti kutegemea maeneo ambayo makosa hayo hutokea.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Utafiti wetu umeshughulikia swala la makosa yanayotokea katika lugha ya kimaongezi tu bila kujikita katika lugha ya kimaandishi. Maongezi haya yalikuwa ni yale ya kawaida ambayo ni yale yasiyokuwa katika miktadha rasmi na vile vile maongezi yaliyokuwa katika vikao rasmi. Kazi yetu ilishughulikia wanafunzi na walimu pekee wakiwa katika muktadha wa shuleni.

Data yetu tuliichanganua katika kiwango cha kimofosintaksia ambacho kinahusu mwingiliano wa mofolojia na sintaksia katika matumizi ya lugha pale ambapo pana baadhi ya maneno ambayo yanaweza kujisimamia kama neno na wakati huo huo liwe na

sifa za sentensi. Makosa ya kimofosintaksia pia huhusu ukosefu wa upatanisho wa viambishi vipatanishi vya makundi ya maneno na viambishi ngeli katika ngeli za nomino. Kuna mengi ya kutafitiwa na kujadiliwa kuhusu matumizi ya lugha, lakini tuliiteua sehemu hii ili tuweze kuishughulikia kikamilifu.

Utafiti wetu ulifanyiwa katika shule za mashambani bali si mijini. Shule hizo zilikuwa ni pamoja na Shule ya Msingi ya Watuha, Shule ya Upili ya Watuha, Shule ya Msingi ya Mukarara, Shule ya Upili ya Wasichana ya Kiangunyi, Shule ya Msingi ya Kanyenya-ini na Shule ya Upili ya Muguru. Tulijikita katika maongezi ya kawaida ya walimu na wanafunzi wa kaunti ndogo ya Kangema. Wahusika wetu walikuwa wale wanaozungumza lugha ya Kikuyu kama lugha yao ya kwanza.

Utafiti wa kazi kama hii unaweza kufanyiwa katika sehemu yoyote ile, iwe mijini au mashambani, mahali ambapo lugha ya Kiswahili inapozungumzwa kwani makosa katika lugha ya kimaongezi huweza kutokea mahali popote kila mara lugha inapozungumzwa. Utafiti huu tuliufanyia mashambani katika kaunti ndogo ya Kangema katika kaunti ya Murang'a.

Tulijishughulisha na utafiti wetu shuleni. Utafiti huu uliyang'amua baadhi ya makosa yanayofanywa na walimu na wanafunzi wa katika eneo hili. Baada ya kuyatambua, tuliyaainisha katika kiwango cha kimofosintaksia. Tulitaja sababu za kutokea kwa makosa hayo na kupendekeza njia za kuyarekebisha.

Utafiti huu unanuia kuikuza lugha ya Kiswahili kwa kufanya juhudi kuiboresha kwani ikiwa lugha ya Kiswahili itakua, inaweza kuleta umoja wa Kitaifa na kurahisisha mawasiliano baina ya watu, kutowapotosha wanaosikiliza na wanaojifunza lugha ya Kiswahili, kukuza biashara na uchumi wa taifa na kudhibiti kuborongwa kwa lugha ya Kiswahili.

Katika utafiti wetu, tulijikita katika kaunti ndogo ya Kangema ambapo wakazi wengi huzungumza kwa lugha ya Kikuyu ingawa kuna baadhi wa watu waliotoka katika

makabila mengine wanaofanya kazi ofisini na katika shughuli za kibiashara. Watu hawa wanazungumza lugha za kwanza tofauti na ile ya Kikuyu. Tutazingatia miktadha mbalimbali, watu wenye viwango tofauti vya elimu shuleni ambao ni wanafunzi na walimu.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti wetu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganizi Makosa. Nadharia hii iliasisiwa na Corder na wenzake mnamo mwaka wa 1960. Kulingana na nadharia hii, makosa husababishwa na visababishi vingi bali na athari za lugha ya kwanza. Nadharia hii inachangia katika kubaini mikakati ambayo hutumiwa na wanafunzi katika harakati za ujifunzaji wa lugha ya pili na vilevile kutambua visababishi vya makosa na hata chanzo cha makosa mengi katika kazi za wanafunzi. Nadharia hii ni muhimu kwani humwezesha mtafiti kujua jinsi watu hujifunza lugha na mikakati wanayoitumia katika harakati za kutambua lugha lengwa, (Corder, 1967:167). Wanaojifunza lugha hukiuka kaida za lugha ya pili.

Nadharia hii ni tawi la isimu tumikizi. Inajihusisha na kuyatambua, kuyachunguza na kuyachanganua makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha ya pili. Watafiti wa lugha ya pili kama vile Mc Laughlin (1987) na Ellis (1985) ndio walioufunga Uchanganuzi Makosa katika nadharia ya lugha kadirifu.

Lugha kadirifu ni lugha inayoundwa na wanaojifunza lugha ya pili katika harakati zao za kuimudu lugha lengwa. Lugha Kadirifu kwa mujibu wa Nemser (1971) ni mfumo wa ukadirifu. Lugha kadirifu ni lugha ambayo ni ya kukisiwa au kufikiriwa. Corder (1967) anaiita lugha kadirifu 'umilisi wa kimpito.' Lugha hii hubadilika na wakati kwani anayejifunza lugha hutafuta mikakati ya kuzungumza kwa lugha anayojifunza.

Selinker (1969) anadai kuwa lugha kadirifu inatokana na mifanyiko mitano ya kiakili (kisaikolojia) ili kuweza kuchanganua matatizo katika matumizi ya lugha. Mifanyiko hiyo ni pamoja na:-

(i) Uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza hivyo kukiuka kanuni za lugha ya pili.

(ii) Mikakati ya mawasiliano katika lugha ya pili.

(iii) Njia za kujifunza zisizokuwa halisi.

(iv) Uhamishaji wa ufundishaji ambapo makosa hutokana na kutokuwa na umilisi kwa wale wanaofunza lugha ya pili.

(v) Ujumlishaji mno kutokana na mifumo ya lugha ya kwanza inayotumiwa kiholela.

Utafiti kuhusu lugha kadirifu kupitia Uchanganuzi wa Makosa umewahi kutumiwa kuimarisha ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya pili. Utafiti huu ulitumia nadharia ya kujifunza lugha kama msingi wake.

Utafiti huu ulitumia ile njia ya kuchanganua matatizo yanayosababisha makosa ya kimofosintaksia. Makosa haya yanakisiwa kuwa ni yale yanayodhihirika katika lugha kati. Lugha kati, kwa mujibu wa Selinker (1962) ni lugha inayoundwa na wanaojifunza lugha ya pili katika harakati zao za kutaka kufikia lugha lengwa. Selinker anaendelea kusema kuwa lugha kati ni mfumo tofauti wa kiisimu ambao unaibuka kutokana na ile harakati ya kujifunza lugha ya pili. Selinker anasema kuwa lugha-kati hubadilikabadilika kulingana na muktadha; jambo ambalo limeungwa mkono na Tarone (1979).

Corder (1967) anasema kwamba katika lugha ya mwanafunzi anayejifunza lugha fulani, kuna muundo fulani ambao hujitokeza na pia mikakati fulani ya kujifunza ile lugha. Matatizo ambayo yanadhihirika (na ambayo yanasababisha makosa) katika muundo huu wa lugha ndio dhihirisho ya kwamba mwanafunzi yuko katika harakati za kujifunza lugha ya pili.

Kutokana na maelezo haya, uchanganuzi wa matatizo haya ukawa ndio unatumika sana na watafiti. Dulay na Burt (1974) wanaeleza kwamba, uchunguzi wa lugha uliofanywa ulidhihirisha kwamba matatizo ya lugha katika mazungumzo yalikuwa tofauti na matatizo ya lugha katika maandishi. Nadharia hii ilitusaidia kuweza kuyaorodhesha makosa ya kimofosintaksia katika makundi mawili ambayo ni:

(i) Makosa yanayotokana na lugha kadirifu.

(ii) Makosa yanayosababishwa na athari za lugha ya kwanza.

## 1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

Swala la uchanganuzi wa makosa yanayopelekea kutokea kwa makosa katika lugha sanifu ya Kiswahili limeshughulikiwa na watafiti kadhaa. Rapando (2005) alichunguza makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili jijini Nairobi.

Aliyabainisha makosa yenyewe na kutathmini jinsi ambavyo wanafunzi wameweza kujirekebisha na hata kujimudu katika lugha ya Kiswahili sanifu. Kazi ya Rapando ilitufaidi katika utafiti wetu kwa kutusaidia kubaini baadhi ya makosa ijapokuwa utafiti wetu hauchunguzi makosa ya kimaandishi bali tulijikita katika kuchunguza makosa ya kutofuata kanuni za lugha ya Kiswahili kimaongezi.

Andala (2008) alichanganua makosa yanayofanywa katika lugha ya Kiswahili yakiwemo ya msamiati, sarufi, yanayotokana na ngeli na yale yanayotokana na lugha zingine. Andala anatoa kauli kuwa kuna mazoea ya watu kutumia lugha ya Kiswahili bila makini. Alidai kuwa uborongaji wa lugha ya Kiswahili unaathari vibaya lugha hii kwa kutoa mifano ifuatayo kama baadhi ya matamshi yasiyofaa aliyowahi kuyasikia:-

**(i)** **'Katoto kale ni kangu'** badala ya **'kijitoto kile ni changu'**

**(ii)** **'Niwekee chai'** badala ya **'nitilie chai'**

**(iii)** **'Sababu ni mgonjwa'** badala ya **'kwa sababu ni mgonjwa'**

Vilevile alitaja matumizi potofu ya viambishi vipatanishi vya vivumishi vya idadi kama vile **visita** na **visaba**. Alitaja pia makosa ya vivumishi kama:

**(i)** **'Vitabu zake zote'** badala ya **'vitabu vyake vyote'**

(ii) **'Choo yetu'** badala ya **'choo chetu'**

(iii) '**Kabati hii'** badala ya **'kabati hili'**

(iv) **'Nywele yake'** badala ya **'nywele zake'**

(v) **'Gari hii'** badala ya **'gari hili'**

Utafiti huu ulitufaidi sana kwani uligusia makosa ya jumla ya vipatanishi yanayotokana na viambishi ngeli kwani kwa mujibu wa Mbaabu (1995), ngeli ndizo nguzo za sarufi ya Kiswahili na viambishi ambavyo vinapotumiwa katika tungo huathiri ufasaha wa yanayoandikwa au yanayosemwa. Kutokujua viambishi – vipatanishi vya kutumia katika

sentensi huleta ukiushi wa lugha. Ukiushi huu huweza pia kuletwa na maingiliano ya ujuzi wa lugha nyingine hasa lugha ya kwanza ya mtu anayetumia Kiswahili. Anasema kuwa, kuna mazoea ya kuacha viambishi–vipatanishi hasa katika nomino za binadamu. Mfano alioutoa ni:

**'Mtoto moja'** badala ya **'mtoto mmoja.'** Mbaabu (1995) anaendelea kusema kuwa idadi kubwa ya makosa ya upatanisho wa ngeli hutokea katika matumizi ya viambishi – vipatanishi vya vimilikishi ambavyo huambishwa kulingana na ngeli husika kwani kuna uwezekano wa kusikia matamshi kama:

(i) **'Kiti yangu'** badala ya **'kiti changu'**

(ii) **'Ngo'mbe yangu'** badala ya **'ng'ombe wangu'**

(iii) **'Kabati yake'** badala ya '**kabati lake'**

Utafiti huu, ingawa uliangazia lugha ya kimaandishi umeetufaa kwani umetuonyesha baadhi ya makosa ya kimofosintaksia katika lugha ya kimaandishi ambayo pia tulikubana nayo katika lugha ya kimaongezi. Kazi ya Adala ilitusadia kung'amua ya kwamba makosa kama haya hupatikana katika maeneo tofauti nchini Kenya. Aidha ulitusaidia kudhihirisha kuwa makosa ya kimofosintaksia katika lugha ya maongezi hujidhihirisha pia katika lugha ya maandishi.

Kapufi (2008) anadai kuwa kuna uwezekano wa kuwa na makosa ya lugha yanayotokana na uteuzi mbaya wa viambishi vipatanishi kuweza kudhihirika katika hali ya wingi- lugha ambapo, kila lugha katika mazingira inatoa athari zake. Utafiti huu ulitufaa kwa kiasi fulani kwani utafiti wetu ulijikita katika kikundi cha watu wanaozungumza lugha moja ya kwanza.

Bila shaka, walimu hawa tuliojihusisha nao katika utafiti wetu walikuwa wanafunzi wakati fulani maishani mwao. Ukiushi unaofanywa na wazungumzaji hawa labda ulitokea walipokuwa shuleni.

Dai hili lilithibitishwa na uchunguzi tulioufanya kwa wanafunzi wanaosoma ama katika shule za msingi au zile za upili. Kwa mujibu wa Kapufi, mwanafunzi anapokiuka kanuni za lugha sanifu ya Kiswahili huwa hajui kuwa anayofanya ni makosa. Mwanafunzi kama

huyo huwa yumo katika harakati za kujifunza lugha ya pili na juhudi zake humfanya kupotoka bila kutambua.

Corder (1974) akinukuliwa na Gass na Selinker (2001: 78) anaeleza kwamba wanafunzi wanapofanya makosa ya uteuzi wa vipatanishi hawafahamu kuwa hayo ni makosa. Kwao, huwa wamejijengea sarufi ubongoni mwao ambayo ndiyo watumiayo kutungia sentensi zilizokiuka kanuni za lugha. Sentensi zilizokiuka kanuni za lugha zinadhihirisha kiwango cha umilisi alichofikia mzungumzaji wa lugha ya pili. Umilisi huu huonyesha mabadiliko kadri muda unavyokwenda. Upotofu huu unasaidia kuonyesha ushahidi wa jinsi lugha zinavyofunzika na hatimaye kumsaidia mwanafunzi kuzielewa kanuni za lugha baada ya kukosolewa na mwalimu wake. Dai hili ni la Kapufi (2008) akinukuliwa na Ellis na Barkuizen (2008:51)

Dai hili la Kapufi hata hivyo halikutilia maanani ukweli kwamba si makosa yote yanayofanywa na wanafunzi hurekebishwa hatimaye. Baadhi ya wanafunzi hukua na kutoka shuleni huku wakiyasheheni makosa yale yale waliyokuwa nayo walipokuwa shuleni.

Kapufi anaendelea kudai kuwa, kwa vile lugha ya Kiswahili ni lugha ambishi-bainishi, inakuwa ni rahisi kwa makosa ya ujumlishaji mno kuwepo kwani vipatanishi vinavyoteuliwa huweza kuwa na maumbo yanayofanana.

Chesire (1962) alifanya utafiti kuhusu makosa katika miundo ya kimofolojia na kisintaksia kati ya wahusika 24 wakiwa ni wavulana na wasichana wa umri wa kati ya miaka 9 na 17. Aligundua kwamba wahusika walifanya makosa mengi zaidi walipokuwa nje ya shule kuliko yale waliofanya walipokuwa katika mazingira ya shule. Aidha aligundua ya kwamba mahali mtu alikotoka humwathiri katika matumizi yake ya lugha kutokana na uzungumzaji aliouzoea. Utafiti huu wa Chesire ulitufaa kwani tuliufanya utafiti wetu katika miktadha aliyotumia na mingineyo.
King'ei na Musau (2002) walishughulikia matatizo yanayowakumba wale wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Waliweza kuzingatia matatizo ya matamshi, sarufi,

msamiati na maana. Waligundua kuwa mojawapo ya matatizo yanayosababisha matumizi yasiyofaa ya Kiswahili hasa kwa wale wanaojifunza lugha hii kama lugha yao ya pili ni kule kujaribu kukizungumza Kiswahili kama wanavyozungumza lugha yao ya kwanza wakififikiri kuwa miundo ya lugha hizo ni sawa. Wao hutafsiri dhana zinazopatikana katika lugha ya kwanza kwa njia iliyo ya moja kwa moja. Kwa kuwa wataalamu hawa walizingatia matatizo mengi kijumla, utafiti wao ulitufaa kwani tuliufanya utafiti unaokaribiana sana na huu lakini katika eneo na upeo tofauti. Hii ni kwa sababu tuliyaorodhesha makosa yaliyosababishwa na athari za lugha ya kwanza kimaongezi.

Musau (1992) alishughulikia mikakati wanayotumia wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya pili. Alidai kuwa nomino, kulingana na ngeli yazo, hupatanishwa na maneno mengine katika sentensi kwa kutumia viambishi. Aliendelea kuelezea kwamba mzungumzaji wa Kiswahili sanifu hana budi kutumia viambishi vinavyofaa. Aligudua katika utafiti wake kuwa wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili hutatizika wanapotumia viambishi mbalimbali. Kwa hivyo akagundua kuwa, makosa ya upatanishi hujitokeza katika sentensi kwa kutotambua ni lini ambapo watatumia viambishi hivi. Anaelezea kuwa kosa la ujumlishaji mno wa baadhi ya viambishi hujitokeza. Viambishi vya ngeli ya I-ZI hutumiwa katika ngeli nyingine. Mfano alioutoa ni **'kiatu imepotea'** badala ya **'kiatu kimepotea.'** Aidha alishughulikia uhamishaji lugha kama tatizo mojawapo linaloathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Kazi hii ya Musau inatufaa kwa kuwa baadhi ya mambo aliyoshughulikia ndiyo yale tuliyoshughulikia.

Rapando (2005) alilinganisha nadharia ya Uchanganuzi Makosa na Uchanganuzi Linganuzi kwa kueleza kuwa Uchanganuzi Makosa huangalia makosa ambayo yametokana na sababu tofauti mbali na yale yanayosababishwa na lugha ya kwanza ilhali Uchanganuzi Linganuzi uliangalia makosa katika misingi ya lugha kuathiriana. Uchanganuzi Makosa hutumia mitazamo miwili. Katika mtazamo wa kwanza, mtafiti huibua kategoria zake za makosa kwa misingi ya makosa anayodhani hutokea katika makundi tofauti. Makosa, katika mtazamo huu, ndiyo yanayoamua kategoria. Mtazamo wa kwanza unajulikana kama 'kategoria iliyoteuliwa awali' nao mtazamo wa pili huitwa 'makosa huamua kategoria' Mtazamo wa pili hauhusiki na kuamua aina ya makosa

yatakayofanywa. Badala yake, ni makosa yaliyoainishwa yanayoamua kategoria hizo tofauti. Sisi tulitumia mtazamo wa pili ambapo makosa yalituelekeza katika kategoria fulani. Isitoshe, tofauti na utafiti wa Rapando, wetu ulijikita katika nadharia moja tu.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

### 1.9.1 UTEUZI WA WATAFITIWA

Tulikuwa na vikundi viwili tu vya watafitiwa ambao ni walimu na wanafunzi. Walimu hawa walikuwa ni wa shule za msingi na shule za upili. Tuliwahusisha walimu wanaofunza lugha ya Kiswahili na wale wasiofunza Kiswahili. Walimu katika shule tatu za upili na tatu za msingi waliweza kuwakilisha walimu wa shule zingine katika kaunti ndogo ya Kangema. Shule hizo zilikuwa katika maeneo tofauti katika kuanti ndogo hiyo. Tulifanya utafiti wetu katika shule zifuatazo: Shule ya Msingi ya Watuha, Shule ya Msingi ya Mukarara, Shule ya Msingi ya Kanyenya-ini, Shule ya Upili ya Watuha, Shule ya Upili ya Muguru na Shule ya Upili ya Wasichana ya Kiangunyi.

Tuliwahusisha wanafunzi kutoka katika shule zizo hizo. Wanafunzi wawili kutoka katika madarasa ya chini na wawili kutoka katika madarasa ya juu katika shule za msingi. Hiyo ni jumla ya wanafunzi 12 wa shule za msingi. Katika shule za sekondari, tuliwahusisha wanafunzi wanne kutoka katika kila shule. Tulimchagua mwanafunzi mmoja kutoka katika kila kidato. Jumla ya wanafunzi katika shule za sekondari walikuwa 12. Kwa hivyo, tulikuwa na jumla ya wanafunzi 24 ambapo 12 walikuwa wa shule za msingi na12 walikuwa wa shule za sekondari. Tulitumia jumla ya walimu18. Watatu kutoka katika kila shule. Kati ya hao watatu, mmoja alikuwa mwalimu asiyefunza Kiswahili na wawili walikuwa walimu wanaofunza lugha ya Kiswahili. Ili kupata wahusika hawa tulichukua sampuli rahisi isiyo na utaratibu maalum. Katika kikundi cha walimu wa Kiswahili tulichagua walimu wowote wawili wanaofunza Kiswahili katika kila shule. Kwa hivyo, jumla ya walimu watafitiwa wetu waliokuwa wanafunza Kiswahili walikuwa 12. Wale ambao hawakuwa wanafunza Kiswahili walikuwa 6.

### 1.9.2 UKUSANYAJI DATA

Katika kushughulikia kazi hii inayohusu matumizi ya lugha kimaongezi, utafiti wetu ulifanyiwa maktabani ambapo tulijiandaa kinadharia, kusoma tasnifu na vitabu vilivyoandikwa na wataalamu kuhusu swala hili kabla ya kuingilia utafiti zaidi huko nyanjani. Tulivitalii vitabu vinavyozungumzia juu ya sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu ili pamoja na ujuzi wetu wa kibinafsi wa lugha hii tuweze kutathmini na kubainisha ukiushi katika maongezi ya wahusika wa utafiti wetu. Tuliwahusisha watafitiwa 42. Ishirini na wanne walikuwa wanafunzi ambapo wengine 18 walikuwa walimu. Wahusika hawa wote walikuwa wazungumzaji wa lugha ya Kikuyu kama lugha yao ya kwanza. Tulichunguza lugha ya maongezi katika mazungumzo yasiyo rasmi na yaliyo rasmi shuleni. Tulikusanya data yetu bila watafitiwa wetu kujua.

Tuliamua kuwashughulikia watafitiwa wachache ili tuweze kufanya utafiti wetu kikamilifu zaidi badala ya kuwahusisha watu wengi na labda tukose wakati wa kutosha kuwashughulikia kikamilifu. Idadi hii ilituwezesha kufanya utafiti wa maongezi yao katika miktadha mbalimbali ambayo ilitupa data mwafaka kwa ajili ya kazi hii.

Ili kuweza kuyapata mazungumzo, tulitumia kinasa sauti kilichokuwa kimefichwa na kukifungulia tu tulipotaka kuinasa sauti ya mzungumzaji. Tulitumia pia rununu kufanyia kazi hii. Tulihakikisha kuwa tunafanya hivi katika mazingira yasiyo na kelele.

Tuliandika maongezi kama yalivyotamkwa hasa pale ambapo ilikuwa vigumu kutumia kinasasauti hasa darasani. Mazungumzo tuliyoyanasa ni yale yaliyotolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa.

### 1.9.3 UCHANGANUZI WA DATA

Baada ya kurekodi na kuyaandika maongezi hayo kitabuni, tuliyabaini na kuyachanganua makosa yaliyoko huku tukijikita katika makosa ya kimofosintaksia. Tulitumia utaratibu wa kimaelezo. Hatimaye tulifanya tathmini yetu kuhusiana na utafiti tulioufanya kwa kuutolea mapendekezo au maoni yetu.

# SURA YA PILI

# KANUNI ZA LUGHA YA KISWAHILI KIMOFOSINTAKSIA

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutaangalia ni nini maana ya lugha kwa kuwarejelea wanaisimu mbalimbali. Kisha tutaona lugha sanifu ni gani kulingana na wanalugha kadhaa. Tutaangalia ni kitu gani kinachohitajika ili lugha isemekane kuwa ni sanifu. Katika kuangalia makosa yanayotokana na matumizi ya lugha katika jamii, tuliona ni muhimu kwanza tuweze kuifafanua kwa ufupi dhana hii ya lugha.

## 2.1 LUGHA

Tutaanza kwa kusema kwamba, lugha ni dhana au hoja ambayo imewahi kujadiliwa na kufafanuliwa na wanalugha kwa namna mbalimbali. Dhana ya lugha ni telezi mno kwani kila maelezo yanayotolewa yanaacha nafasi ya kupatikana kwa ufafanuzi badalia wa kuwasilisha jambo lilo hilo. Hivi ni kusema kwamba tunaweza kutoa maelezo ya lugha ni nini kwa kutumia njia mbalimbali.

Mweri (2010) anasema kuwa binadamu huzaliwa katika mazingira fulani ambamo huingiliana na binadamu wengine kwa kupokea au kupeleka ujumbe. Hali hii ya kuupitisha ujumbe au fikra kutoka kwa binadamu mmoja hadi mwingine huitwa mawasiliano. Anaendelea kusema kuwa njia tunayotumia kuwasilisha ujumbe au fikra ili kuwasiliana ni njia ya ishara. Ishara hizi zinaweza kutumia hewa tunayovuta hadi mapafuni kutokea kinywani au puani. Ishara zinazotolewa hivi huitwa ishara za sauti. Ishara hizi hutumiwa katika mawasiliano ya kuzungumza au lugha ongezi.

Ishara zinazotumiwa katika mawasiliano, zikiwemo ishara za sauti na ishara zitumiwazo katika lugha-ishara zote hujulikana kama lugha, ikiwa zina mambo fulani muhimu yanayokubaliwa na wasomi katika sayansi ya lugha yaani isimu.

Hughes (1962) anasema kwamba lugha ni mfumo wa ishara za sauti nasibu ambazo kwazo jamii fulani huwasiliana. Naye Tradgil (1974) anafasili lugha kama mfumo wa

sauti nasibu zinazotumiwa katika mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake.

Chomsky (1957) akinukuliwa na Obuchi na Mukhwana (2010) naye anasema kuwa lugha ni seti ya sentensi (zenye ukomo au zisizo na ukomo), na kila moja ikiwa na urefu fulani na ikiwa imeunda seti za elementi ambazo zina ukomo wa idadi.

Furgasson (1969) anaeleza lugha kama tukio la kijamii.

Sapir (1921) naye anaeleza lugha kama mfumo ambao mwanadamu hujifunza ili autumie kuwasilishia mawazo, maono na mahitaji. Mfumo huu hutumia ishara ambazo hutolewa kwa hiari.

Kamusi ya TUKI (1990) inasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana.

Chomsky (1970) akinukuliwa na Obuchi na Mukhwana (2010) anabainisha lugha kama elementi ya kiakili ambayo mtu hupitia kwa kujifundisha, na elementi hii hutumiwa na mzungumzaji pamoja na msikilizaji. Chomsky vilevile anazungumzia muundo wa nje wa lugha, kwa maana ya mkusanyiko wa sentensi zinazoeleweka pasina kurejelea sifa za kimuktadha.

Mghambi (1991) anasema kuwa lugha ni tukio la kijamii. Katika jamii yenye kuzungumza lugha tofautitofauti na yenye tamaduni mbalimbali hutokea hali ya kuathiriana kwingi. Athari hizi hutokea katika viwango tofautitofauti. Kwa mfano, katika hali ya mgusano katika lugha, hutokea ukopaji na ukopeshaji wa msamiati na pengine pia hutokea mabadiliko ya kisauti. Ni katika hali hii ambapo wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili huenda wakadhihirisha athari za lugha zao za kwanza. Hii ndiyo sababu tunaweza kusikia baadhi ya watu wakisema kuwa fulani anaongea 'Kiswahili cha Kidholuo' au mwingine anasema kuwa fulani anaongea 'Kiswahili cha Kimeru.' Mahali popote lugha inapotumiwa na watu wengi, huibuka matumizi ya lugha kwa namna

tofautitofauti ambapo tunapata lugha za 'kimtaa' ambazo yamkini huwa na makosa mengi dhidi ya lugha sanifu.

Kutokana na fasiri hizi zilizotolewa na wataalam hawa, ni wazi kwamba, lugha ni mfumo wa sauti unaotumiwa na watu ili kuwasiliana. Mtu huipata lugha kwa kujifunza na kufunzwa. Kujifunza na kufunzwa huku kunaweza kufanyika kimakusudi au bila kuwa na hiari. Lugha mtu anayojifunza kwanza inakuwa msingi wa kujifunzia lugha ya pili na lugha nyingine zozote anazotaka kujifunza. Kwa hivyo lugha ya pili haina budi kuathiriwa na lugha ya kwanza kwa kiwango fulani. Aidha kumeibuka lugha isiyotumia sauti ambayo inatumia ishara pekee. Lugha hiyo inaitwa lugha ishara. Lugha hii pia hutumiwa kuwasiliana. Kwa muhtasari basi tunaweza kusema kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano baina ya watu kinachoweza kutumia au kutotumia sauti.

## 2.2 KISWAHILI SANIFU

Lugha sanifu ni sharti iwe na upatanisho mwafaka wa kisarufi unaoletwa na uwiano wa nomino ambayo huwa kiima katika kila tungo na kategoria zingine saba za maneno. Kwa kuwa sisi tulikuwa tukichunguza ukiushi wa kimaongezi katika viwango vya mofolojia na sintaksia, tulitumia uainishaji wa ngeli kisintaksia kwani uliweza kukithi mahitaji yetu yote ya utafiti wetu. Baada ya kuainisha ngeli kisintaksia, tulijadili vikundi saba vya maneno vilivyobaki na kutathmini uhusiano uliopo kati ya nomino na kila kikundi cha maneno. Tulipoona uhusiano huo basi tuliweza kujua lugha sanifu ni ipi na lugha iliyo na ukiushi wa kanuni ni ipi.

Lugha sanifu ni aina ya lugha inayotumika katika maandishi, inayofunzwa darasani na kufunza wageni wanaotaka kuijua lugha fulani. Haya ni kwa mujibu wa Mghambi (1991). Naye Trudgil (1974) anasema kwamba lugha sanifu ni aina ya lugha inayozungumzwa na wasomi, kutumika katika vyombo vya habari na katika hali nyingine kama hizo. Sisi tunaipinga hoja hiyo kwani baadhi ya wasomi hufanya makosa wanapozungumza. Watangazaji vilevile hukiuka kanuni za Kiswahili sanifu wanapoitumia lugha ya Kiswahili. Maoni yetu ni kwamba lugha sanifu ni aina ya lugha

inayostahili kuzungumzwa na wasomi na watangazaji katika vituo vya radio na televisheni na inayofuata kanuni zinazokubalika na wanaisimu.

Lugha sanifu ni lugha iliyowekewa taratibu, kaida na kanuni za matumizi na wanaisimu waliokubaliana kufanya hivyo kwa kutumia taratibu zilizoko katika tajriba ya kila mtumiaji stadi wa lugha hiyo hivi kwamba anapozikiuka kanuni hizo, mjuzi wa lugha ya Kiswahili sanifu ataelewa wazi kwamba pamefanyika makosa. Madai haya ni ya Halle na Steven (1964). Tukifuata mkabala huu wa mawazo basi, tunaweza kusema kuwa Kiswahili sanifu ni kile kinachofuata kanuni na kaida tulizozijadili hapo juu.

Juhudi za kusanifisha lugha ya Kiswahili zilianza mnamo mwaka wa 1925 wakati Gavana wa Tanganyika wakati huo alipoita mkutano huko mjini Dar es Salaam ili wazungumze kuhusu elimu. Haja ya kuchagua lugha moja ya Kiafrika katika Afrika Mashariki ilipendekezwa na Kiswahili kikachukua nafasi hiyo.

Mnamo mwaka wa 1928, washiriki kutoka Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar walikutana mjini Mombasa kushauriana juu ya lugha ya Kiswahili. Pakaundwa kamati ya lugha ya Kiswahili iliyojulikana kama 'Interterritorial Language Committee' mnamo mwezi wa Januari mwaka wa 1930. Baadhi ya kazi za kamati hiyo zikawa ni kuunda Kiswahili sanifu.

Lahaja ya Kiunguja iliteuliwa kwani ilidaiwa kuwa lahaja ya Kiswahili iliyokuwa imeenea sana katika Afrika Mashariki. Kamati hiyo baadaye iliunda kamati nyingine ndogo ya uandikaji wa vitabu vya aina moja ili kuepusha maandishi tofautitofauti. Kamati hii iliitwa 'Central Publishing Committee.' Kamati hiyo pia ilijishughulisha na uandikaji wa kamusi ya Kiswahili-Kingereza na Kiingereza-Kiswahili. Hizi zote zilikuwa juhudi za kutaka kuunganisha lugha ili kuwe na lahaja moja ya Kiswahili sanifu itakayotumika. Juhudi hizo zilizaa matunda kwani hivi sasa, Kiswahili hutumika katika sekta zote za kiuchumi nchini Kenya. Aidha, Kiswahili hutumika katika nchi zingine barani Afrika kama vile Msumbiji, Bukini, Tanzania, Rwanda, Burudi na Visiwa vya Ngazija.

Ili lugha yoyote iwe sanifu, haina budi kuwa na uwiano wa kisarufi unaoletwa na upatanisho mwafaka wa ngeli na aina zote za maneno katika lugha hiyo. Ngeli za maneno ndizo uti wa mgongo wa sarufi ya Kiswahili. Kwa hakika, asiyejua ngeli na matumizi yake asijidai anajua Kiswahili. Ngeli hizi hata hivyo haziwezi kufanya kazi kikamilifu bila kutumiwa pamoja na maneno mengine ya lugha ya Kiswahili katika kiwango cha sintaksia na semantiki. Kwa hivyo hatuna budi kuziorodhesha ngeli za Kiswahili kwa kuutumia mtazamo wa kisintaksia kwani ndio utakaotufaa zaidi katika utafiti wetu. Uainishaji huu hutumia viambishi vipatanishi ambavyo ndivyo tunahitaji katika utafiti wetu.

Kwa kweli, usanifu au ukiushi wa kanuni za lugha kiisimu au hata kifasihi hutegemea kwa kiwango kikubwa jinsi mzungumzaji anavyooanisha ngeli za nomino na aina zingine za maneno katika tungo.

## 2.3 DHANA YA UKIUSHI

Kwa mujibu wa Mghambi (1991), neno **ukiushi** linatokana na kitenzi **'kiuka'.** Neno 'kiuka' lina maana ya **'fanya isivyostahili yaani vunja sheria.'** Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kwamba maana ya kukiuka ni **'kufanya makosa.'** Ni dhahiri shahiri kwamba lugha yoyote ile ina kanuni na kaida zake. Lugha ya Kiswahili aidha ina sheria zake zinazohusu muundo na sarufi yake. Maingiliano yoyote yanayoathiri lugha kimuundo, kisarufi na hata kimsamiati ambayo yanazivunja sheria za lugha hiyo ni ukiushi wa kimatumizi.

Ukiushi unaweza kuwa wa matumizi ya sauti na miundo ya maneno ya lugha ya kwanza katika lugha ya Kiswahili. Mzungumzaji anafanya hivyo kwa kutojua kuwa lugha hutofautiana kimatamshi. Lugha zingine huwa na sauti ambazo hazipatikani katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano sauti /l/ na /z/ zinapatikana katika lugha ya Kiswahili lakini hazipatikani katika lugha ya Kikuyu. Mifano ya sentensi na maneno tutakayotoa yataeleza kwa mapana na marefu makosa yanayosababishwa na uchukulizi katika sura ya tatu.

Tutazungumzia ukiushi katika viwango viwili ambavyo ni kile cha mofolojia na cha sintaksia.

## 2.4 NGELI ZA NOMINO ZA KISWAHILI

### 2.4.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Mgullu (1999:48), istilahi 'ngeli' imechukuliwa kutoka lugha ya Kihaya kutoka nchini Tanzania. Katika lugha hiyo, neno ngeli humaanisha aina ya kitu. Obuchi na Mukhwana (2010) wanasema kuwa ngeli ni namna ya kuweka nomino katika makundi yanayowiana au yanayofanana. Wanaendelea kusema kuwa ngeli ni kundi la nomino za aina moja na hujumuisha makundi ya nomino ambapo kundi moja la nomino zilizo na upatanisho wa kisarufi unaofanana huwekwa pamoja. Kulingana nao, kila ngeli huwa na viambishi vya umoja na vile vya wingi vinavyofanana au kuelekeana. Kwa hivyo, kwa maoni yao ngeli ni jamii ya nomino zenye mabadiliko ya aina moja ya viambishi vya umoja na vya wingi vinavyoleta upatanisho wa kisarufi wa aina moja kwenye vitenzi, vivumishi na pia viwakilishi.

Nayo Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) inaeleza kuwa ngeli ni utaratibu wa taaluma ya sarufi ya lugha katika kupanga aina za majina (nomino) k.m ki-, vi- , ma-, n.k. Mgullu (1999) anaipinga kauli hii kwa kusema kuwa ngeli ni kundi la nomino za aina moja na si ule utaratibu wa kupanga nomino katika makundi.

TUKI (1990) nao wanaeleza kuwa ngeli ya nomino ni kundi moja la majina yaliyo na upatanisho wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana. Fasili hii inaweka pamoja vigezo viwili yaani kigezo cha kisintaksia na kile cha kimofolojia na kuwacha nje kigezo cha kisemantiki kinachoziainisha nomino kwa kuzingatia maana za nomino. Mgullu (1999) anasema kuwa kigezo hiki cha kisemantiki kina uwezo mdogo sana wa kutumiwa kuainisha nomino za Kiswahili katika ngeli kwani kinaweza kutumiwa kuainisha ngeli moja tu ambayo ni ile ya viumbe hai. Hata hivyo, kigezo hiki hutumiwa wakati wa kuzigawa nomino katika aina mbalimbali.

## 2.5 UAINISHAJI WA NGELI KISINTAKSIA

Uainishaji huu huziainisha ngeli za nomino kwa kuzingatia uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo. Unatumia vipatanishi vya nomino. Matei (2008) aliuita uainishaji huu uainishaji wa ngeli kwa kutumia vimbishi vya upatanisho. Obuchi na Mukhwana (2010) wanasema kuwa uainishaji huu unalenga katika kusuluhisha baadhi ya matatizo yaliyosababishwa na uainishaji wa ngeli za nomino kimofolojia uliozingatia viambishi awali vya nomino. Iribemwangi (2008) anasema kuwa kigezo hiki cha uainishaji kinaweza kuyashughulikia matatizo mengi ya kiuainishaji. Hii ni kwa sababu uainishaji huu hutilia mkazo zaidi suala zima la uamilifu badala ya umbo au muundo wa nomino husika. Matatizo yanayoweza kushughulikiwa ni kama yafuatayo:

a) Nomimo zote zinazowahusu wanadamu na wanyama huwekwa katika kundi moja la nomino kinyume na zilivyoainishwa awali.

Nomino zimeainishwa kiukubalifu. Nomino kama vile '**magonjwa'** , **'mapishi'** , **'malezi '**, na **'maovu'** zimeainishwa kwa njia iliyo sawa. Mwanzoni, nomino hizi ziliingizwa katika ngeli ya **'u'**, ingawa vivumishi, vitenzi na viwakilishi vilivyohusishwa nazo havisheheni umbo **'u'.**

b) Mtafaruku uliohusu vibainishi ngeli mbalimbali vya majina na vile vya vipatanishi, uliweza kusuluhishwa.

Uainishaji wa kisintaksia hutumia vipatanishi vya nomino. Vipatanishi ni maumbo maalum ambayo huwekwa katika maneno mengine wakati nomino fulani inapozungumziwa. Vipatanishi hivi huwekwa hasa katika vitenzi, vivumishi au viwakilishi.

Mohammed (2001) anasema kuwa uainishaji wa ngeli kisintaksia huzingatia vitambulishi vya kisarufi vinavyoitwa viambishi –mtenda. Viambishi hivi ni pamoja na viambishi vya viwakilishili, vya vitenzi na vya vivumishi. Viambishi vyote hivi hurejelea nomino. Nomino ndizo hutawala tungo na viambishi vyote vitumiwazo. Katika kuziainisha ngeli hizi, baadhi ya wanaisimu hutumia nambari tofauti katika kuorodhesha umoja na wingi wazo. Wengi hawaweki/hawatumii nambari kwa umoja na wingi bali huipa jozi moja nambari moja.

Sisi tutautumia mtindo huo wa kuipa jozi moja nambari moja. Kisintaksia, wanaisimu wameibuka na ngeli kumi na mbili ambazo zinadhihirika ifuatavyo. Uainishaji huu ni kwa mujibu wa Mgullu (1999).

### 2.5.1 Ngeli ya A –WA

Hii ni ngeli ya majina ya viumbe vyenye uhai kama vile watu, wadudu, ndege, miungu, malaika, wanyama wa kufugwa, wanyama wa majini na wale wa mwituni. Mifano ya majina; mkulima, nzi, heroe, chui, ng'ombe, papa na panya. Mifano katika sentensi:

(i) Ngombe ***a***lichungwa. - Ngombe ***wa***lichungwa.

(ii) Chui yule ***a***liniuma. - Chui wale ***wa***liniuma.

### 2.5.2 Ngeli ya U-I

Ngeli hii huwakilisha vitu visivyokuwa na uhai isipokuwa mimea. Aghalabu vitu hivyo vyote vilivyo katika ngeli hii havina damu. Majina yote ya ngeli hii huanza kwa mofimu **{m}** katika hali ya umoja na **{mi}** katika hali ya wingi. Mifano ya nomino ni kama vile, **mfupa –mifupa**, **mkate –mikate, mjeledi –mijeledi, mto –mito** n.k. Mifano katika sentensi ni kama ifuatayo:

(i) Mto ***u***mefurika. – Mito ***i***mefurika.

(ii) Mkebe ***u***navuja. – Mikebe ***i***navuja.

### 2.5.3 Ngeli ya LI-YA

Ngeli hii hujumuisha majina ya viumbe visivyo na uhai pamoja na nomino zilizo katika hali ya ukubwa. Majina katika ngeli hii huchukua miundo mbalimbali. Kuna yale ambayo huchukua mofu **{ji}** katika hali ya umoja na mofu {**ma**} katika hali ya wingi. Mifano; **jicho –macho**, **jiwe – mawe**, **jiko –majiko**.

Muundo mwingine ni ule unaochukuwa mofu kapa **{Ø}** katika hali ya umoja na mofu **{ma}** katika hali ya wingi. Mifano: **rinda –marinda**, **shati – mashati**, **embe – maembe**.

Majina katika hali ya ukubwa vilevile hupatikana katika ngeli hii. Mifano:

(i) Tunda ***li***taliwa na mtoto. - Matunda ***ya***taliwa na watoto.

(ii) Jiko ***li***mewaka. – Majiko ***ya***mewaka.

### 2.5.4. Ngeli ya KI- VI

Hii ni ngeli ya vitu visivyo na uhai. Nomino hizo huanza kwa mofu **(ki-)** au **(ch-)** katika hali ya umoja na mofu **(vi-)** au **(vy-)** katika hali ya wingi. Aidha, ngeli hii hujumuisha majina ya vitu vilivyo katika hali ya udogo. Kuwa katika hali ya udogo humaanisha kitu au kiumbe huwa kidogo kuliko ilivyo kawaida yaani kidogo sana. Mifano ya majina ni kama ifuatayo:

(i) kiti – viti (hali ya kawaida)

(ii) kijitoto—vijitoto (hali ya udogo)

**Mifano katika sentensi:**

(i) Kitabu changu ***ki***liraruka. – Vitabu vyetu ***vi***liraruka.

(ii) Kijito hicho ***ki***takauka. – Vijito hivyo ***vi***takauka.

### 2.5.5 Ngeli ya I-ZI

Majina katika ngeli hii hayana mofu ya umoja wala wingi. Wingi au umoja wa nomino katika ngeli hii huthihirika zinapotumika katika sentensi. Mofu ya umoja au wingi huwa dhahania au kapa.

Majina yote ni ya vitu visivyo na uhai.

**Mifano ya majina ni kama vile:-**

(i) shilingi – shilingi

(ii) pete – pete

**Mifano katika sentensi:**

(i) Nguo yangu ***i***lioshwa. – Nguo zetu ***zi***lioshwa.

**(ii)** Meza ya mwalimu ***i***lipakwa rangi. - Meza za walimu ***zi***lipakwa rangi.

### 2.5.6 Ngeli ya U – U

Ngeli hii hujumuisha majina yenye kiambishi '**u**' katika hali ya umoja na kiambishi '**u**' katika hali ya wingi majina hayo ni ya vitu visivyoweza kuhesabika. Kwa mfano:uvivu,

ugali na uji, Aidha hujumuisha majina yasiyoanza kwa kiambishi '**u**'. Majina hayo ni ya nomino dhahania ambazo zinasimamia vitu visivyoonekana wala kushikika. Mifano ni kama werevu, wizi, wema, wembamba na ujinga.

Aghalabu maneno haya huanza kwa fonimu **/w/.**

**Mifano katika sentensi**

(i) Ujinga wake ***u***limfanya aanguke mtihani. - Ujinga wao ***u***liwafanya waanguke mitihani.

(ii) Wema wangu ***u***menisaidia. –Wema wetu *u*metusaidia.

### 2.5.7 Ngeli ya U- YA

Hiki ni kikundi cha nomino zinazochukua kiambishi **'u'** katika hali ya umoja na **'ya'** katika hali ya wingi.

**Mifano ya majina:**

(i) uyoga – mayoga

(ii) ugonjwa – magonjwa

**Mifano katika sentensi:**

(i) Ugonjwa ***u***limuua Kamau. – Magonjwa ***ya***liwaua akina Kamau.

(ii) Uyoga ***u***naweza kuliwa. - Mayoga ***ya***naweza kuliwa.

### 2.5.8 Ngeli ya U- ZI

Ngeli hii hurejelea majina ambayo huchukua kiambishi **(u)** katika hali ya umoja na kiambishi **(zi)** katika hali ya wingi. Majina yenye silabi tatu au zaidi hubadilishwa kwa wingi kwa kutoa sauti ya kwanza **/u/.** Kwa mfano:

(i) **ukucha–kucha**

(ii) **ukuta-kuta**

Majina ya silabi mbili huongezwa **/ny/** katika hali ya wingi. Kwa mfano:

(i) **ufa – nyufa**

(ii) **waya – nyaya**

Kuna majina yanayoanza kwa herufi **'w'** katika hali yaumoja. Katika hali ya wingi, '**w**' hubadilika na kuwa '**ny'.** Mifano ya majina hayo ni;

(i) **wimbo- nyimbo**

(ii) **wia – nyia**

Baadhi ya majina huanza kwa herufi '**u**' katika hali ya umoja. Katika hali ya wingi, kiambishi hicho hubadilika na kuwa '**nj'.** Kwa mfano:

(i) **ujiti- njiti**,

(ii) **ujaka- njaka.**

Kuna baadhi ya majina yanayoanza kwa kiambishi '**u'** katika hali ya umoja na huwa yana silabi tatu. Kiambishi '**u'** hicho huondolewa na nafasi yake kuchukuliwa na '**m'** katika hali ya wingi. Mifano yamajina hayo ni:

(i) **Ubawa – mbawa**

(ii) **Ubao – mbao**

**Ifuatayo ni mifano katika sentensi.**

(i) Ukuta huo ***u***tabomolewa. - Kuta hizo ***zi***tabomolewa.

(ii) Uzi ***u***likatika. – Nyuzi ***zi***likatika.

### 2.5.9 Ngeli ya YA-YA

Hii ni ngeli ya vitu visivyoweza kuhesabika. Majina hayo huitwa nomino za wingi. Majina haya hayana umoja. Ngeli hii hujulikana kama ngeli ya vimiminwa. Majina haya yanapotumiwa pamoja na vivumishi, vivumishi hivi hujitokeleza na kiambishi awali **'ma'** ambacho hujidhihirisha kama **'me'** katika baadhi ya sifa k.v -eupe,-ekundu,na – eusi.

Mfano*: Maziwa **meupe** yananyweka.* Hatahivyo kiambishi ngeli katika vitenzi huwa ni **'ya'** katika hali ya umoja na wingi.

**Mifano ya majina:**

(i) maziwa – maziwa

(ii) maji – maji

Ngeli hii vilevile hujumuisha majina ya vitu vinavyoweza kuhesabika lakini haviwezi kudhihirika iwapo viko katika hali ya umoja ama wingi. Mifano ni: **makala, maktaba maskani, mastakimu, mazingira** na **mazingaombwe.**

**Mifano ya sentensi:**

(i) Maziwa ***ya***limwagika. - Maziwa **ya**limwagika.

(ii) Mafuta haya ***ya***nanukia. -Mafuta haya **ya**nanukia.

### 2.5.10 Ngeli ya I- I

Hii ni ngeli ya majina ya vitu visivyohesabika ambayo yanachukua viambishi ngeli **'i'** katika hali ya umoja na kiambishi ngeli hichohicho katika hali ya wingi. Baadhi ya vitu vinavyorejelewa na ngeli hii vinaweza kuonekana na kugusika lakini kuna baadhi ambavyo ni dhahania, yaani havionekani, havigusiki wala kushikika.

**Mifano ya majina ni kama vile: chai, petroli, kahawa, hewa** na **diseli.**

Nomino dhahania ni kama vile **furaha na huzuni**

**Mifano katika sentensi:**

(i) Furaha yake ***i***natuchangamsha. - Furaha yao ***i***natuchangamsha.

(ii) Petroli iliyonunuliwa ***i***litumika yote. -Petrol iliyonunuliwa ***i***litumika yote.

### 2.5.11Ngeli ya KU

Hii ni ngeli ya majina ya vitenzi. Majina hayo yote huanza kwa silabi '**ku**' na huchukua kiambishi ngeli '**ku**' kila mara.

Mifano; **kucheza, kuimba, kukimbia, kuingia, kutoka, kukimbia na kufurahisha.**

**Mifano katika sentensi:**

(i) Kucheza huko ***ku***nafurahsha. – Kucheza huko ***ku***nafurahisha.

(ii) Kucheka kwake ***ku***naudhi. – Kucheka kwao ***ku***naudhi.

### 2.5.12 Ngeli ya PA- KU – MU

Ngeli hii huitwa ngeli ya mahali. Maumbo **'pa''ku' 'mu'** hutegemea umbali au masafa au panapozungumziwa. Mahali '**hapa**' ni mahali panapodhihirika karibu na mzungumzaji.

Mahali '**humu**' ni mahali ndani ya kitu kama vile chungu, nyumba au shimo. Mahali '**huku**' ni mahali karibu na mzungumzaji kusikodhihirika.

**Mifano katika sentensi:**

(i) Mahali hapa ***pa***lifungwa na mjomba. — Mahali hapa ***pa***lifungwa na wajomba.

(ii) Chunguni humu ***m***na siafu wengi. – Chumbani humu ***m***na sifu wengi.

(iii)Nilimwona akilima ***ku***le shambani. –Nilimwona akilima ***ku***le shambani.

**2.5.13 Ngeli nyinginezo**

**2.5.13.1 Ngeli ya ZI-ZI**.

Mifano ya majina ni **nguvu**na **mbio.** Majina haya hayapatikani katika hali ya umoja**.** Mfano wa sentensi.

(i) Nguvu za tembo ***zi***naogopwa sana. - Nguvu za tembo ***zi***naogopwa sana.

(ii) Mbio hizo ***zi***liwavutia mashabiki wengi. – Mbio hizo ***zi***liwavutia mashabiki wengi.

**2.5.13.2 Ngeli ya VI-VI**

Ina jina moja ambalo halipatikani katika hali ya umoja –**vita**. Mfano wa sentensi. Vita ***vi***liiharibu nchi ya Rwanda. – Vita ***vi***liiharibu nchi ya Rwanda.

**2.5.13.3 Ngeli ya LI-LI**

Ngeli hii huwa na jina moja tu- '**jua**' ambalo huwa katika hali ya umoja pekee. Hii ni kwa sababu kuna jua moja tu na kwa hivyo hapana haja ya kuwa na wingi. **Mfano katika sentensi:** Jua ***li***liangaza asubuhi- Jua ***li***liangaza asubuhi.

**2.6 HITIMISHO**

Kama tulivyokwisha kutaja hapo awali, kuna njia tatu za uainishaji wa ngeli za Kiswahili. Uainishaji kisemanitiki, uainishaji kimolololojia na uainishaji kisintaksia kama tulivyofanya sisi. Ingawa uainishaji wa kwanza na wa pili ni muhimu, sisi hatuoni ukitusaidia katika utafiti wetu kwani takribani makosa yote tuliyonuia kufanyia utafiti wetu yamejumuishwa katika uainishaji huu wa kisintaksia. Hii ni kwa sababu majina yote ya Kiswahili yanapatikana katika mojawapo ya ngeli hizi. Aidha, upatanisho wa kisarufi

wa majina hayo vilevile umeelezwa katika uainishaji huu. Hivyo basi uainishaji huu ni toshelevu kabisa katika uchunguzi wetu.

## 2.7 AINA ZA MANENO

### 2.7.1 UTANGULIZI

Ili kuweza kufafanua na kuelezea kwa undani kabisa kuhusu lugha sanifu ya Kiswahili ilivyo, hatuna budi kuelezea makundi manane ya maneno ya Kiswahili na kuonyesha bayana jinsi yanavyoweza kutumika pamoja na nomino tulizokwisha zitaja huku tukionyesha kile tulichokuwa tukiita upatanisho wa kisarufi. Hatuwezi kuonyesha upatanisho wa kisarufi iwapo hatutaonyesha uhusiano wa kategoria zote za maneno katika tungo ili tuonyeshe sheria zinazotumika.Tulifanya hivi kwa kuonyesha viambishi vipatanishi vya kila ngeli ya majina. Kwa mkabala huu, tutaweza kujua sheria zinazoitawala kila ngeli ya majina. Baada ya kujua sheria na kaida zinazostahili kutumika katika lugha sanifu, basi tunaweza kutambua ukiushi wa kimofosintaksia kwa urahisi sana.

Kunazo aina nane za maneno ya Kiswahili ambazo ni nomino au majina, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, vielezi, viingizi (vihisishi), vihusishi na viunganishi. Sentensi huundwa kwa kutumiaaina mbalimbali za maneno. Aina hizi za maneno hupata kategoria yake kulingana na jumbe ambazo zinatumiwa kuwasilisha.

### 2.7.2 NOMINO

Haya ni majina yanayotaja vitu, viumbe, hali, mahali, vyeo, matendo, n.k. Nomino vilevile huitwa majina ingawa sisi tunaipendelea istilahi 'nomino'. Kiswahili kina nomino nyingi. Wanaisimu wamejaribu kuziainisha nomino hizo kisemantiki yaani wakizingatia maana kama ifuatavyo:

#### 2.7.2.1 Nomino za pekee/nomino halisi.

Nomino hizi hutaja vitu vya kipekee ambavyo ni mahususi kwani vipo vyenyewe tu hapa duniani Nomino hizi za pekee hutaja majina ya watu, milima, miji, mito, nchi, maziwa na bahari. Nomino hizi huwa hazina wingi. Huanza kwa herufi kubwa hata kama

zinapatikana katikati ya sentensi. Mifano: Njoroge, Mlima Kenya, Galana, Uhabeshi, Victoria na Pasifiki.

#### 2.7.2.2 Nomino za kawaida

Hizi ni nomino zinazotaja vitu vya kawaida ambavyo si vya pekee. Hutaja vitu ambavyo ni vingi hapa duniani. Zinaweza kuwa na umoja na wingi. Hata hivyo baadhi ya nomino za kawaida huwa na umoja tu au wingi tu. Majina haya hayaanzi kuandikwa kwa herufi kubwa kama yalivyo majina ya kipekee isipokuwa pale yanaanza sentensi. Nomino hizi hudhihirika kama mizizi isiyoambikwa viambishi ama vya awali au vya tamati.

Mifano ya nomino hizi ni:

(i) kalamu-kalamu

(ii) ng'ombe –ng'ombe

#### 2.7.2.3 Nomino za dhahania

Haya ni majina ya vitu vinavyofikirika tu kwani havionekani wazi au kushikika. Ni nomino za vitu tusivyoweza kuvishika, kuvionja wala kuvinusa. Vitu vinavyowakilishwa na nomino hizi havina umbo halisi. Vimo akilini tu na haviwezi kupimwa kwa njia yoyote ile. Mifano ni: wivu, wizi, urembo, upole, ukarimu, urafiki, uadui, wema, woga na mawazo.

#### 2.7.2.4 Nomino za wingi (vitu visivyohesabika)

Pamoja na vimiminwa, kuna nomino zinazoashiria vitu vingine visivyohesabika, k.v maudhui, makala, mawasiliano na maoni. Dhana ya wingi katika majina haya hudhihirika katika upatanisho wa kisarufi. Mifano ya vimiminwa ni maji, mafuta, maziwa, mate, manukato na marashi.

#### 2.7.2.5 Nomino za vitenzi–jina

Nomino hizi huhusu vitenzi. Huundwa kwa kuongeza kiambishi **ku-** cha unominishaji (uundaji wa nomino) kwenye mzizi wa kitenzi halisi (kitenzi cha kutenda) ili kukifanya nomino. Mifano, ***penda*** – ku*pend*a, ***soma*** – ku*som*a, ***ona***-ku***ona*** na **piga**-ku***piga.***

#### 2.7.2.6 Nomino za jamii

Hizi ni nomino ambazo zina vitu vingi ndani yake. Vitu hivi aghalabu huwa ni vya aina moja. Mifano ya nomino za jamii ni: kikosi, timu, thurea, kamati, jeshi, kikoa, genge na halmashauri.

#### 2.7.2.7 Nomino za mguso

Hizi zinarejelea vitu vinavyohisika kwa kutumia macho, mikono, pua, masikio na ulimi. Kwa hivyo ni vitu vinavyoweza kushikika, kunusika, kusikika, kugusika na kuonjeka. Mifano ni k.v maji, ugali, ugoro, maji, sukari na chumvi.

#### 2.7.2.8 Nomino ambatano

Hizi ni nomino ambazo ni muungano wa maneno mawili ambayo yanatumiwa kama nomino moja. Mifano: mwana + hewa→mwanahewa, bata + mzinga → batamzinga na mbwa+mwitu→mbwamwitu.

### 2.7.3 VIVUMISHI

Kivumishi ni neno au kundi la maneno yanayotoa maelezo zaidi juu ya jina au kiwakilishi chake. Mgullu (1999) anasema kuwa kivumishi ni neno ambalo hufafanua kitu, sifa, hali au tendo linalowakilishwa na nomino. Mifano:

*(i)* Nyumba ***kubwa***

*(ii)* Kiatu ***kichafu***

Kuna aina zifuatazo za vivumishi:

#### 2.7.3.1 Vivumishi vya sifa.

Hivi hutoa maelezo yanayotupa wasifu wa mtu, jambo au kitu fulani. Hujibu swali; cha aina gani? Enye tabia gani? Enye hali gani? Mifano ni mzuri, chema na vyeusi.

#### 2.7.3.2 Vivumishi vionyeshi (viashiria).

Vivumishi hivi hutumika wakati wa kuonyesha nomino. Hugawika katika vikundi viwili ambavyo ni vivumishi vionyeshi vya karibu na vivumishi vionyeshi vya mbali. Mifano

ya vivumishi vionyeshi vya karibu ni **huyu**, **hiki** na **hili.** Mifano ya vivumishi vionyeshi vya mbali ni **huko, kile** na **hicho. Mifano:** mtoto ***huyu,*** kiatu ***hiki,*** jani ***hili,*** mahali ***huko***

### 2.7.3.3 Vivumishi viulizi.

Hivi ni vivumishi ambavyo hutumiwa pamoja na nomino ili kuuliza juu ya nomino hiyo. Mizizi ya vivumishi viulizi vinavyotumika sana ni: {**gani**}, {**ngapi**} na {**pi**}.

### 2.7.3.4 Vivumishi virejeshi.

Haya ni mafungu ya maneno ambayo hufafanua nomino kwa kuirejelea. Vivumishi hivi huundwa kwa faridi **'o'**-rejeshi na kirejeshi **'amba'. Mifano:** mtoto ali*ye*enda, mtoto ***ambaye*** alienda.

### 2.7.3.5 Vivumishi vya 'a' unganifu.

Vivumishi hivi hufafanua nomino. Ni virai vihusishi ambavyo huundwa kwa kihusishi **'a'** unganifu na kawaida huandamana na nomino na pengine maneno mengine kuunda kundi la maneno ambalo huitwa kirai husishi. Mifano: Kuku ***wa*** baba, kikombe ***cha*** chai na yai ***la*** kuku.

### 2.7.3.6 Vivumishi vimilikishi.

Vivumishi hivi hueleza umilikaji. Hufafanua nomino kwa kutaja nafsi ambayo inaimiliki. Nafsi huwa tatu ambazo ni: nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Vimilikishi vya nafsi ya kwanza ni **–angu** na **–etu.** Vya nafsi ya pili ni **–ako** na **–enu** na vya nafsi ya tatu ni **–ake** na **–ao**. Mifano ya nomino zilizovumishwa ni: mtoto ***wangu,*** fulana ***zetu,*** shati ***lako,*** magari ***yenu na*** shule ***yake.***

### 2.7.3.7 Vivumishi vya idadi.

Vivumishi hivi hueleza zaidi kuhusu nomino kwa kuonyesha idadi au kiasi chake. Kuna vivumishi vya idadi kamili kama vile; ng'ombe ***watatu***, nguo ***mbili*** na vikombe ***vinne.*** Vilevile kuna vivumishi vya idadi isiyodhihirika. Mifano: karatasi ***nyingi***, mikono ***michache*** na nyumba ***kadhaa.***

### 2.7.3.8 Vivumishi visisitizi

Vivumishi hivi huvumisha nomino kwa kutilia mkazo habari zake. Kimsingi, vivumishi visisitizi huundwa kwa kurudiarudia vivumishi viashiria. Mifano: mtoto ***huyu huyu***, kikapu ***hiki hiki,*** mahali ***hapa hapa*** na shule ***hii hii.***

### 2.7.3.9 Vivumishi vya majina

Haya ni maneno ambayo kwa kawaida huainishwa kama nomino lakini huweza kuwa na uamilivu wa vivumishi. Mfano: Mwanamke ***mzee*** huheshimiwa na wengi. Msichana ***bikira*** hawezi kupata miba.

### 2.7.3.10 Vivumishi vya pekee

Vivumishi hivi huitwa vivumishi vya pekee kwa sababu kila mojawapo huwa na maana yaka mahususi na vilevile upatanisho wake maalum wa kisarufi kulingana na ngeli ya nomino inayovumishwa. Vivumishi vya pekee huwa vitano ambavyo ni: **-ote,-o-ote, -ngine, -enye** na **–enyewe.** Huvumisha nomino hivi: mchanga ***wote***, mwalimu ***yeyote***, darasa ***jingine***, tarakilishi ***yenye,*** na kiberiti ***chenyewe.***

## 2.7.4 VIWAKILISHI

Kiwakilishi ni neno/fungu la maneno/kiambishi ambacho hutumiwa badala ya nomino. Kiwakilishi huchukua nafasi ya nomino/kirai nomino katika sentensi. Katika huku kuwakilisha, kiwakilishi huwa ni kibadala cha nomino. Hufanya kazi ya nomino, na kinapotumiwa, nomino haitumiwi hapo hapo. Hata hivyo, ni muhimu kutaja kwamba nomino na kiwakilishi chake huweza kutokea pamoja katika mfululizo wa maelezo. Kwa mfano:

Mjomba aliondoka mapema, *yeye* hakutaka kuchelewa.

**'Yeye'** katika sentensi hii ni kiwakilishi cha nomino '**mjomba**,' ambayo ndiyo kitangulizi cha kiwakilishi *yeye.*

Kiwakilishi kimoja huweza kutumiwa kuwakilisha zaidi ya nomino moja tangulizi, kama katika mfano ufuataao:

Waithera na Njoki wamestaafishwa. ***Wao*** ndio walikuwa wa mwisho kuajiriwa. (hapa, kiwakilishi ***'wao'*** kinawakilisha nomino '**Waithera**' na **'Njoki'**).

Kiwakilishi kinapotumiwa katika mfululizo wa maandishi hupata maana yake (hueleweka) kutokana na nomino tangulizi (inayotangulia) au fuatilizi (inayofuata). Kwa mfano:

a) Kanyuira atawauza kuku wengine. ***Hawa*** wameanza kuzeeka. (hapa, kiwakilishi **'hawa'** kinaeleweka kwa kurejelea nyuma kwa mifugo). ***'Hawa'*** linasimama pahala pa ***'mifugo.'*** '**Hawa**' likitokea peke yake katika maandishi, hatutajua kama ni kiwakilishi cha mifugo au cha watu.

b) **Ndugu yangu** ameanzisha biashara humu. ***Yeye*** ni mfanyi biashara mashuhuri. (hapa, kiwakilishi ***' yeye'*** kinapata maana tunaporejelea nyuma kwa ' **ndugu yangu'**).

Viwakilishi husimama badala ya:

(i) **Majina ya watu/wanyama**. Kwa mfano: badala ya kusema, 'Mutua ameondoka.' Unaweza kusema '*Yeye* ameondoka.'

(ii) **Nomino inayomilikiwa**, kwa mfano: ***Lake*** limeuzwa. Badala ya tunda lake limeuzwa.

(iii) **Nomino anayoashiriwa**, kwa mfano: ***Zile*** ni zao, zangu ni zile. Badala ya: Nguo zile ni zao, zangu ni zile.

(iv) **Nomino inayorejelewa,** kwa mfano: ambacho kilipatikana ni chake. Badala ya: Kitambaa kilichopatikana ni chake.

(v) **Nomino yenye sifa/mkao fulani,** kwa mfano: **Wema** husifiwa na wengi. Badala ya: Watu wema husifiwa na wengi.

(vi) **Nomio zilizo na uhusiano fulani,** kwa mfano: **La kuvunda** halina ubani. Badala ya: Tunda la kuvunda halina ubani.

(vii) **Nomino zenye idadi fulani,** kwa mfano: **Wengi** hawakuipenda katiba hiyo. Badala ya: Wakenya wengi hawakuipenda katiba hiyo.

(viii) **Nomino inayouliziwa 'habari zake,'** kwa mfano:

(i) Unahitaji **mangapi?** Badala ya: Unahitaji magunia mangapi?

(ii) **Kipi** kilichoundwa upya? Badala ya: Chuma kipi kilichoundwa upya?

(ix) **Nomino ambayo habari zake zinasisitizwa,** kwa mfano:

(i) **Chenye** kimeoza. Badala ya: Kiazi chenyewe kimeoza.

(ii) Nataka **lilo hilo**. Badala ya: Nataka embe lilo hilo.

(x) **Ngeli ya nomino inayowakilishwa,** kwa mfano: Nyumba hiyo imejengwa upya.

Mifano zaidi:

(i) **Watano** walipandishwa cheo.

(ii) **Mwenye** shamba ameliuza.

**Ni muhimu kukumbuka kwamba:**

(i) Kiwakilishi huweza kuwa neno moja tu, kwa mfano: Ninaandika.

(ii) Huweza kuwa kiambishi, kwa mfano ***'ki'*** katika: *Kilipatikana.* Hapa kiambishi **'ki'** kinawakilisha nomino yoyote katika ngeli ya ki-vi, katika hali ya umoja.

Mifano:

(i) Mimi nataka **ambacho** uliniahidi.

(ii) **Cha** Mwangi kimetengenezwa vyema.

- Huweza kuwakilisha zaidi ya nomino mbili. Kwa mfano:

***Munyao na Ombanga*** wamepata wadhifa wa uwaziri. Wao ni wafanya kazi waadilifu. (***'wao'*** inawakiliisha **Munyao na Ombanga**.)

- Vipo baadhi ya viwakilishi ambavyo havirejelei vitu maalum; vinawakilisha kwa jumla/ kitu chochote. Kwa mfano, tunaposema 'Wote wametosheka.' kiwakilishi ***wote*** hakionyeshi mtu maalum. Labda kinasimama badala ya watu kwa jumla. Haijulikani ni yupi katika kundi hilo.

Viwakilishi vya aina hii havina nomino tangulizi maalum kwa sababu vitu/watu ambao vinawakilisha havijulikani wazi.

Havijatengwa wala kudhihirishwa wazi. Mathalani, unaposema***'chochote'*** kinatumika.' kiambishi ***chochote*** hakirejelei kifaa maalum kama vile kiti, bali kinawakilisha nomino yoyote (katika ujumla wake) katika ngeli ya KI- VI umoja. Ni kiwakilishi kisicho mahususi. Hata hivyo, unaposema *kile kitanifaa,* ***kile*** ni kiwakilishi mahsusi kwa sababu kinarejelea kitu ambacho kinaonyeshwa kwa kidole. Tazama mifano zaidi:

a) ***Kila mtu*** atanufaika kwa mradi huo.

b) ***Wengine*** watatumiwa mwaliko.

c) ***Baadhi*** walipeperusha bendera.

Kuna aina zifuatazo za viwakilishi:

#### 2.7.4.1 Viwakilishi nafsi

Viwakilishi nafsi husimama mahali pa nomino ambazo ni majina ya watu/wanyama. Haya ni maneno mazima yanatumiwa badala ya majina ya watu /wanyama. Hugawika katika makundi matatu:

**i. Vya nafsi ya kwanza**

Hivi huwa ***'mimi'*** katika umoja na ***'sisi'*** katika wingi. Kwa mfano:

***Mimi*** nimepanda mche- ***Sisi*** tumepanda miche.

**ii. Vya nafsi ya pili**

Hivi huwa ***'wewe'*** katika umoja na ***'nyinyi'*** katika wingi. Kwa mfano:

***Wewe*** umepandishwa cheo- *Nyinyi* mmepandishwa vyeo.

**iii. Vya nafsi ya tatu**

Hivi huwa ***'yeye'*** katika umoja na ***'wao'*** katika wingi. Kwa mifano:

*Yeye* ni mhandishi- ***Wao*** ni wahandishi.

Viwakilishi nafsi huweza kuwa na uamilifu wa watenda. Kwa mfano, katika **'Wao** walipika chakula kitamu,' '***wao'*** ni watenda.Ndio wanaofanikisha upikaji wa chakula kitamu. Vilevile, viwakilishi nafsi huweza kuwa yambwa (watendwa). Kwa mfano, katika sentensi "*Nyinyi* mlipikiwa uji mtamu," '***nyinyi'*** ni watendewa – ndio wanapokea kitendo cha kupikiwa, kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

#### 2.7.4.2 Viwakilishi nafsi viambata/vitegemezi

Hivi ni viambishi vinavyoambikwa kwenye mzizi wa kitenzi kuwakilisha nomino ama kiwakilishi huru kilichotajwa awali, ama ambacho hakikutajwa awali. Kwa mfano:

(i) Irungu ***a***licheza mchezo wa kupendeza.

(ii) Wanafunzi ***wa***liandika barua kwa kalamu.

Katika sentensi hizi, viambishi **'a'** na **'wa'** ni viwakilishi nafsi viambata. Vinasimama mahali pa nomino 'Irungu' na 'wanafunzi'. Sawa na viwakilishi nafsi huru, viwakilishi nafsi viambata huweza kuwa watenda au yambwa. Kwa mfano:

**Mtenda**

| Nafsi | umoja | wingi |
|---|---|---|
| Kwanza | ni | tu |
| Pili | u | m |
| Tatu | a | wa |

Mifano katika sentensi:

(i) Mimi ***ni***nasoma habari. Sisi ***tu***nasoma habari.

(ii) Wewe ***u***nafyeka nyasi. Nyinyi ***m***nafyeka nyasi.

(iii)Mkulima ***a***takulimia shamba. Wakulima ***wa***tawalimia shamba.

Ni muhimu kutaja kwamba kipo kiwakilishi nafsi ambacho husimama mahali pa mtenda ambaye pia ni mtendwa/mtendewa. Hiki ni kiambishi ***'ji'*** cha kujirejelea. Kwa mfano:

(i) Njeru ata***ji***palia makaa.

(ii) Wao wata***ji***andikia barua.

**2.7.4.3 Viwakilishi vya sifa**

Viwakilishi hivi ni maneno ya sifa kama vile -refu, -nene, na nono ambayo huchukua nafsi ya nomino katika sentensi. Ni vyema kukumbuka kwamba, japo kimsingi maneno haya ni vivumishi, yanapotumiwa kama viwakilishi, nomino ambazo zilistahili kuvumishwa na vivumishi hivi havitajwi. Mifano:

(i) ***Wema*** husifiwa kwao.

(ii) ***Watukutu*** hawana maisha matulivu.

**2.7.4.4 Viwakilishi vionyeshi/ viashiria**

Baadhi ya viwakilishi hutumiwa kuashiria watu na vitu mahususi. Hivi huitwa viwakilishi vionyeshi. Husimama mahali pa nomino kwa kuiashiria. Viwakilishi vionyeshi husaidia kuonyesha nafasi (umbali/ ukaribu) wa watu/vitu kutoka kwa msemaji. Viwakilishi vionyeshi huweza kusimamia:

Nomino iliyo karibu na msemaji. Kwa mfano: ***Hiki*** ni cha Macharia.

(i) Nomino iliyo mbali kidogo na msemaji. Kwa mfano: Nataka ***hicho*** kikubwa.

(ii) Nomino iliyo mbali sana na msemaji. Kwa mfano: ***Yale*** yameiva vizuri.

#### 2.7.4.5. Viwakilishi vimilikishi

Haya ni maneno ambayo husimama mahali pa nomino ambayo imemilikiwa na mtu. Huundwa kwa mizizi ifuatayo:

(i) Nafsi ya kwanza: **-angu, -etu**

(ii) Nafsi ya pili: **-ako, -enu**

(iii)Nafsi ya tatu: **-ake, -ao**

Tazama mifano katika sentensi:

(i) Nitakuletea ***chako***, ***chake*** hakikufai.

(ii) ***Mwao*** mmeoshwa vizuri.

#### 2.7.4.6 Viwakilishi vya pekee

Hivi huundwa kwa mizizi ifuatayo:

a) **-ote** – huwakilisha nomino kwa kuonyesha kuhusika kwake kijumla/bila kubakiza. Kwa mfano: Kiti ***chote*** kilikaliwa.

b) **-o-ote** – huwakilisha nomino isiyo mahsusi, kuonyesha 'bila kubagua'. Kwa mfano: Kanda alisema atatumia ***chochote.***

c) **-ingine** – huwakilisha nomino:

(i) Ambayo ni kibadala cha nyingine, kwa mfano: Nipe ***kingine,*** hiki hakifai.

(ii) Ya ziada/zaidi – kwa mfano: Mpishi alipika ***kingine****, kilichokuwapo hakikutosha.*

(iii) *Kuleta maana ya* ***'baadhi ya'*** *– kwa mfano:* ***Mengine*** hayapaswi kuambiwa vijana.

(i) **-enye** – huandamana na nomino kuwakilisha mtu/kitu kinachoimiliki nomino husika. Kwa **mfano:** ***Mwenye*** mali hataki kuiuza.

**d)** **-enyewe** – kuonyesha nomino ambayo inasisitizwa/binafsi/hiyo hiyo. Kwa mfano: Alikuja ***mwenyewe.***

#### 2.7.4.7 Viwakilishi visisitizi

Haya ni maneno ya kutilia mkazo ambayo husimama mahali pa nomino. Kimsingi hivi ni viashiria vya kusisitiza ambavyo hutumiwa badala ya nomino ambayo habari zake

zinatiliwa mkazo. Huweza kuundwa pia kwa mzizi **–enyewe.** Mifano: ***Wale wale*** ndio waliochaguliwa.

#### 2.7.4.8 Viwakilishi viulizi

Viwakilishi hivi ni maneno yanayowakilisha nomino kwa kuulizia habari zake. Kwa mfano: Unataka ***kipi?***

#### 2.7.4.9 Viwakilishi virejeshi

Aghalabu kiwakilishi hiki huwa ni fungu la maneno ambalo husimama mahali pa nomino (ambayo haikutajwa) kwa kuirejelea. Kiwakilishi kirejeshi huundwa kwa kuambika faridi rejeshi **'o'** kabla ya mizizi wa kitenzi. Kirejeshi hicho ndicho kinachorejelea nomino ambayo haijatajwa/ambayo inatangulia katika kauli ya awali. Pia huweza kuundwa kwa kirejeshi **'amba'** kinachoandamana na kitenzi kuwakilisha nomino. Kwa hakika viwakilishi virejeshi ni vishazi virejeshi ambavyo vinasimama mahali pa nomino katika sentensi. Kwa mfano:

(i) ***Kiendacho*** kwa mganga hakirudi. (hapa '***kiendacho'***, ingawa ni kitenzi, kinafanya kazi ya kiwakilishi kwani kinasimamia nomino ambayo inarejelewa na kiambishi kirejeshi **'cho'**).

(ii) ***Ambaye*** huvuma baharini ni papa kumbe wengine wapo? ( hapa , '**ambaye**' huvuma baharini inarejelea kitu ambacho hakikutajwa.) Hivyo, ni kiwakilishi cha nomino katika ngeli ya A-WA, umoja.

#### 2.7.4.10 Viwakilishi vya 'a' – unganifu

Viwakilishi hivi huundwa kwa kuhusishi **'a'** – unganifu kikiandamana na nomino ambayo haikutajwa. Kwa kweli, ni kirai-husishi ambacho husimama mahali pa nomino:

a) Iliyomiliki: kwa mfano: **La** baba limeuzwa.

b) Ya aina fulani: kwa mfano: **Za** fedha zina thamani.

c) Inayochukua nafasi fulani katika orodha: kwa mfano:

   (i) ***Wa tatu*** hajawasili.

   (ii) ***Wa mwisho*** hakupata wali.

#### 2.7.4.11 Viwakilishi vya idadi

Haya ni maneno ambayo husimamia nomino kwa kutaja idadi yake. Idadi ya nomino hiyo huweza kuwa kamili (halisi), au ya jumla. Kwa mfano:

(i) **Mengi** yalikuwa yameoza. (jumla)

(ii) **Asilimia themanini** imetafutiwa makao. (idadi kamili)

#### 2.7.4.12 Viwakilishi vya ngeli

Hivi ni viambishi ambavyo huambikwa kwenye mizizi ya vitenzi kuwakilisha nomino katika ngeli mahususi. Viwakilishi hivi hubadilika kulingana na ngeli ya nomino. Hivi ndivyo vitambulishi vya ngeli za nomino za Kiswahili:

U-ZI: Ukuta **u**najengwa- Kuta **zi**najengwa.

YA –YA: Maji **ya**mechemka- Maji **ya**mechemka.

### 2.7.5 VIELEZI

Vielezi ni maneno ambayo kwa kawaida hueleza zaidi kuhusu tendo, tukio au hali. Vielezi huonyesha:

(i) Wakati kitendo/tukio lilipofanyika, kwa mfano: Watalii waliwasili ***jioni.***

(ii) Mahali pa kutendeka kwa tendo, kwa mfano: Maina anaishi ***Mombasa.***

(iii)Jinsi tukio/tendo linavyofanyika, kwa mfano: Jamlick amefanya hiyo kazi ***vizuri.***

Vielezi pia huelezea zaidi kuhusu vivumishi.Kwa mfano: Jengo hili limejengwa kwa mawe ***makubwa mno.***

Aidha vielezi hutoa habari zaidi kuhusu vielezi vingine. Kwa mfano:

Wanahabari walifafanua suala hilo **vizuri mno.**

Kielezi hujibu maswali yafuatayo kuhusu tendo/tukio/kivumishi/kielezi kinachovumisha.

(i) Lini? Kwa mfano: Kenya ilipata uhuru kamili ***miaka kumi iliyopita.***

(ii) Wapi? Kwa mfano: Meri inaelea ***majini.***

(iii) Vipi? Kwa mfano: Mwalimu alituelezea ***kinaganaga*** kuhusu madhara ya ulevi.

(iv) Kwa kutumia nini? Kwa mfano: Niliukata mti ***kwa shoka.***

(v) Kilitendwa na nani? Kwa mfano: Wali huu umepikwa***na mpishi.***

(vi) Kwa nia gani? Kwa mfano: Wanariadha walifanya mazoezi ***ili washinde mchezoni.***

(vii) Kwa kiasi gani? Mara ngapi? Kwa mfano: Mtetemeko wa ardhi haujatokea ***mara nyingi.***

(viii) Kwa kina kipi/ kwa hali gani? Kwa mfano: Mhadhiri huyu ametufundisha vizuri ***sana.***

Vilevile, vielezi huonyesha mawazo yetu kuhusu uwezekano wa tendo/tukio fulani. Kwa mfano:

(i) ***Bila shaka*** Ngahu atashinda katika uchaguzi huu.

(ii) ***Kwa hakika*** bibi huyo anasingiziwa tu.

Vielezi pia huonyesha uamuzi wetu/tathmini yetu kuhusu tendo la mtu. Kwa mfano: Macharia alilieleza jambo hilo ***kinaganaga.***

Vielezi huweza kuchukua miundo mbalimbali, kama:

(i) Huwa neno moja tu, kwa mfano: Sikutarajia ***kamwe*** anisaidie.

(ii) Vikundi (virai elezi) vya maneno ambayo neno lake kuu ni kielezi. Kwa mfano: Kiongozi mwadilifu hufanya kazi yake ***vizuri mno***.

(iii)Pia huundwa kutokana na kishazi, kwa mfano: ***Baada ya kutuzwa*** tuliongozwa hadi uwanja wa ndege.

**Nafasi (mahali) ya kielezi katika sentensi**

- Kielezi huweza kutokea mwanzoni mwa sentensi, kwa mfano: ***Mwaka jana*** bei ya mafuta ilishuka.

Hapa, ingawa **'mwaka jana'** ni kikundi nomino, kinatumiwa kama kielezi kinachoonyesha wakati wa kushuka kwa bei.

- Pia kielezi huweza kutumika mara tu baada ya kitenzi kikuu/halisi, kwa mfano: Rais aliondoka ***mara moja***.
- Vilevile, kielezi huenda kikatumika baada ya kitendwa/kitendewa (yambwa), kwa mfano: Mwalimu anawapenda wanafunzi wake ***kwa dhati.***

Pahali pa kielezi katika sentensi hutegemea kwa kiasi fulani:

Aina yake: Je, ni kirai husishi kinachotumiwa kama kielezi? Hali ikiwa hivyo, kielezi kinaweza kuja baada ya kitenzi kikuu/yambwa/mwishoni mwa sentensi. Kwa mfano: Mfadhili alinilipia karo baada ya kuona maendeleo yangu ***shuleni.***

Maana ya kielezi – je, kinaashiria wakati, mahali, ama namna? Kwa mfano: Yego alisafiri kwao ***usiku.***

Kielezi kinapotumiwa kuelezea zaidi kuhusu kivumishi, kielezi hicho kwa kawaida huja baada ya kivumishi/kielezi husika, kwa mfano: Kazi za kifasihi huwa na mfanano ***mkubwa mno***.

1. Kielezi ambacho huelezea kielezi kingine huja baada ya kielezi kinachofafanuliwa. Kwa mfano:

a) Mombasa ni jiji ***la pwani.***

Mnazi hupandwa ***Mombasa.***

b) Marekani ni miongoni mwa mataifa ***yanayotufadhili.***

Adrew ameenda Marekani ***kusoma.***

c) ***Asubuhi hiyo*** ilijaa umande.

Umande ulitanda nyasini ***asubuhi***.

d) Ni muhimu kukumbuka kuwa:

(i) Vivumishi huvumisha nomino. Kwa mfano: Guu ***lake*** linauma.

a) Vielezi huvumisha vitenzi, vivumishi, ama vielezi. Kwa mfano: Mvua imenyesha ***sana*** humu.

(ii) Tunatumia kielezi, wala si kivumishi, kusema jinsi jambo lilivyofanyika. Kwa mfano ni sahihi kusema:

a) Riwaya hiyo imeandikwa ***vizuri,***wala si, Riwaya hiyo imeandikwa '**nzuri**' kwani '**nzuri**' ni kivumishi bali si kiwakilishi.

b) Watoto hao hutembea ***kwa haraka.***

Baadhi ya vielezi hutokana na vivumishi, kwa mfano: Msomi amefanya utafiti **mzuri.** Msomi ametafiti ***vizuri.*** Kielezi '**vizuri**' kimetokana na kivumishi '**mzuri**.'

Baadhi ya vielezi huundwa kutokana na vitenzi. Vitenzi hivyo huongezewa viambishi:

- Kiambishi **'po'**- cha hali kuunda kielezi cha wakati. Kwa mfano: Watoto waliamka nili***po***ingia.

- **Po, ko, mo** vya mahali kuunda vielezi vya mahali. Kwa mfano:
  Kamau atanipeleka ana*mo*ishi.
- **Ki** ya hali. Kwa mfano: Utapita u*ki*soma.
  Kunazo aina zifuatazo za vielezi:

### 2.7.5.1 Vielezi vya namna

Hivi ni vielezi ambavyo huonyesha namna kitendo kilivyofanyika. Huonyesha jinsi tukio lilivyotokea. Hujibu swali: **vipi? Kwa namna gani?**

*Vielezi vya namna* hufafanua kitenzi kwa kuonyesha:

- Namna/njia ya kukifanya kitendo, kwa mfano: Msichana mrembo alitembea ***kitausi*** mbele ya wanaume.
- Mbinu iliyotumika kufakinisha kitendo fulani, kwa mfano: Boniface hufanya kazi yake ***kwa utaalamu.***
- Kifaa kilichotumiwa kutendea kitendo fulani, kwa mfano: Julius aliandika kumbukumbu ***kwa chaki.***

Tazama mifano zaidi:

(i) Gathunga alirukaruka ***kama mama yake***. (mbinu ya kufanya)

(ii) Nisamehe kwa kukucheleweshа ***hivyo***. (namna ya kufanya)

Mara nyingine vielezi vya namna hufafanua kitenzi/kivumishi kwa kulinganisha na jambo (nomino/kivumishi) lingine, kwa mfano: Sungura alimruka fisi ***kama zimwi.***
Vielezi vya namna pia huonyesha kinachosababisha kitendo. Hujibu swali-'kipi kinachosababisha tendo/tukio fulani?' Hapa tunaangazia mtendaji wa jambo/tendo. Kwa mfano: Jumba lake lilichomwa na ***majambazi.***
Vielezi vya namna hufafanua kitenzi kwa kuonyesha chanzo/sababu ya tendo hilo, kwa mfano: Mpango wa chanjo kwa watoto wadogo utatayarishwa ***na madaktari.***

Katika (a), **'na madaktari'** ni kielezi kwa sababu inafafanua kitenzi **utatayarishwa** kwa kuonyesha chanzo cha mpango huo. Vielezi vya namna hufafanua kitenzi kwa kuonyesha nia/kusudi la kutendwa kwa kitendo hicho, Kwa mfano: Waumini walifika mapema***ili kusali sala za asubuhi.***

Vielezi vya namna huonyesha hali/kiwango cha kufanyika kwa kitendo, kwa mfano: Tunu anakupenda ***sana.***

Zipo aina zifuatazo za vielezi vya namna.

#### 2.7.5.1.1 Vielezi vya namna halisi

Hivi ni vielezi vya namna ambavyo vyenyewe ni vielezi. Havitokani na maneno mengine. Kwa kawaida huwa vielezi tu. Ni maneno mazima yanayojisimamia-hayaambikwi viambishi vyovyote. Tazama mifano:

(i) Ukuta huo umepakwa rangi ***kiholela.***

(ii) Nguo yake imechanika ***kabisa.***

#### 2.7.5.1.2 Vielezi vya namna hali

Hivi hujibu swali: **'kwa kiwango kipi?'** Huitwa pia vielezi vya namna kiwango. Huonyesha hali ambayo kitendo kinatendwa. Baadhi huundwa kutokana na nomino dhahania. Tazama mifano:

(i) Kazi ifanywayo ***haraka*** huwa na dosari.

(ii) Chai hiyo ni moto ***mno.***

Vielezi halisi ni mifano ya vielezi vya hali.

#### 2.7.5.1.3 Vielezi vya namna mfanano

Hivi hufananua kitendo kwa kukifananisha na jambo fulani. Baadhi huundwa kwa kuambika kiambishi ***ki*** au ***vi*** cha kufananisha katika mizizi ya nomino/kivumishi. Kwa kufanya hivi kitendo kinachofafanuliwa kinafananishwa na nomino kivumishi husika. Tazama mifano:

(i) Askari walipigana ***kijeshi***.

(ii) Alijibu maswali yote ***kijinga.***

Baadhi ya vielezi vya namna mfanano huundwa kwa kutumia maneno ya kufananisha kama vile **kama, mithili, ja** na **jinsi**. Chunguza mifano:

(i) Mhubiri huyo alihubiri ***kama kasisi.***

(ii) Mwanariadha huyo alikimbia ***ja duma.***

#### 2.7.5.1.4 Vielezi vya namna viigizi

Hivi pia vimaweza kuchukuliwa kama vielezi vya namna ambavyo hufafanua kitenzi kwa kufananisha. Viigizi huonyesha jinsi kitendo kilivyofanywa kwa kuiga sauti/ mlio unaotokea kwakawaida kitendo chenyewe kinapofanyika. Kwa mfano: Mlango unapogotwa sauti inayotokea ni 'ngo'; hivyo tunasema: Mlango uligongwa **ngo ngo ngo**. Sauti **ngo** ni mwigo wa tokeo la kugongwa kwa mlango. Chunguza mifano zaidi:

(i) Tunda lilianguka chini ***pu.***

(ii) Machozi yalinitiririka ***tiriri.***

Kutokana na mifano hii, ni wazi kwamba tanakali zote za sauti ni aina ya vielezi vya namna viigizi.

#### 2.7.5.1.5 Vielezi vya namna ala/kitumizi

Hivi hufafanua namna ya kutendeka kwa tendo kwa kutaja kifaa ambacho kilifanikisha kutendeka kwa tendo hilo. Kwa mfano: Zamani watu walibadilishana bidhaa ***kwa bidhaa***.

#### 2.7.5.1.6 Vielezi vya namna vinavyoonyesha mtenda /kitenda

Hivi hufafanua vitendo kwa kuonyesha mtendaji. Kwa mfano: Kikosi hicho kiliongozwa na ***mwanajeshi shujaa.***

#### 2.7.5.1. Vielezi vya namna vinavyoonyesha mbinu/mikakati iliyotumiwa kufanikisha kitendo.

Kwa mfano: Uvunaji huo ulifanywa ***kwa ushirikiano*** ukakamilika mapema.

#### 2.7.5.1.8 Vielezi vya namna vikariri

Hivi hufafanua kitenzi kwa kurudiarudia neno linalotumika kama kielezi. Kwa mfano: Mwizi alitembea ***haraka haraka*** ili asipatikane.

#### 2.7.5.2 Vielezi vya wakati

Hivi hufafanua kitenzi kwa kuonyesha wakati kilipotendeka. Huweza kuwa:

(i) Nomino moja inayotumika kama kielezi cha wakati, Kwa mfano: Mgeni wetu atafika ***kesho.***

(ii) Fungu la maneno (kirai husishi) linalofanya kazi kama kielezi cha wakati, Kwa mfano: Rais aliuhutubia umati ***baada ya dakika thelathini.***

(iii) Kishazi kinachofanya kazi kama kielezi, Kwa mfano: Wazili wa elimu ***alipowasili*** alitangaza matokeo ya mtihani.

### 2.7.5.3 Vielezi vya mahali.

Vielezi hivi hufafanua kitenzi kwa kutaja mahali kinapofanyika, Kwa mfano: Kiweke chakula ***mezani.***

Vielezi vya mahali huweza kuwa:

(i) Neno moja linaloonyesha upande.Kwamfano: Pikipiki imeelekea ***kushoto.***

(ii) Kirai husishi kinachofanya kazi kama kielezi. Kwa mfano: Mwalimu anasimama ***mbele ya wanafunzi.***

(iii) Nomino ya pekee inayotumiwa kama kielezi. Kwa mfano: Uchaguzi huo ulifanyika ***Nakuru***.

(iv) Kishazi ambacho kinafafanua mahali kitendo kimefanyika, Kwa mfano: James atakuonyesha ***walikoweka*** nguo zao.

### 2.7.5.4 Vielezi vya idadi/kiasi

Vielezi hivi hujibu swali **'mara ngapi?'** Hufafanua kitendo kwa kuonyesha mara ya kufanyika kwake. Idadi hii huweza kuwa dhahiri/kamili/halisi au ya jumla. Kwa mfano:

a) Yeye huja hapa ***mara kwa mara.*** (idadi isiyodhihirika)

b) Yeye huja hapa ***mara mbili kila wiki***. (idadi dhahiri/kamili)

Zipo aina zifuatazo za vielezi vya idadi:

#### 2.7.5.4.1 Vielezi vya idadi ya jumla

Hivi hueleza kwa njia ya jumla (isiyo halisi/kamili) idadi/mara ya kutendeka kwa kitendo. Kwa mfano: ***Mara nyingine*** Mugo alikuwa akitutembelea.

#### 2.7.5.4.2 Vielezi vya idadi kamili

Hivi huonyesha idadi ya kutendeka kwa kitendo kwa kutaja idadi halisi ya kutendeka. Tarakimu hutumiwa kuonyesha mara ya kufanyika kwa kitendo, kama ilivyo katika mfano ufuatao: Mwanafunzi alibisha ***mara mbili***.

### 2.7.6 VITENZI

Kitenzi ni neno ambalo huonyesha tendo lililofanywa au hali ya kuwa. Kitenzi huarifu:

a) Kinachotendwa: Kwa mfano: Msasi ***amebeba*** uta na mishale.

b) Nomino ni nini? / ni ya aina/ tabia gani? Kwa mfano: Ukuta huo ***ni*** mrefu.

c) Hali ya *kuwa* au *kutokuwa na,* kwa mfano: Makasisi wote ***wana*** ungwana.

d) Hali- vitenzi vya aina hii huelezea hali fulani badala ya tendo. Kwa mfano: Julia aliamini kwamba ***angepita*** mtihani.

Kila sentensi lazima iwe na kitenzi. Vitenzi vingi huwa vitenzi vya kutenda – yaani, huonyesha kutendeka kwa jambo. Kwa mfano: Mpira ***umepotea.***

Baadhi ya vitenzi vya kutenda hurejelea kitendo halisi kinachoonekana na watu kikitendwa/kikitendeka. Kwa mfano, tunaposema '*Mjomba* ***anasoma*** *gazeti'* kitenzi ***'anasoma'*** kinaweza kuonekana kikitekelezwa. Vitenzi vingine vya kutenda hurejelea kitendo cha akilini, (dhahania) ambacho hakiwezi kuonekana. Kwa mfano tunaposema"Watalii ***huvutiwa*** na wanyama wa porini." Kitendo '**v*utiwa***' hakiwezi kuonekana kikitekelezwa; kimo akilini mwa anayekitenda (anayekikisia).

Baadhi ya vitenzi havionyeshi kutendeka kwa jambo, ila huonyesha tu hali ya kitu au mtu, vile alivyo mtu ama kilivyo kitu. Kwa mfano:

(a) Kaiku ***ni*** mrefu.

(b) Gari lako ***limekuwa*** safi sana.

Kwa jumla, kitenzi huonyesha:

(i) Anachofanya mtu. Kwa mfano: Mlinzi ***amefunga*** mlango.

(ii) Alichonacho mtu. Kwa mfano: Sonara ***ana*** pete nzuri.

(iii) Alicho mtu. Kwa mfano: Otieno ***ni*** msanii hodari.

(iv) Alichohisi mtu. Kwa mfano: Huyu ***anapenda*** kazi yake.

(v) Kuwapo kwa hali: Jambo hili ***limekuwa*** gumu.

#### 2.7.6.1Aina za vitenzi

Katika mjadala wa hapo juu, imejitokeza kwamba kuna makundi mawili makuu ya vitenzi:

1) Vya kutenda. Kwa mfano: **anaenda, alilima, aliniangalia, atasimamia** na **watanifunza.**
2) Vya kuwa. Kwa mfano: **alikuwa akicheza, atakuwa akiwafunza, amekuwa akisoma** na **mlikuwa mkiniita.**

Vitenzi huweza pia kuainishwa kulingana na uamilifu (kazi) wake katika sentensi. Kwa kufuata mkabala huu wa mawazo, tunaibusha maswali yafuatayo:

a) Je, kitenzi ndicho kinatoa habari/ujumbe wa kimsingi katika sentensi? Kwa mfano: Hawa **ni** wake.
b) Je, kitenzi kinasaidia kitenzi kikuu? Kwa mfano: Tanui **alikuwa** akizungumza.
c) Je, kitenzi kinashirikisha pamoja vipashio fulani katika sentensi hiyo? K.m: Hawa **ni** wake.

Vitenzi huweza kuainishwa kulingana na jinsi vinavyotokea katika mfuatano/mfululizo fulani. Hapa tunapata vitenzi sambamba kama ilivyo katika sentensi ifuatayo: Paa **alikimbia akitazama** nyuma. Tuchunguze aina zifuatazo za vitenzi:

##### 2.7.6.1.1 Vitenzi halisi

Hivi ni vitenzi ambavyo huonyesha kutendeka kwa kitendo. Huitwa vitenzi halisi kwa sababu vyenyewe ni vitendo tu. Wakati mwingine huitwa vitenzi vya kutenda. Kwa mfano: Watafiti ***walizuru*** makavazi mbalimbali nchini. Vitenzi halisi huweza kuwa:

##### 2.7.6.1.2 Vitenzi elekezi

Hivi ni vile vitenzi vya kutenda ambavyo vinaweza kuchukua kitendwa/kitendewa (yambwa). Muundo wake unadokeza kuwa kuna kitendwa/kitu kinachoelekezwa tendo hilo. Kwa mfano, unaposikia "Gachui **alivuna**...." Unajiuliza: "alivuna nini?" Katika sentensi **"**Gachui **alivuna** mahindi mengi.**"** Kitenzi '**alivuna**' ni elekezi kwa sababu kinachukua kitendwa/kitendewa **'mahindi mengi'**. Mfano mwingine: Juma ***alituandalia*** chakula.

#### 2.7.6.1.3Vitenzi visoelekezi

Hivi ni vitenzi vya kutenda ambavyo havichukui yambwa (kitendwa/kitendwa). Muundo wake haudokezi uwezekano wa kuwapo kwa yambwa. Tendo halielekezwi kwa yeyote/chochote. Kwa mfano: Mwangi ***alitabasamu.***

#### 2.7.6.1.4 Vitenzi vikuu

Kitenzi kikuu huelezea tendo au hali ya kuwa. Ndicho hubeba ujumbe wa kimsingi wa sentensi; lazima kiwepo kwa sentensi. Huweza kutokea peke yake katika sentensi bila hata kipashio kingine. Kwa kawaida kitenzi kikuu ni kitenzi halisi tu/kitenzi cha kuwa tu. Kwa kawaida kitenzi kitaitwa kikuu ikiwa kinaandamana na kingine kisaidizi katika sentensi. Tazama mfano: Mawingu ya mvua **yamekuwa yakikusanyika** angani. **('yamekuwa'** ni kitenzi kisaidizi ilhali **'yakikusanyika'** ni kitenzi kikuu).

Kitenzi kisaidizi kinapotumika pamoja na kitenzi kikuu, aghalabu kitenzi kisaidizi huja kwanza.

#### 2.7.6.1.5 Vitenzi visaidizi

Hivi ni vitenzi ambavyo husaidia vitenzi vikuu kupitisha ujumbe fulani. Vitenzi vikuu huandamana na vitenzi visaidizi kutoa dhana zifuatazo:

(i) Njeo/wakati. Kwa mfano: Mhubiri ***atakuwa akihubiri.***

(ii) Uwezekano/kutowezekana kwa jambo. Kwa mfano: ***Huenda akaja*** kwetu kesho.

(iii) Ukanushi, kwa mfano: ***Siwezi kulifanya*** swali hili.

Baadhi ya vitenzi visaidizi huweza kutokea pekee katika sentensi, hasa pale ambapo vinatumika kama jibu la swali linalotangulia. Kwa mfano: Je, ***umewahi*** kumwona mbogo?

### 2.7.6.2 Vitenzi vya hali/dhamira

Vitenzi vya hali ni aina ya vitenzi visaidizi ambavyo huonyesha uamuzi/uwezekano/dhana ya uwajibikaji au uhuru wa kutenda jambo. Huonyesha:

(i) Uamuzi kutokana na jambo. Kwa mfano: Lazima ***awe*** wazimu kuweza kuamini hayo.

(ii) Haja ya kutendeka kwa tendo. Kwa mfano: ***Unapasa*** kuandika orodha tunayohitaji.

(iii) Ikiwa jambo linawezekana au la.Kwa mfano: Hakika tunayohitaji ***tutayapata?***

(iv) Uhakika wa kutenda jambo.Kwa mfano: '***Nitaweza*** kukusaidia.'inaonyesha ya kwamba mtu ana uhakika wa kuweza kusaidia.

Ikiwa mtu ana hiari ya kutenda jambo au inamjuzu kulitenda. Kwa mfano tunaposema: 'Ukitaka kufanikiwa **sharti** ujitahidi.' Kitenzi '**sharti'** ni cha hali. Kinaonyesha dhamira/mwelekeo kuwa kujitahidi ni lazima –mtu hana hiari. Tazama mifano zaidi:

(i) Kipchoge ***anaweza*** kukimbia mbio za masafa marefu. (kuna uwezakano )

(ii) ***Pengine nitakuja*** kukutembelea. (hana uhakika)

**2.7.6.3 Vitenzi vishirikishi**

Hivi ni vitenzi ambavyo vinashirikisha kiima cha sentensi na kijalizo. Kiima ni nomino /kiwakilishi ambayo habari zake zinatolewa katika sentensi. Kwa mfano:

Jua ni kali. (Hapa, **'jua**' ndicho kiima.'**kali'** ndicho kijalizo). Katika sentensi:

*Mwangi ni mwalimu.*

a) '**Mwangi'** ni kiima.

b) '**Ni'** ni kitenzi kishirikishi.

c) '**Mwalimu'**ni kijalizo –linafafanua zaidi kuhusu **Mwangi.**

Mifano zaidi ni pamoja na:

1. **Hicho** *kilikuwa* ***kipindi kigumu***.

Kiima t kijalizo

2. **Wale** *watakuwa* ***washirika wetu.***

Kiima t kijalizo

**Aina za vitenzi vishirikishi**

Zipo aina mbili za vitenzi vishirikishi;

**i) Vitenzi vishirikishi vipungufu**

Hivi ni vitenzi vishirikishi ambavyo havichukui viambishi vya njeo (wakati) na hali, lakini huweza kuchukua viambishi vya nafsi/vya ngeli. Kwa mfano: Kwake ***kungali*** mbali na mji.

**ii) Vitenzi vishirikishi vikamilifu**

Hivi huchukua viambishi vya njeo/wakati/hali/nafsi/ngeli. Kwa mfano: Jane ***alikuwa*** mwanawe Juma.

### 2.7.6.4 Vitenzi sambamba

Hivi vi vitenzi ambavyo hutokea mfululizo katika sentensi. Huweza kuwa vitenzi viwili halisi, au kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu vikifuatana. Tazama mifano:

(i) Mbiu ya mgambo ***ingali inalia***.

(ii) Ndama ***anakimbia akitafuna*** nyasi.

### 2.7.7 VIHUSISHI

Kihusishi ni neno ambalo huonyesha uhusiano uliopo kati ya nomino/kiwakilishi na neno/maneno mengine yaliyopo katika sentensi hiyo. Huweza kuonyesha uhusiano kati ya mtu na kitu, mtu na mtu, kitendo na mahali, kitendo na wakati wa kutendwa, kitu na kitu, n.k. Kihusishi:

**a)** Huonyesha uhusiano wa kiwakati, kwa mfano: Ngoma hiyo ilipigwa ***hadi asubuhi.***

**b)** Huonyesha uhusiano wa mahali, kwa mfano: Jiwe limetupwa ***ndani ya*** kidimbwi.

**c)** Huonyesha uhusiano kwa kulinganisha, kwa mfano: Dhahabu ni ghali ***kuliko shaba.***

**d)** Huonyesha uhusiano wa umilikaji, kwa mfano: Shamba ***la Wachira*** ni kubwa mno.

**e)** Huhusisha kitu na aina/sampuli yake, Kwa mfano: Ndege ametua ***juu ya mti***.

Vihusishi huweza kuwa **sahili**. Hivi ni vihusishi ambavyo kwa kawaida ni neno moja, kama vile; **hadi, mpaka, tangu** na **kwa**. Kwa mfano: Hajarudia tendo hilo ***tangu*** aonywe na wazazi.

Vilevile, vihusishi huweza kuwa **changamano**. Hivi huwa maneno mawili au matatu ambayo hutumiwa pamoja kuonyesha uhusiano kati ya vipashio viwili katika sentensi. Kwamfano: Julie alikuwa ***miongoni mwa*** washindi wa kombe la dhahabu.

Vihusishi huweza pia kutumiwa kuunganishia (kama viunganishi) sentensi/vipashio mbalimbali. Kwa mfano: Tindi aliwasili ***halafu*** akaondoka. (hapa, **'halafu'**inaunganisha; Tindi aliwasili na Tindi aliondoka).

Vihusishi huweza pia kutumiwa kama vielezi vya wakati, kwa mfano: Nitakujuza ***baadaye.***

Wakati mwingine vihusishi huandamana na nomino/kiwakilishi kuunda kirai kuhusishi ambacho kinafanya kazi kama kielezi au kivumishi. Ufuataο ni mifano: Watalii hupenda kutembea ***kando ya ufuo***.

Vihushi vilevile huonyesha mtenda/kitenda/kifaa. Kwa mfano:

a) Kazi hiyo imefanywa na ***mfanyakazi hodari.*** (mtenda)

b) Zulia alilima shamba ***kwa jembe***. (kifaa)

c) Leo anaumwa ***na tumbo***. (kitenda)

#### 2.7.7.1 AINA YA VIHUSISHI

##### 2.7.7.1.1 Vihushi vya wakati

Hivi huhusisha kitendo (jambo) na wakati kinapotendeka. Huonyesha uhusiano wa kiwakati. Kwa mfano: Ubaguzi wa rangi ulishamiri ***hadi*** karne ya ishirini.

Vihusishi vingine vya wakati ni kama vile **kisha, halafu, kufikia na mpaka.**

##### 2.7.7.1.2 Vihusishi vya mahali

Hivi huonyesha mahali/tendo lipo/linafanyika kwa kuhusishwa na mahali fulani. Huonyesha uhusiano wa kimahali. Mifano ya vihusishi hivi ni pamoja na **hadi, mpaka, kando ya, katika, kati ya, miongoni mwa, mbele ya, juu ya na chini ya.**Tazama mfano katika sentensi: Wazazi wake waliishi **karibu na** shule.

##### 2.7.7.1.3 Vihusishi vilinganishi/vya kulinganisha

Hivi huhusisha vitu kwa kuvilinganisha. Kwa mfano: Njia hii ni ndefu **kuliko** ile.

#### 2.7.7.1.4 Kihusishi cha 'a' unganifu

Vihusishi hivi huundwa kwa mzizi wa uhusiano. Huonyesha uhusiano kwa kuibua dhana zifuatazo:

(i) Umilikaji/hali ya kuwa na. Kwa mfano: Ufunguo ***wa*** mlango huu haujapatikana.

(ii) Aina/hali ya kitu. Kwa mfano: Mkono ***wa kulia*** unaniuma.

(iii) Nafasi katika orodha. Mathalan: Kanyongoro alikuwa ***wa nne*** kuadhibiwa.

#### 2.7.7.1.5 Kihusishi 'na' cha mtenda

Hiki huonyesha uhusiano kati ya kitendo na mtenda. Kwa mfano: Darasa zima litatuzwa ***na*** mwalimu mkuu.

#### 2.7.7.1.6 Kihusishi 'kwa' cha kitenda/kifaa/jinsi

Hiki huonyesha uhusiano kati ya tendo na kifaa kinachofanikisha tendo hilo/jinsi kitendo kilivyofanyika. Kwa mfano: Mzigo huo ulifungwa ***kwa*** *kamba.*

#### 2.7.7.1.7 Vihusishi vya sababu

Hivi hutaja uhusiano kwa kuonyesha kisababishi cha jambo/tendo. Huhusisha tendo na sababu/chanzo chake. Kwa mfano: Nitakuarifu mapema ***kwa*** *vile sitaki ukose sherehe hiyo.*

### 2.7.7.2 Matumizi zaidi ya kihusishi 'kwa'

Pamoja na kuonyesha kifaa kilichotumiwa 'kwa' hutumiwa kuleta dhana zifuatazo:

a) *Kitendo kilichofanyika.* Kwa mfano: Marafiki hao huishi ***kwa*** amani.

b) *Sababu ya kutendwa kwa jambo.* Kwa mfano: Mtu huheshimiwa ***kwa*** matendo yake.

c) *Sehemu fulani ya kitu kizima.* Mathalani: Kima alipata alama kumi ***kwa*** ishirini.

d) Kuonyesha mahali *(kitendo) kilikomilikiwa.* Kwa mfano: Kule ***kwa*** Mbondo kuna miti mingi.

### 2.7.8 VIUNGANISHI

Kiunganishi ni neno/fungu la maneno/kiambishi ambacho huunganisha na kuonyesha uhusiano kati ya maneno, virai au vishazi. Viunganishi basi huunganisha:

(a) Neno na neno. Kwa mfano: Mpunga ***na*** mhindi hupandwa humu.

(b) Kirai na kirai. Kwa mfano: *Mwalimu huyo* ***na*** *watoto wake* wamewasili.

(c) Kishazi na kishazi. Kwa mfano: Wanawake walibaguliwa zamani ***lakini*** sasa wamepewa nafasi sawa na wanaume.

(d) Sentensi na sentensi. Kwa mfano: Maafisa wote waliohamishwa humu wamejengewa nyumba ***lakini*** badala ya nyumba hizo ni hali duni.

Yapo makundi mawili makuu ya viunganishi:

- Viunganishi ambatani/ambatishi
- Viunganishi vitegemezi

#### 2.7.8.1 Viunganishi ambatani/ambatishi

Hivi huunganisha vipashio vya hadhi sawa /vya aina moja. Kwa mfano:

(a) Nomino na nomino. Mfano: Nimenunua kalamu ***na*** kitabu.

(b) Kirai na kirai. Kwa mfano: Hawa wake ***na*** hawa wetuwametuzwa.

(c) Kishazi huru/kikuu na kishazi huru/kikuu. Kwa mfano: Caroline amewasili ***lakini*** wengine hawajafika.

(d) Kishazi kitegemezi na kishazi kitegemezi. Kwa mfano: *Walioalikwa* ***na*** wasioalikwa walihudhuria.

Viunganishi ambatani vilivyozoeleka ni: ***na, lakini, au, wala, ama, ila na ilhali.***

#### 2.7.8.2 Viunganishi vitegemezi

Hivi huunganisha vishazi vitegemezi na vishazi vikuu/huru. Huweza kuwa maneno au viambishi. Kwa mfano: **Badala ya** kuwasili tuliondoka.

#### 2.7.8.3 Aina za viunganishi

Mbali na makundi mawili makuu ya viunganishi (ambatani na tegemezi), viunganishi huweza kuainishwa zaidi kwa kuzingatia maana/dhamira zinazoibuliwa na kimojawapo. Kwa kufuata mkabala huu tuna aina zifuatazo za viunganishi:

#### 2.7.8.3.1 Viunganishi viongezi/vya kuongeza

Hivi ni viunganishi ambavyo huunganisha vipashio kwa kuleta dhana ya **'ziada ya'** Mifano ya viunganishi hivi ni**:** ***na, tena, pia, aidha, pamoja na,*** na ***zaidi ya.*** Tazama mifano katika sentensi:

(i) Utu ***na*** bidii yake imemfanya kupendwa na wengi.

(ii) Mbatia ni msomi stadi ***tena*** ni mwandishi wa riwaya.

#### 2.7.8.3.2 Viunganishi visababishi/vya sababu

Hivi ni viunganishi ambavyo huunganisha maneno/mafungu ya maneno/sentensi kwa kuonyeshakusababishi kwa dhana/matukio. Hutoa sababu ya kutendeka kwa jambo/kuwapo kwa hali fulani. Huweza kutumiwa mwanzoni au katikati mwa sentensi. Tazama mifano:

**a)** *Kwa **vile*** giza limeanza kuingia nitarejea nyumbani.

**b)** Daktari hakuweza kumsaidia ***kwa sababu*** alikataa kumwambia ukweli.

#### 2.7.8.3.3 Viunganishi vya nia/dhamira/matokeo

Viunganishi huonyesha lengo la tendo fulani. Hueleza kwa nini tendo linafanywa.

Pia huonyesha matokeo ya tendo. Huhusiana kwa kiasi kikubwa na viunganishi vya sababu.

Tazama mfano: Aisha alikuja kwetu ***kwa*** kutaka kuniona.

#### 2.7.8.3.4 Viunganishi vya kinyume

Viunganishi hivi hutumiwa kuleta dhana ya kinyume na matarajio. Huonyesha ukinzani kati ya kile kilichotendeka na kile ambacho kilitarajiwa kutendeka. Tazama mifano: Zainabu alikuwa maskini ***licha ya***kuwa mwimbaji hodari.

#### 2.7.8.3.5 Viunganishi vya wakati

Hivi kwa kawaida huwa vihusishi vya wakati. Huunganisha mafungu ya maneno kwa kuonyesha jinsi yanavyofuatana kiwakati.

Huonyesha tukio moja linafuata lingine. Kwa mfano: Sara aliondoka ***kisha*** Ali akamfuata.

**2.7.8.3.6 Viunganishi vya masharti**

Hivi huleta dhana ya kutegemeana kwa matukio. Huunganisha mafungu ya maneno kwa kuonyesha kwamba yanategemeana. Kwa mfano: Mimea hiyo itanawiri ***iwapo*** itanyunyiziwa maji vyema.

**2.7.8.3.7 Viunganishi vya uteuzi**

Hivi huunganisha maneno/mawazo ili kuleta dhana ya kutofanyika kwa lolote. Pia huleta dhana ya kufanya jambo moja tu wakati fulani wala si yote mawili kwa pamoja. Huonyesha kuchagua / kubagua baina ya mambo mawili. Kwa mfano: Wageni wangependa pilau ***au*** chapati?

**2.7.8.3.8 Viunganishi vitegemezi**

Kwa kawaida ni viambishi ambavyo huunganisha sentensi mbili. Viambishi hivi ni *faridi* ***'o' rejeshi 'ki', 'ngali' na 'nge'***. Viunganishi vya masharti pia ni vitegemezi. Viunganishi vitegemezi vinapotumiwa kuunganisha vishazi/sentensi, sentensi mpya inayobuniwa huwa changamano, yaani yenye kishazi kitegemezi na kishazi huru/vishazi viwili vitegemezi. Mifano mingine ya viunganishi vitegemezi ni ***baada ya, kwa sababu*** na **kwa kuwa**. Ifuatayo ni mifano katika sentensi:

(a) Sherehe **ili*po*malizika** sote tulienda nyumbani.

(b) Wale wote **wali*o*alikwa** walituzwa zawadi.

## HITIMISHO

Tuliamua kujadili kuhusu ngeli za nomino, na aina za maneno katika sura hii na hatimaye upatanisho murua wa aina za maneno na ngeli katika mifano ya sentensi tuliyoitoa ili kuonyesha lugha sanifu ya Kiswahili inavyostahili kuwa. Mifano hiyo inaonyesha mifano ya sentensi sahihi za lugha ya Kiswahili. Mifano hiyo itaweza kumwelekeza kwa kiwango fulani mtu anayetaka kujifunza lugha sanifu ya Kiswahili. Kwa hakika huwezi kujadili makosa iwapo wewe mwenyewe hujui kanuni za lugha sanifu ama huwezi kuelezea lugha sanifu ni gani. Hiyo ndiyo sababu iliyotufanya kujadili kuhusu ngeli, makundi ya majina na uhusiano uliopo kati ya ngeli hizo na makundi hayo.

Makosa yote ya kimaongezi ya kimofosintaksia hutokea pale ambapo nomino katika ngeli yoyote zimekosa kupatanishwa vizuri wakati wa mazungumzo.

# SURA YA TATU

## 3.0 MAKOSA YA KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA

## 3.1 UTANGULIZI.

Katika sura hii tutajadili kuhusu dhana ya kifonolojia na makosa ya kimofolojia. Ni ukweli usiopingika kwamba huwezi kuwa na mofolojia bila kuwa na fonolojia, huwezi pia kuwa na sintaksia bila kuwa na mofolojia na huwezi kujadili kuhusu mofosintaksia bila kujihusisha na mofolojia na sintaksia. Mofolojia hutokana na vipashio vya sauti vilivyo katika taaluma ya fonolojia. Sintaksia nayo huundwa kwa vipashio vya maneno vinavyopatikana katika taaluma ya mofolojia.

Kwa kufuata mkabala huu wa mawazo basi, ni wazi kuwa makosa ya kifonolojia husababisha makosa ya kimofolojia. Aidha, makosa ya kimofolojia husababisha makosa ya kisintaksia. Makosa ya kimofolojia na yale ya kisintaksia husababisha makosa ya kimofosintaksia. Ukweli huu ndio uliotupa mshawasha wa kutaka kujadili kuhusu makosa ya kifonolojia na ya kimofolojia. Hatukuweza kujadili kuhusu makosa ya kisintaksia kwa sababu yalionekana kusabihiana sana na makosa ya kimofosintaksia. Hii ni kwa sababu sintaksia na mofosintaksia zote huhusu sarufi katika virai, vishazi na sentensi. Tulijiepusha na kushughulikia makosa ya kisintaksia ili kuepuka utata kwani tuligundua kuwa makosa ya kisintaksia ndiyo ya kimofosintaksia.

### 3.2 Makosa ya kifonolojia

Kwa mujibu wa Mweri (2010), fonolojia ni kiwango cha uchunguzi wa isimu ambacho huchambua mfumo wa sauti katika lugha fulani mahsusi. Fonolojia hushughulikia sauti za lugha mahsusi, Sauti zinapotamkwa visivyo husababisha ukiushi wa kifonetiki. Ukiushi huu unaweza kuwa unasababishwa na athari za lugha ya kwanza ya mzungumzaji, kutojua au hata kutamka sauti bila kujali.

Kama tulivyokuwa tumetaja hapo awali, kunazo sauti zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili lakini hazipatikani katika lugha ya Kikuyu. Sauti hizo ni /v/, /z/, /l/, /tʃ/ na /p/. Kuhusiana na na haya, maneno ya Kiswahili yaliyo na sauti hizi yaliwatatiza wahusika wetu wa utafiti. Watafitiwa wengi walikuwa wanazitumia sauti zilizokaribiana na zile

zinazopatikana katika lugha ya Kikuyu. Kwa mfano: walitamka /l/ kama /r/, /v/ kama /β/. Wanafunzi hasa wa shule za msingi walishindwa kutofautisha kati ya sauti /f/ na /v/, sauti /s/, /ʃ/, /tʃ/ na /z/. Baadhi ya wanafunzi hao walisema:

(i) ***'Nilirara'*** mapema ili niamke mapema, badala ya; ***Nililala*** mapema ili niamke mapema.

(ii) ***'Nilikura chakura'*** changu kabla ya '***mwarimu'*** kuingia, badala ya; ***Nilikula chakula*** changu kabla ya ***mwalimu*** kuingia.

(iii) ***'Mwarimu'***alisema kuwa hamjafagia vizuri, badala ya; ***Mwalimu*** alisema kuwa hamjafagia vizuri.

(iv) Ning'iniza '***shati'***ukutani, badala ya; Ning'iniza ***chati*** ukutani.

(v) Mimi '***nimeshoka,'*** sana badala ya; Mimi ***nimechoka*** sana.

(vi) Sikuwa nimebeba '***shai,'*** badala ya; Sikuwa nimebeba ***chai.***

(vii) ***'Fijana'*** wa siku hizi wameharibika, badala ya; ***Vijana*** wa siku hizi wameharibika.

(viii) ***'Ludi'*** darasani, badala ya; ***Rudi*** darasani.

(ix) '***Usifae sale'*** ya shule iliyo na ***ushafu,*** badala ya; ***Usivae sare*** ya shule iliyo na ***uchafu.***

(x) Kuku ***'alichakulachakula'*** akitafuta chakula' badala ya kusema; Kuku *alichakurachakura* **akitafuta chakula.**

(xi) 'Nitawaletea ***'shati lililoshorwa'*** sehemu ***'sa'*** mwili' badala ya; Nitawaletea ***chati iliyochorwa*** sehemu ***za*** mwili.

(xii) ***'Usirare'*** kabla ya kumaliza ***'kasi'*** niliyokupa' badala ya; ***Usilale*** kabla ya kumaliza ***kazi*** niliyokupa.

(xiii) ***'Fijana'*** wa ***'dalasa'*** la nane wanaandika ***'fisuri'*** sana badala ya kusema; ***Vijana*** wa ***darasa*** la nane wanaandika ***vizuri*** sana.

*(xiv)* ***'Nashukua fulsa*** hii ***kuwasukulu warimu*** na ***wasasi*** kwa ***kuhuthuria*** mkutano huu,' badala ya; *Nachukua fursa hii kuwashukuru walimu na wazazi kwa kuhudhuria mkutano huu.*

Matamshi haya yaliathiri kwa kiwango kikubwa mawasiliano kwa sababu mzungumzaji aliishia kutunga sentensi ambazo hazikuwa na mantiki.

Katika uchanganuzi wetu, sentensi, virai au vishazi vilivyotamkwa vikiwa vina ukiushi dhidi ya kanuni za Kiswahili sanifu vimeonyeshwa kwa alama za kunukuu.

### 3.3 Makosa ya kimofolojia

#### 3.3.1 Dhana ya mofolojia

Ili kuweza kujadili makosa ya kimofolojia, hatuna budi kujadili kuhusu maana ya mofolojia. Kwa mujibu wa Obuchi na Mukhwana (2010) mofolojia au mofemiki ni taaluma inayohusu maneno. Taaluma hii hudhihirisha muundo wa maneno kwa kurejelea mofu mbalimbali zenye kazi za kisarufi. Wanaendelea kusema kuwa, mofolojia huhakiki viungo vidogo kabisa katika lugha vyenye maana na mpangilio wavyo katika maneno.Mathews akinukuliwa na Mgullu (1999) anasema kuwa mofolojia ni tawi la taaluma ya isimu ambalo huchunguza maumbo ya maneno na hususan maumbo ya mofimu. Mofolojia huchunguza mofimu na alomofu zake na jinsi ambavyo hukaa pamoja kuunda maneno mbalimbali katika lugha zinazotumika.

Wanaisimu wengi wamekubali kuwa mofolojia kama taaluma hugawika katika matawi mawili makuu yaani mofolojia ya minyambuliko ya maneno namofolojia ya uundaji wa maneno. Mofolojia ya minyambuliko ya maneno hushughulikia zaidi ile minyambuliko ya maneno ambayo huwekwa kwenye mizizi ya maneno kuwakilisha maana mbalimbali lakini minyambuliko hiyo isibadili aina za maneno hayo.

Mofolojia ya uundaji wa maneno ni eneo ambalo hushughulikia mikondo na matokeo ya kiisimu ya uundaji wa maneno kwa kuweka viambishi katika mizizi ya maneno. Kiambishi nyambuaji kinaweza kubadili aina ya neno.Kwa muhtasari basi tunaweza kusema kuwa mofolojia ni tawi la kiisimu linaloshughulika na maneno na vipashio vyote vinavyounda maneno.

#### 3.3.2 Ukiushi wa kiwango cha kimofolojia

Ukiushi wa kimofolojia huhusu mambo kadhaa. Yafuatayo ni baadhi ya mambo haya. Mengi ya makosa haya yalifanywa na wanafunzi wa shule za msingi.

**a) Kuongeza vokali, kwa mfano:**

(i) **'mutu'** badala ya *'mtu',*

(ii) **'muzuri'** badala ya *'mzuri',*

(iii) **'mutoto'** badala ya *'mtoto.'*

Katika lugha ya Kikuyu, sauti /m/ sharti ifuatwe na vokali isipokuwa tu pale inapofuatwa na sauti /b/ kwa sababu sauti hizo mbili ni za midomoni ingawa sauti /b/ ni kipasuo ilhali sauti /m/ ni nazali. Kwa sababu ya uzoefu huo wa kutamka sauti /m/ ikifuatwa na vokali mzungumzaji wa lugha ya Kikuyu hujikuta akiongeza vokali baada ya sauti /m/ hata pale ambapo hapastahili.

**b) Kuongeza 'n' kabla ya 'd'** Kwa mfano:

(i) '**ndunia**' badala ya *'dunia',*

(ii) '**ndunga'** badala ya *'dunga',*

(iii) '**ndanda**' badala ya *'dada'*

Sababu ya kutokea kwa ukiushi huu ni kuwa lugha ya Kikuyu haitumii sauti /d/ bila kutanguliwa na sauti /n/. Kwa hivyo, katika lugha ya Kiswahili, neno lolote linaloanza kwa sauti /d/ mzungumzaji wa lugha ya Kikuyu hujikuta akitamka sauti aliyoizoea ya /nd/.

**c) Kuongeza 'm' kabla ya 'b'.** Mifano:

(ii) **'Mbakora'** badala ya; *'bakora'*

(iii) **'Mbahari'** badala ya; *'bahari'*

(iv) **'Mbasi'** badala ya; **'***basi'*

Katika lugha ya Kikuyu sauti /b/ ikiwa haijatanguliwa na sauti /m/ hudhihirika kama sauti /β/ kwa hivyo pale ambapo inatakiwa kutamkwa kama sauti /b/ mzungumzaji wa lugha ya Kikuyu hujikuta akiitamka kama sauti /mb/ kwani hiyo ndiyo sauti aliyozoea kuitamka katika lugha yake.

**c) Kuongeza 'n' kabla ya 'g'**Mifano:

(i) ***'Ngazeti'*** badala ya; *gazeti*

(ii) ***'Ngunia'*** badala ya; *gunia*

(iii) ***'Ngondoro'*** badala; *godoro*

Maneno tuliyoyaandika kwa herufi za mlazo na ambayo yana ukiushi hudhihirisha vile yanavyotamkwa kwa lugha ya Kikuyu. Mzungumzaji wa Lugha ya Kikuyu huuchukua

muundo huo na kuupeleka katika lugha ya Kiswahili hivyo kusababisha ukiushi wa kimofolojia.

**d) Kuongeza 'n' kabla ya 'j'** Mifano:

(i) **'Njogoo'** badala ya *'jogoo'*

(ii) **'Njaa'** badala ya *'jaa'*

(iii) **'Njali'** badala ya *'jali'*

Katika lugha ya Kikuyu, sauti /j/ sharti itanguliwe na sauti /n/. Kwa hivyo, wazungumzaji wa lugha hiyo huhamisha muundo huo kwa lugha ya Kiswahili.

**e) Msamiati ambao haukutumika kwa maana yake.** Kwa mfano:

(i) **'buda'** kumaanisha *'baba'*

(ii) **'Baby'** kumaanisha *'msichana'*

*(iii)* **'Chari'** kumaanisha *'mvulana mtu mzima'*

Tulikisia kwamba ukiushi huu ulitokana na kuathiriwa na lugha ya sheng' kutoka kwa wanafunzi waliotoka mijini.

**f) Uchopekaji wa irabu /u/**

Baadhi ya watafitiwa walichopeka irabu /u/ isipostahili. Mifano:

(i) **'Niliamuka'** badala ya *'niliamka'*

(ii) **'Sikumukuta'** badala ya *'sikumkuta'*

(iii)**'Umuri'** badala ya *'umri'*

**g) Tafsiri ya moja kwa moja.** Mifano:

(i) **'Wavulana *wanakunywa* sigara'** badala ya; '*wavulana* ***wanavuta*** *sigara.'*

(ii) ***Nasikia*** **njaa** badala ya; *nahisi njaa*

(iii) **Alikuwa *anaangalia* kipindi radioni** badala ya; *Alikuwa* ***anatazama*** *kipindi kwenye televisheni*

(iv) **Nilikuja *na* miguu** badala ya; *Nilikuja* ***kwa*** *miguu.*

(v) **Nitakula ugali *na* sukumawiki**, badala ya; *Nitakula ugali* ***kwa*** *sukumawiki.*

Makosa haya hutokana na ukosefu wa msamiati unaosababishwa na kutojua. Makosa mengi ya aina hii yalidhihirika zaidi katika mazungumzo ya wanafunzi wa shule za msingi.

**h) Muundo wa silabi usiofaa.**

Baadhi ya wazungumzaji waliongeza kiyeyusho /y/ baada ya vokali /i/. Kwa mfano.

(i) ***Miyale*** ya jua ilitumulika uwanjani, badala ya; ***Miale*** ya jua ilitumulika tukiwa uwanjani.

(ii) Tumebakisha ***miyezi*** miwili tufanye mtihani, badala ya; Tumebakisha ***miezi*** miwili tufanye mtihani.

(iii) ***Miyenendo miyema*** ndiyo tunataka badala ya; ***Mienendo miema*** ndiyo tunataka.

**i) Uyeyushaji**

Makosa mengine yaliyopatikana ni kuyeyusha irabu na kuwa kiyeyusho. Katika uyeyushaji, irabu /i/ hubadilika na kuwa kiyeyusho /y/ ilhali irabu /u/ hubadilika na kuwa kiyeyusho /w/. Sababu hasa huwa ni kuepuka ufuatanaji wa irabu mbili. Pia kuunda muundo \wa silabi uliopendelewa. Kwa mfano:

(iv) Watoto ***mwendelee*** vivyo hivyo. badala ya; Watoto ***muendelee*** vivyo hivyo.

(v) ***Mwelewane*** bila kupigana. badala ya; ***Muelewane*** bila kupigana.

Maneno haya yaliyo na makosa yanaendelezwa yakifuata kanuni za lugha ya Kikuyu ambayo ina silabi ya KKV iliyopigwa mstari lakini haina muundo wa silabi ya KII iliyopigwa mstari. Kwa hivyo ni vigumu kupata muundo huu wa KII katika maneno asilia ya Kikuyu.

**j) Kubadili msimbo**

Baadhi ya walimu na wanafunzi walitumia maneno ya lugha nyingine isipokuwa ile ya Kiswahili katika mazungumzo yao. Ifuatayo ni mifano tuliyoisikia:

(i) Nipe chapati nami nikupe '***ngwachii,***' badala ya***;*** Nipe chapati nami nikupe ***viazi vitamu.***

(ii) Huyu ndiye ***'boss'*** wangu, badala ya; Huyu ndiye ***mkubwa*** wangu.

(iii) Shule yetu itapewa '***supervisor'*** yupi? Badala ya; shule yetu itapewa ***msimamizi*** yupi?

(iv) Sitaki ***'excuses,'*** enda umlete mzazi, badala ya; Sitaki ***mazingizio,*** enda umlete mzazi.

(v) ***'Cucuu'*** hapendi '***chapoo'***, badala ya ***nyanyangu*** hapendi ***chapati.***

**3.4 Hitimisho**

Sababu za makosa mengi kutokea ni kuathiriwa na lugha ya kwanza. Wanafunzi wengi hutatizwa na L1 na hili huchangia katika baadhi ya makosa yanayofanywa katika harakati zakujifunza L2. Hii ni kwa sababu wakati mwanafunzi anapojieleza katika lugha lengwa, atarejelea lugha ambayo anaifahamu vizuri na ambayo ni L1. Mwanafunzi atahamisha kanuni kutoka L1 hadi L2. Makosa haya yanayofanywa hufanana na sifa za L1 na hivyo utapatakuwa baadhi ya makosa yametafsiriwa moja kwa moja kutoka L1. Hata hivyo mitindo ya L1 huwa muhimu kwa sababu huwa kama msingi wa sarufi za kwanza za wanaojifunza L2. Kwa sababu hii, kuingiliana kwa lugha ni sababu mojawapo inayochangia wanafunzi kufanya makosa haya.

Sababu nyingine iliyochangia kutokea kwa makosa haya ni ufundishaji mbaya kutokana na uelewa mbaya wa mwalimu. Walimu wengi wa Kiswahili sio wazawa wa lugha ya Kiswahili, wamejifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Wakati mwingine mwalimu na mwanafunzi huwa na lugha ya kwanza tofauti, kwa hivyo si rahisi mwalimu kuelewa ugumu alionao mwanafunzi. Huenda ukapata mwalimu naye ameathirika na lugha yake ya kwanza. Kwa sababu mwanafunzi hujifunza lugha kwa kumsikiza mwalimu wake anavyozungumza, wanaposikia matamshi mabaya kutoka kwa mwalimu nao hufanya makosa yayo hayo. Mwanafunzi haelewi kuwa mwalimu amefanya makosa, yeye huyachukua makosa yale na kuyachukulia kama maumbo sahihi, hufanya hivi kwa kusahilisha sarufi ili kufikia uamilifu mpana wa mawasiliano. Kwa mfano, mwanafunzi ametamka 'hio hio' badala ya 'hiyo hiyo.' Vile vile anatamka nguo ***hio ndio ilioshonwa*** na mama, badala ya; Nguo ***hiyo ndiyo iliyoshonwa*** na mama.

Mwanafunzi amedondosha fonimu /y/ ili kurahisisha matamshi. Fonimu /y/ hutumia nguvu nyingi kutamkwa ikilinganishwa irabu /i/. Tukizingatia uainishaji wa ngeli kisintaksia, maneno mengi ya Kikuyu ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili hupatikana katika ngeli tofauti. Kwa hivyo, wazungumzaji wa Kikuyu huzingatia kiambishi awali katika kuunda sentensi na wanapohamisha matumizi haya katika Kiswahili, hufanya makosa. Katika hali hii wanafunzi wanajumuisha makosa kwa kuhamishakanuni za lugha ya kwanza. Kwa mfano, mzungumzaji wa lugha ya Kikuyu husema '***nguku yakwa'*** inayomaanisha kuku wangu. Katika lugha ya Kiswahili, atajikuta akisema '***kuku yangu.'*** Isitoshe, tumegundua kuwa kuna tofauti kati ya miundo ya maneno ya lugha hizi mbili. Tofauti hizo huathiri matumizi ya Kiswahili kwa kiwango fulani.

## SURA YA NNE

### 4.0 Makosa ya kimaongezi ya kiwango cha kimofosintaksia

### 4.1 utangulizi

Watu wanapozungumza hufanya makosa mbalimbali. Makosa haya yanaweza kuwa ya kifonetiki, kimofolojia, kisintaksia, kimofosintaksia au ya kisemantiki. Kila mojawapo ya makosa haya huathiri mawasiliano. Kwa hivyo kila mzungumzaji hana budi kujiepusha na makosa ili kufanikisha mawasiliano.

Kuna makosa yanayofanywa mara nyingi na watu wengi kuliko makosa mengine. Makosa yanayofanywa na wazungumzaji huwa tofauti kutegemea kiwango cha elimu, makazi, muktadha wa mazungumzo na hali ya kiafya ya mzungumzaji. Makosa haya huwa tofauti na yanaweza kugawanywa katika makundi manne kama anavyodokeza Mbaabu (1995). Makundi hayo ni pamoja na makosa ya kimatamshi, makosa ya kisarufi, makosa ya kimaana na makosa ya kimaandishi.

Anaendelea kusema kuwa makundi haya manne huingiliana hivi kwamba kosa la kimatamshi linaweza pia kuwa la kisarufi na linaweza kuathiri maana ya matamshi au maandishi. Mengi kati ya makosa ya kimatamshi yanatokana na maingiliano kati ya lugha ya kwanza na Kiswahili sanifu.

Nia na azma ya kuufanya utafiti kuhusu makosa ya kimofosintaksia ni kuyafahamu makosa yanayofanywa na wanafunzi na walimu wa shule nne za Kangema, kung'amua sababu za kutokea kwayo na kubuni njia za kuyarekebisha makosa hayo au kuyapunguza kabisa.

Ni ukweli usiopingika kuwa lugha hubadilika kwa kukua, kufifia ua hata kufa. Kwa hivyo ni makosa kudai kwamba tafiti zilizofanywa awali zitaweza kuendelea kutufaa milele. Kuna mabadiliko yanayosababishwa na teknolojia, mabadiliko yanayoletwa na athari za maingiliano ya watu wa makabila mbalimbali na yale yanayoletwa na kuibuka kwa msamiati mpya. Hivyo basi ni muhimu kufanywa kwa tafiti zingine mara kwa mara ili kukabiliana na kuborongwa kwa lugha kunakosababishwa na yale tuliyokwisha kuyataja na mengine mengi. Kwa mfano, makosa mengi ya kisarufi yanahusu kuchanganya viambishi vya ngeli tofauti

hasa viambishi vya hali ya umoja na wingi vya ngeli ya I-ZI. Kunayo pia makosa yanayosababishwa na athari za lugha ya kwanza. Tulipokuwa tukifanya utafiti wetu tuliingiliana na walimu na wanafunzi moja kwa moja, Tulifanya hivyo tukiwa katika mazingira ya shuleni. Tuliyakusanya makosa yaliyofanywa kimaongezi na kuyaorodhesha bila kufuata utaratibu maalum.

Baadaye tuliyaweka katika makundi kulingana na aina na sababu za kutokea kwa makosa hayo. Kwanza tuliyaorodhesha huku tukizingatia kuvunjwa kwa kanuni za upatanifu wa viambishi katika ngeli tofautitofauti. Hatimaye tuliyaorodhesha makosa yaliyosababishwa na athari za lugha ya kwanza.

## 4.2 KATEGORIA ZA MAKOSA

### 4.2.1 Makosa yanayohusu ukosefu wa upatanifu katika ngeli za nomino.

Makosa haya ni ya kisarufi kwa sababu yanahusu upatanifu wa viambishi katika ngeli. Ujuzi wa matumizi ya ngeli katika lugha sanifu ya Kiswahili ni muhimu sana. Maana kama asemavyo Mbaabu (1995), ngeli ndio uti wa mgongo wa sarufi ya Kiswahili na makosa hutokea mara tu viambishi visivyofaa vinapotumiwa katika sentensi. Makosa haya vilevile hudhihirika katika kirai na kishazi. Katika utafiti wetu tulikuja kugundua kwamba makosa haya ni mengi mno.

Ili kuweza kuyabainisha kwa uwazi zaidi, tuliyapanga kama yanavyodhihirika katika kila ngeli. Vile vile tuliyapanga kulingana na kisababishi cha kila kosa. Kama tulivyodokeza hapo awali, makosa haya ni mengi sana na kwa hivyo tuliweza kuandika mifano tu. Hivi ni kumaanisha kuwa kuna makosa mengine ya aina hii lakini hatukuweza kuyaorodhesha.

#### 4.2.1.1 NGELI YA A-WA

Hii ni ngeli ya majina ya viumbe wenye uhai na damu. Huchukua kiambishi ngeli **a-** katika hali ya umoja na kiambishi ngeli **wa** katika hali ya wingi. Sentensi, kishazi au hata kirai kinachokaidi kanuni hii husemekana kuwa ina makosa ya kisarufi. Makosa haya tuliyaweka katika makundi na kutoa mifano mitatu au minne kama tulivyoyasikia.

a) **Kuacha viambishi**

Makosa mengi ya kuacha viambishi yalitokea pale ambapo wazungumzaji walikosa kupatanisha nomino za ngeli hii na vivumishi vya sifa. Walifanya hivyo kwa kudondoa viambishi. Tutazame mifano:

(i) **'Sungura zuri'** badala ya; *sungura mzuri.*

(ii) **'Walimu chache'** badala ya; *walimu wachache.*

(iii) **'Watoto baya'** badala ya; *watoto wabaya.*

(iv) **'Mkulima chafu'** badala ya; *mkulima mchafu.*

b) **Wengine waliongeza kiambishi kisichostahili.**

Kwa mfano:

(i) **'Mtoto huyu ni *m*safi.'** badala ya; *Mtoto huyu ni safi.*

(ii) **'Watoto hawa ni *wa*safi.'** badala ya; *Watoto hawa ni safi.*

(iii) **'Mamake alikuwa *m*tasa'** badala ya**;** *Mamake alikuwa tasa.*

(iv) **'Rais Uhuru Kenyatta ni *m*shujaa'** badala ya; *Rais Uhuru Kenyatta ni shujaa.*

c) **Matumizi yasiyofaa ya kirejeshi 'o' cha kati na cha mwisho**

Makosa haya yalidhihirika zaidi katika maongezi ya walimu majilisini na watoto wakicheza uwanjani. Baadhi yalisikika kutoka kwa walimu wakifunza darasani.

Mifano ni kama ifuatayo:

*(i)* '**Watoto wana*ye*chelewa wataadhibiwa.**' badala ya; *Wanafunzi wanaochelewa wataadhibiwa.*

(ii) **'Niletee kiroboto uli*cho*kipata.'** badala ya; *Niletee kiroboto uliyempata.*

(iii) **'Ngombe za shule zili*zo*nunuliwa'** badala ya; *Ng'ombe wa shule walionunuliwa.*

d) **Makosa ya kushindwa kutumia kirejeshi 'o' cha tamati.**

(i) **'Mwalimu aendae'** badala ya; *mwalimu aendaye*

(ii) **'Mtoto afukuzwao'** badala ya; *mtoto afukuzwaye*

*(iii)* **'Mtayarishaji wa pombe ashikwao**' badala ya; *Mtayarishaji wa pombe ashikwaye.*

e) **Kushindwa kutumia kirejeshi 'o' cha kati**

*(i)* **'Wanywaji wa pombe watakayeshikwa'** badala ya; *Wanywaji wa pombe watakaoshikwa.*

*(ii)* **'Mitume inayopatikana katika bibilia'** badala ya; *Mitume wanaopatikana katika bibilia.*

(iii) **'Kiziwi kilichotajwa'** badala ya; *Kiziwi aliyetajwa.*

f) **Baadhi ya wazungumzaji waliondoa kirejeshi 'o' katika sentensi**. Mifano:

(i) **'Ng'ombe anaenda ni wangu**' badala ya**;** *Ng'ombe anayeenda ni wangu.*

*(ii)* **'Marafiki wanacheka wanapendana'** badala ya; *Marafiki wanaocheka wanapendana.*

*(iii)* **'Wanasiasa walitukanana wataadhibiwa'** badala ya; *Wanasiasa waliotukanana wataadhibiwa.*

g) **Wengine walitumia kirejeshi 'amba' pamoja na kirejeshi 'o' katika sentensi moja.**

Mifano:

*(i)* **'Mhubiri *ambaye* aliyehubiri alitufurahisha**' badala ya; *Mhubiri ambaye alihubiri alitufurahisha.*

*(ii)* **'Wanafunzi *ambao* waliochelewa waadhibiwe'** badala ya; *Wanafunzi ambao walichelewa waadhibiwe.*

*(iii)* **'Wasichana ambao wanaokuwa wachafu hukasirisha**.' badala ya***;*** *Wasichana ambao wanakuwa wachafu hukasirisha.*

h) **Matumizi yasiyofaa ya viambishi ngeli vya ngeli hii.**

Mifano ni kama ifuatayo:

(i) **'Ng'ombe *zi*naenda mtoni'** badala ya; *Ng'ombe wanaenda mtoni.*

*(ii)* **'Mbuzi *i*nakula mahindi'** badala ya; *Mbuzi anakula mahindi.*

*(iii)* **'Ng'ombe *i*lichinjwa'** badala ya; *Ng'ombe alichinjwa.*

i) **Upatanisho usiofaa wa viashiria/vionyeshi.**

Mifano:

(i) **'Kuku *zilezi*nataga**.' badala ya; *Kuku wale wanataga.*

(ii) **'Vipepeo *hivyovi*napendeza.'** badala ya; *Vipepeo hao wanapendeza.*

(iii) **'Nguruwe *hiii*menona.'** badala ya; *Nguruwe huyu amenona.*

j) **Matumizi potovu ya vimilikishi vya nafsi zote tatu.**

a) Nafsi ya kwanza: Mifano:

(i) **'Ng'ombe *yangu* imezaa**.' Badala ya; *Ng'ombe wangu amezaa.*

(ii) **'Kifaranga *changu* kinanenepa**.' badala ya; *Kifaranga **wangu** ananenepa.*

(iii) **'Madaktari *yetu* ya Kenya wanawajibika.'** badala ya; *Madaktari **wetu** wa Kenya* **wanawajibika.**

b) Nafsi ya pili: Mifano ya makosa:

(i) **'Chura *chake* kiliruka mtoni.'** badala ya; *Chura **wake** aliruka mtoni.*

(ii) **'Samaki *zako* zimeoza.'** badala ya kusema; *Samaki **wako** wameoza.*

(iii) **'Sungura *yako* ilikula majani?'** badala ya; *Sungura **wako** alikula majani?*

c) Nafsi ya tatu. Mifano ya makosa:

*(i)* **'Vifaranga *vyao* vinapiga kelele**.' badala ya kusema; *Vifaranga **wao** wanapiga kelele.*

*(ii)* **'Kuku *zao* hutaga mayai mengi.'** badala ya kusema; *Kuku **wao** wanataga mayai mengi.*

(iii) **'Ndege *yake* ilitoroka**.' badala ya; *Ndege **wake** alitoroka.*

I) **Matumizi yasiyofaa ya 'a' unganifu**.

Mifano katika sentensi:

*(i)* **'Ng'ombe *za* jirani zinatoa maziwa mengi.'** badala ya; *Ng'ombe **wa** jirani wanatoa maziwa mengi.*

(ii) **'Mtoto *ya* shule asiajiriwe'** badala ya; *Mtoto **wa** shule asiajiriwe.*

*(iii)* **'Mitume ile *ya* zamani inayotajwa katika bibilia.'** badala ya; *Mitume wale **wa** zamani wanaotajwa katika bibilia.*

J) **Matumizi yasiyofaa ya 'ndi' sisitizi**.

Mifano ya matamshi potovu yaliyosikika:

*(i)* **'Mimi *ndiye* niliyemwona.**' badala ya; *Mimi **ndimi** niliyemwona.*

*(ii)* **Ng'ombe hizi *ndizo* zitakazokamwa** badala ya; *Ng'ombe hawa **ndio** watakaokamwa.*

**(iii) Sisi *ndio* walimu wa shule hii.'** badala ya; *Sisi **ndisi** walimu wa shule hii.*

#### 4.2.1.2 Ngeli ya U-I

Obuchi na Mukhwana (2010) wanasema kuwa ngeli hii hutokana na majina kuambishwa kiambishi **'m'** katika hali ya umoja na **'mi'** katika hali ya wingi yanapoambatana na vivumishi.

Ngeli hii ni ya majina yanayochukua kipatanishi **'u'** na **'i'** katika hali ya umoja na wingi mtawalia. Makosa yafuatayo yalidhihirika.

**a) Kudondosha na kuongeza viambishi;**

Mifano:

*(i)* **'Mkate uliokuwa *msafi* tuliupenda**.' Alistahili kusema; *Mkate uliokuwa **safi** tuliupenda.*

*(ii)* **Mfuko baya unaweza kupoteza vitabu** badala ya; *Mfuko **mbaya** unaweza kupoteza vitabu.*

*(iii)* **'Mikutano *ingine* haifai wakati wa usiku'** badala ya; *Mikutano **mingine** haifai wakati wa usiku.*

**b) Matumizi yasiyofaa ya kirejeshi 'o'**

**Mifano:**

(i) **'Miti ili*o*katwa'** badala ya; *miti iliyokatwa.*

(ii) **'Mlima watoto wali*yo*upanda'** badala ya; *mlima watoto walioupanda.*

(iii) **'Mfupa uli*yo*utupa'** badala ya; *mlima ulioutupa.*

**c) Kushindwa kutumia vivumishi mahsusi/vya pekee/halisi vizuri.**

Vivumishi hivi ni kama vile –enye, -enyewe, -ote, –o-ote na –ngine.

Mifano ya makosa:

(i) **'Mjeledi *mwenyewe* ulipotea.'** badala ya kusema; *Mjeledi **wenyewe** ulipotea.*

*(ii)* **'Miti *ingine* iliyopandwa imekauka.'** badala ya; *Miti **mingine** iliyokatwa imekauka.*

(iii) **'Mkate *mwenye* utamu utaliwa.'** badala ya; *Mkate **wenye** utamu utaliwa.*

d) **Matumizi yasiyofaa ya vimilikishi.**

Mifano:

(i) **'Mikono zangu zinauma'** badala ya; *Mikono yangu inauma.*

(ii) **'Usiutupe mpira yangu'** badala ya; *Usiutupe mpira wangu.*

(iii) **'Hatutaki mikutano zenu za ujinga'** badala ya; *Hatutaki mikutano yenu ya ujinga.*

**e) Kukosa upatanisho mzuri wa viashiria. Mifano:**

(i) **'Mikeka *hizo* hazijaoshwa.'** badala ya; *Mikeka* ***hiyo*** *haijaoshwa.*

(ii) **'Mpango *hiyo* haitafaa.'** badala ya; *Mpango* ***huo*** *hautafaa.*

(iii) **'Nirudishie mikate *zangu*'** badala ya; *Nirudishie mikate* ***yangu****.*

**f) Matumizi yasiyofaa ya 'a' unganifu. Mifano:**

(i) **'Michungwa *za* jirani'** badala ya; *Michungwa ya jirani*

(ii) **'Moyo *ya* mtoto'** badala ya; *Moyo wa mtoto.*

(iii) **'Kuna mkutano *ya* walimu'** badala ya kusema; *Kuna mkutano wa walimu.*

**g) Baadhi walishindwa kutumia *'ndi'* sisitizi vizuri. Walisema:**

(i) **'Mikebe *ndio* hii,'** badala ya; Mikebe *ndiyo* hii.

(ii) **'Hizi *ndizo* mifupa *za* mbwa.'** badala ya; *Hii ndiyo mifupa ya mbwa.*

(iii) **Mpaka huu *ndiyo* wa shule yetu.'** badala ya; Mpaka huu *ndio* wa shule yetu.

### 4.2.1.3 Ngeli ya LI-YA

Hujumuishanomino zinazochukua upatanisho wa kiambishi ngeli ***'li'*** na ***'ya'*** katika umoja na wingi mtawalia. Nomino hizi huhesabika. Ngeli hii ilikumbwa na matatizo mengi zaidi kuliko ngeli zote. Makosa ya kimofosintaksia yalikuwa chungu kizima. Tuliandika baadhi ya makosa hayo.

**a) Kudondosha na kuongeza viambishi.**

Mifano:

*(i)* **'Tunda *li*zuri litapewa mtoto mwerevu.'** badala ya; *Tunda zuri litapewa mtoto mwerevu.*

*(ii)* **'Tunda *m*baya halitaliwa'** badala ya; *Tunda baya halitaliwa.*

(iii) **'Likariri shairi *n*zima'** badala ya; *Likariri shairi zima.*

(iv) **'Shati *m*bovu lisivaliwe'** badala ya; *Shati bovu lisivaliwe.*

**b) Matumizi yasiyofaa ya 'o' rejeshi**

Mifano ya makosa tuliyokubana nayo:

(i) **'Godoro nili*yo*nunuliwa'** badala ya; godoro nili*lo*nunuliwa.

(ii) **'Matatizo tuli*zo*kuwa nazo Januari'** badala ya; matatizo tuliyokuwa nayo Januari.

(iii) **'Soko ili*yo*uziwa matunda'** badala ya; soko lili*lo*uziwa matunda.

**c) Matumizi yasiyofaa ya viambishi vinavyopatanishwa na vivumishi vya sifa.**

Shida kubwa ilidhihirika katika matumizi ya vivumishi vya sifa vinavyochukua viambishi ngeli k.v -refu, -embamba, -eupe, -dogo na –zuri. Makosa mengi yalipatikana pale ambapo mzungumzaji alitakiwa kutunga sentensi iliyo katika hali ya umoja.Mifano:

(i) **'Shati *nyeupe* itapata uchafu haraka.'** badala ya; Shati *jeupe* litapata uchafu haraka.

(ii) **'Dirisha *ndogo* haitaingiza mwangaza'** badala ya; Dirisha *dogo* halitaingiza mwangaza.

*(iii)* **'Darasa lenu lina dirisha *nyembamba*'** badala ya; *Darasa lenu lina dirisha jembamba.*

d) **Upatanisho usiofaa wa viashiria.** Mifano:

(i) **'Rinda *hiyo* isije shuleni kesho.'** badala ya; Rinda *hilo* lisije shuleni kesho.

(ii) **'Parachichi *hii* imeiva.'** badala ya; Parachichi *hili* limeiva.

(iii) **'Maandishi *hii* ina makosa.'** Alistahili kusema; Maandishi *haya* yana makosa.

**e) Upatanisho usiofaa wa vimilikishi**

Ilidhihirika wazi kwamba wazungumzaji wengi hawakuweza kutofautisha kati ya vimilikishi vinavyopatanishwa na nomino za ngeli ya **I-ZI** na vile vinavyopatanishwa na ngeli ya LI-YA. Baadhi ya wazungumzaji walisema:-

(i) **'Shati *yake* imeraruka'** badala ya; **Shati lake limeraruka.**

(ii) **'Marinda *zenu* zikiraruka zishonwe'** badala ya; **marinda yenu yakiraruka yashonwe.**

(iii) **'Soko *yenu* ni ya Gakira?'** Badala ya; soko *lenu* ni la Gakira?

**f) Matumizi yasiyofaa ya 'a' unganifu**

Wazungumzaji wengi walipendelea kutumia viambishi vya ngeli ya **I-ZI** badala ya vile vya ngeli ya LI-YA. Chunguza mifano ifuatayo.

(i) **'Magari *za* abiria'** badala ya; magari *ya* abiria.

(ii) **'Majina *za* wanafunzi'** badala ya; **majina ya wanafunzi.**

(iii) **'Jina *ya* mamangu'** badala ya; **jina la mamangu.**

(iv) **'Peleka parachichi *ya* mwalimu majilisini.'** badala ya; **peleka parachichi *la* mwalimu majilisini.**

g) **Kushindwa kutumia vivumishi vya sifa vizuri wengi wao au waliongeza viambishi visivyostahili ama kuviondoa vinavyostahili kuwepo.** Mifano:

(i) **'Darasa *nzuri* ni lile lililooshwa.'** badala ya; Darasa *zuri* ni lile lililooshwa.

(ii) **'Mwalimu alinipa tunda *ndogo.'*** badala ya; Mwalimu alinipa tunda *dogo*.

(iii) **'Ulikate ua *nyeupe* uache ile nyekundu.'** badala ya; Ulikate ua *jeupe* uache lile jekundu.

**h) Kutoweza kutumia 'ndi' ya kutilia mkazo** ipasavyo. **Mifano ya makosa ni pamoja na:**

(i) **'Madarasa *ndio* yataoshwa kwanza.'** badala ya; Madarasa *ndiyo* yataoshwa kwanza.

(ii) **'Yai yangu *ndiyo* kubwa.'** badala ya; **'Yai langu *ndilo* kubwa.'**

(iii) **'Soko *ndiyo* itajengwa kwanza kisha tutengenezewe barabara.'** Badala ya; Soko *ndilo* litajengwa kwanza kisha tutengenezewe barabara.

(iv) **'Tumbo *ndiyo* sehemu ya mwili iliyo muhimu kuliko sehemu nyingine.'** Badala ya; Tumbo *ndilo* sehemu ya mwili iliyo muhimu kuliko sehemu nyingine.

### 3.2.1.4 Ngeli ya KI-VI

Makosa yaliyohusishwa na kutotumia viambishi vya ngeli hii inavyostahili yalionekana kwamba yalisababishwa na kupendelea kutumia viambishi vya ngeli ya **I-ZI** zaidi ama kutoka na athari za lugha ya kwanza au kwa kutojua.

a) **Kudondosha au kuongeza viambishi.**Mifano katika sentensi:

(i) '**Nunua vijiko *visita.'*** badala ya kusema; Nunua vijiko *sita*.

(ii) **'Kitanda *ndefu* ni cha baba.'** badala ya; Kitanda *kirefu* ni cha baba.

(iii) **'Chakula *nzuri* kinatamanisha.'** Badala ya; Chakula *kizuri* kinatamanisha.

(iv) **'Kijiko *ndogo* kitatoshea kinywani.'** badala ya; Kijiko *kidogo* kitatoshea kinywani.

**b) Matumizi yasiyofaa ya 'o' rejeshi.**

Wahusika wengi ambao ni wanafunzi na walimu wasiofunza Kiswahili walionyesha matatizo ya kushindwa kutumia 'o' rejeshi ipasavyo.Walifanya makosa kama yafuatayo:

*(i)* **'Kioo *i*li*yo*vunjwa na mtoto *i*pelekwe ofisini.'** badala ya kusema; *Kioo kilichovunjwa na mtoto kipelekwe ofisini.*

*(ii)* **'Kitabu yangu niliyokupa.'** badala ya; *Kitabu changu nilichokupa.*

*(iii)* **'Kipindi tuliyopoteza itafunzwa kesho.'** badala ya; *Kipindi tulichopoteza kitafunzwa kesho.*

**c) Matumizi mabaya ya 'a' unganifu. Kwa mfano:**

(i) **'Vikombe *za* walimu zilioshwa na mpishi.'** badala ya; Vikombe *vya* walimu vilioshwa na mpishi.

(ii) **'Choo moja *ya* wavulana haikuoshwa.'** badala ya; Choo kimoja *cha* wavulana haikuoshwa.

(iii) **'Pelekeni viti *za* walimu.'** badala ya**;** Pelekeni viti *vya* walimu.

(iv) **'Kiranja aniletee vitabu *za* insha baadaye.'** Badala ya kusema; Kiranja aniletee vitabu *vya* insha baadaye.

**d) Matumizi potovu ya vivumishi.** Mifano ya makosa:

*(i)* **'Viti ndogo ya watoto wa chekechea.'** badala ya kusema; *viti vidogo vya watoto wa chekechea.*

(ii) Badala ya kusema **Ukitumie kijiti *chembamba* kumpiga mtoto,** mwalimu mmoja alisema 'Ukitumie kijiti *kiembamba* kumpiga mtoto'

(iii) **Walivipeleka viti vile *ndefu* ukumbini.'** badala ya; Walivipeleka viti vile *virefu* ukumbini.

**e) Upatanisho mbaya wa vimilikishi. Mifano ya makosa:**

- **'Vikombe *zetu* si safi.'** badala ya; Vikombe *vyetu* si safi.

(i) **'Kiatu *yangu* ni ya rangi nyeupe'** badala ya**;** *Kiatu changu ni cha rangi nyeupe.*

*(ii)* **'Vitendo *zenu* zilimkasirisha mwalimu wa zamu.'** badala ya; *Vitendo vyenu vilimkasirisha mwalimu wa zamu.*

**f) Matumizi yasiyofaa ya 'a' unganifu. Tazama mifano:**

*(i)* **'Weka kikomo *ya* kuonyesha mwisho wa sentensi.'** Badala ya kusema; *Weka kikomo cha kuonyesha mwisho wa sentensi.*

(ii) **'Onyesheni vitambaa*za* kupengea makamasi.'** Badala ya; Onyesheni vitambaa *vya* kupengea makamasi.

(iii) **'Uende ukalete viazi vitamu *za* kumpa mwalimu wetu**.' Badala ya; uende ukalete viazi vitamu *vya* kumpa mwalimu wetu.

**g) Matumizi yasiyofaa ya 'ndi' ya kutilia mkazo.**

Walimu na wanafunzi wengi waliweza kutumia 'ndi' ya kutilia mkazo katika ngeli hii ingawa kuna baadhi ya makosa yaliyopatikana. Kwa mfano:

(i) **'Hiki *ndikio* kitabu *kiangu.'*** badala ya; Hiki *ndicho* kitabu changu.

(ii) **'Hizo *ndizo* vijiko chafu.'** badala ya; Hivyo *ndivyo* vijiko vichafu.

(iii) Badala ya kusema; **Hivi *ndivyo* viatu vya shule** mtoto alisema; 'Hizi *ndizo* viatu za shule viatu.'

### 4.2.1.5 Ngeli ya I-ZI

Ngeli hii ndiyo iliyopendelewa zaidi na wazungumzaji wengi katika shule tulizozuru. Walimu na wanafunzi wengi walionekana kuegemea upande wa matumizi ya vipatanisho au viambishi vya ngeli hii ama kwa kutojua au kwa kuathiriwa na lugha ya kwanza. Hata hivyo, baadhi walifanya makosa kwa kutumia vipatanisho visivyofaa vya ngeli hii. Mifano ya makosa yaliyofanywa ni kama yafuatayo:

a) **Kudondosha, kubadilisha au kuongeza viambishi ngeli wanapotumia vimilikishi.**

Mifano:

(i) **'Hatutaki meza *ingine.'*** badala ya; Hatutaki meza *nyingine.*

(ii) **'Karatasi *zuri* ndiyo inatakikana.'** badala ya; Karatasi *nzuri* ndiyo inayotakikana.

(iii) **'Mashini mawili ya kushonea nguo yalipotea.'** badala ya; Mashini mbili za kushonea nguo zilipotea.

*(iv)* **'Lugha mingi za kiafrika.'** badala ya; *Lugha nyingi za kiafrika.*

b) **Kutumia wingi wa nomino kimakosa na kwa hivyo kubadilisha upatanisho wa kisarufi.** Mifano;

(i) ***'Mashule*** **hayo mengine yametushinda.'** badala ya; *Shule* hizo zingine zimetushinda.

(ii) ***'Manyumba*** **yenu yawe yanafagiliwa.**' badala ya kusema**;** *Nyumba* zenu ziwe zinafagiliwa.

(iii) ***'Makaratasi*** **ambayo yataandikiwa yawe safi'** badala ya; *Karatasi* ambazo zitaandikiwa ziwe safi.

c) **Kulikuwa na wazungumzaji ambao walisikika wakiongeza sauti /y/ katika mazingira ambayo haikuhitajika na kuidondosha ilipohitajika**. Mifano:

(i) Neno '**ziara'** tunayoitayarisha itakuwa ya kupendeza; lilitamkwa kimakosa hivi: ***Ziyara*** tunayoitayarisha itakuwa ya kupendeza.

(ii) **'Shule yetu ni shule *ipendwao* na wazazi.'** badala ya kusema; Shule yetu ni shule *ipendwayo* na wazazi.

(iii) ***'Njia hio'*** badala ya; *njia hiyo.*

(iv) **Usipitiye njiya** ya mkato badala ya kusema **usipitie njia** ya mkato.

d) Upatanisho usiofaa wa viashiria pia ulidhihirika katika mifano ya sentensi zifuatazo:-

(i) **'Blauzi *hili'*** badala ya; *blauzi hii.*

(ii) **'Mablauzi *haya'*** badala ya; *blauzi hizi.*

(iii) **'Usiposoma kwa bidii utapatwa na *mashida* kama haya**.' Alistahili kusema kuwa, Usiposoma kwa bidii utapatwa na *shida* kama hizi.

(iv) **Tengeneza *masiku zako za* usoni'** badala ya kusema; Tengeneza *siku zako* za usoni leo.

(v) **Ndege *i*nayokula nafaka *i*naweza kuliwa na baadhi ya watu**; Badala ya; Ndege *a*nayekula nafaka anaweza kuliwa na baadhi ya watu.

e) **Matumizi ya msamiati usiostahili, hivyo kubadilisha maana ya sentensi au kutunga sentensi ambayo si sahihi kimantiki.** Mifano ya sentensi kama hizi ni:

(i) **'Mkipata alama mia nne nitawaandalia kalamu ya kukata na *choka.*'** badala ya kusema; Mkipata alama mia nne nitawaandalia *karamu* ya kukata na shoka.

*(ii)* **'Ukija kesho ukiwa umechelewa nitakupi*ka'* badala ya kusema'** *Ukija ukiwa umechelewa nitakupiga.*

(iii) **'Kuku *wanachakulachakula* nyuma ya darasa wakitafuta chakula.'** badala ya kusema; Kuku *wanachakurachakura* nyuma ya nyumba wakitafuta chakula.

*(iv)* **'Baba alimnunulia nyanyangu suka.'** badala ya; *Baba alimnunulia nyanyangu shuka.*

### 4.2.1.6 Ngeli ya U-ZI

Makosa yaliyohusishwa na ngeli hii ni kama yafuatayo:-

a) **Kuongeza au kubadilisha viambishi pasipostahili au kudondosha viambishi vinavyostahili kuwepo.** Mifano ya sentensi:

(i) **'Uzi ina*yo*tumiwa'** badala ya; uzi una*o*tumiwa

(ii) **'Ukuta *i*lipakwarangi.**' badala ya; ukuta *u*lipakwa rangi

(iii) **'Nyufa ya ukuta *i*napitisha upepo**.' badala ya; **Nyufa za ukuta *zi*napitisha upepo.**

b) **Upatanisho usiofaa wa vivumishi vya pekee**.

Tulikumbana na mifano ya makosa ifuatayo.

(i) **'Mwalimu alisema tuimbe wimbo** *yoyote*.' Mwanafunzi huyo alistahili kusema: Mwalimu alisema tuimbe wimbo *wowote.*

(ii) **'Kata kucha hizi *ingine.'*** badala ya; Kata kucha hizi *zingine*.

*(iii)* **'Ufa mwenyewe utazibwa na mwalimu.'** badala ya; *Ufa wenyewe utazibwa na mwalimu.*

(iv) **'Huyu ananing'olea uzi yangu *yenye* madoadoa.'** badala ya; Huyu ananing'olea uzi wangu *wenye* madoadoa.

c) Kutumia kirejeshi **'amba'** na **'o'** katika sentensi moja. Mifano ya sentensi:

*(i)* **'Ufunguo *ambao* uli*o*tupwa umepatikana'** badala ya; *Ufunguo ambao ulitupwa ulipatikana au ufunguo uliotupwa umepatikana.*

(ii) Badala ya kusema: *Kurasa ambazo zilichafuka zilimkasirisha mwalimu,* mwanafunzi mmoja alisema: '**Kurasa ambazo zilizochafuka zilimkasirisha mwalimu**.'

*(iii)* **Kuta *ambazo* zili*zo*pakwa rangi haziandikiki'** badala ya; *Kuta ambazo zilipakwa rangi haziandikiki.*

### 7.2.1.7 Ngeli ya YA-YA

Nomino katika ngeli hii ziliegemea katika matumizi ya vipatanishi vya ngeli ya **I-I.** Shida hii ilipatikana hasa kwa walimu wasiofunza Kiswahili na asilimia 90 ya wanafunzi wa shule za msingi na zile za upili. Mifano ya sentensi ni kama vile:

(i) **'Maziwa *hiyo* ni tamu.'** badala ya; Maziwa *hayo* ni matamu.

(ii) **'Maziwa *inafanya* mate itiririke.'** badala ya; Maziwa *yanafanya* mate yatiririke.

(iii) **'Machozi yangu *ilitiririka.'*** badala ya; Machozi yangu *yalitiririka.*

(iv) **'Maji ya kuosha darasa *iliisha.'*** badala ya; Maji ya kuosha darasa *yaliisha.*

(v) **'Usinawe mikono kwa maji *hii.*'** badala ya**;** Usinawe mikono kwa maji *haya.*

(vi) **'Mate *hiyo* uliyotema ndiyo iliyomfanya mwenzako akasirike'** badala ya; Mate *hayo* uliyoyatema ndiyo yaliyomfanya mwenzako akasirike.

vii) **'Penga makamasi *hiyo.'*** badala ya; Penga makamasi *hayo.*

### 4.2.1.8 Ngeli ya PA-KU-MU

Makosa yaliyohusishwa na ngeli hii yalikuwa mengi sana.

**a) Wengi wa wahusika wetu hawakuonekana kujali vipatanisho walivyovitumia kwa walitumia vyovyote na hata pia kuvichanganya.** Walifanya mifano ifuatayo ya makosa:

(i) **'Darasani huku kuna uchavu**.' badala ya; *Darasani humu mna uchavu.*

*(ii)* **'Hapa ndiko kwangu.'** badala ya; ***hapa ndipo pangu.***

*(iii)* **'Nilipofagia kulikuwa na uchavu.'** badala ya; *Nilipofagia palikuwa na uchavu au* aseme; *Nilikofagia kulikuwa na uchavu.*

(iv) **'Humu ndimo ambako mtakaa**.' Badala ya; *Humu ndimo ambamo mtakaa.*

*(v)* **'Mahali kwenyewe ndipo kuliwapendeza.'** Badala ya**;** *Mahali kwenyewe ndiko kuliwapendeza.*

(vi) **'Mahali kwokwote kunafaa.'** badala ya; *Mahali kokote kufaa.*

(vii) **'Darasani mwomwote mnafaa.'** badala ya; *Darasani momote mnafaa.*

(viii) **'Kwokwote huko kufagiliwe.'** badala ya; *Kokote huko kufagiliwe.*

b) Zaidi ya asilimia 60 ya wahusika wetu walitumia vipatanishi vya ngeli za nomino zilizoambatanishwa na kiambishi tamati '***ni***'cha mahali. Tazama mifano ifuatayo.

*i)* **'Ukutani *ulikuwa* na chati za hisabati**.' badala ya; *Ukutani palikuwa na chati za hisabati.*

ii) **Mwalimu mkuu aliingia darasani *ambalo* halikuwa na watoto.'** badala ya; Mwalimu mkuu aliingia darasani *ambamo* hamkuwa na watoto.

iii) **Nchini Kenya *ina* mamilioni ya watu.'** badala ya; Nchini Kenya *kuna* mamilioni ya watu.

**Kitabuni hiki *kina* picha za kupendeza**. badala ya; Kitabuni humu *mna* picha za kupendeza.

**4.3 HITIMISHO**

Makosa ya kimofosintaksia kwa hakika ni mengi sana. Ukweli ni kwamba hatungeweza kuyaorodhesha yote. Tuliorodhesha mifano tu ya kila aina ya makosa. Hatukuweza kugundua ukweli huu hapo awali kabla ya kuanza uchunguzi huu. Makosa haya yalifanywa kila mara na wanafunzi na walimu. Lililotushangaza zaidi ni kwamba walimu waliokuwa wakifunza Kiswahili walikuwa wakifanya makosa haya mara nyingi lakini bado waliwakemea wanafunzi wao waliofanya makosa yayo hayo.

Wazungumzaji wengi hawakujali kamwe walipokuwa wanazungumza. Walioonekana kujali ni walimu waliokuwa wakifunza Kiswahili darasani lakini hata wao walifanya hivyo tu walipokuwa wakifunza sarufi. Walimu wao hao walionekana kusahau waliyokuwa wamefunza na kuanza kukiuka kanuni za uzungumzaji wa Kiswahili sanifu walipokuwa wakizungumza katika vikao visivyo rasmi na hata vile ambavyo ni rasmi. Halikadhalika walifanya makosa ya walipokuwa wakifunza msamiati.

Tulitaka kujua ni kwa nini baadhi ya walimu walizungumza bila kufanya makosa na kisha kufanya makosa baadaye. Tulimuuliza mmoja wao maswali kuhusu sarufi na akaweza kuyajibu yote bila kufanya makosa yoyote. Jambo hilo lilionyesha kwamba kutokuwa makini ni sababu moja ya kuweko kwa ukiushi dhidi ya kanuni za Kiswahili sanifu.

Ukiushi mwingine ulihusishwa na athari za lugha ya kwanza. Baadhi ya wazungumzaji walihamisha kanuni za lugha ya kwanza ambayo ni Kikuyu moja kwa moja hadi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtoto mmoja alisema: **'Ng'ombe *i*le *i*liyochinjwa *i*likuwa yetu.'** Sentensi hii ikitafsiriwa kwa lugha ya Kikuyu itakuwa: **'Ng'ombe *i*ria *i*rathinjirwo *i*rari**

**itu**.' Ukiiangalia miundo ya maneno katika sentensi hii utaona inakaribiana sana. Mwanafunzi huyu labda alifikiria kwamba alistahili kutumia viambishi vivyo hivyo katika lugha ya Kikuyu. Viambishi vilivyoandikwa kwa herufi za mlazo vitaonyesha wazi ukweli wa dai hili. Sentensi sahihi ni: **Ng'ombe aliyechinjwa alikuwa wetu.**

## SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 MUHTASARI

Utafiti wetu ulinuia kuchanganua makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika mazungumzo ya walimu na wanafunzi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi. Tuligusia kidogo makosa ya kifonolojia na ya kimofolojia kwa sababu makosa haya yote huingiliana na kusababishana. Makosa ya kifonolojia husababisha makosa ya kimofolojia, aidha makosa ya kimofolojia husababisha makosa ya kisintaksia. Makosa yanayosababishwa na mwingiliano wa maneno katika sentensi huitwa makosa ya kimofosintaksia.

Tuligundua kuwa makosa mengi ya kimofosintaksia yalikuwa makosa ya kimatamshi na yalitokana na mazingira na athari ya lugha ya kwanza ya wazungumzaji. Tulishangazwa na ukweli kwamba ukiushi wa kimofosintaksia ulijitokeza pale walimu wa Kiswahili wanapowahutubia wanafunzi katika vikao rasmi. Tuligundua pia kuwa kuna uwezekano wa makosa hayo kurekebishwa kwani walimu waliokiuka kanuni za Kiswahili sanifu katika mazingira yasiyo rasmi waliweza kujirekebisha walipokuwa wakifunza Kiswahili darasani.

Kazi yetu imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ni muhtasari wa jinsi utafiti ulivyofanywa. Imeshughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni, nadharia tete, sababu zakuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tulianza kwa kuziainisha ngeli za lugha ya Kiswahili kisintaksia. Baadaye tulivijadili vikundi vya majina na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya vikundi vya majina na ngeli kwa kuonyesha upatanisho wa kisarufi. Tulifanya hivi ili kuonyesha lugha sanifu ni gani.

Katika sura ya tatu tumeyanasa na kuyaorodhesha makosa haya bila wahusika wetu kufahamu. Tulijadili kidogo kuhusu makosa ya kifonolojia na makosa ya kimofolojia. Tuliwasikiliza walimu wa Kiswahili wakifunza darasani na pia wakiwa nje ya madarasa.

Tuliweza vilevile kuwasikiliza wanafunzi kutoka katika shule tatu za msingi ambazo ni Shule ya Msingi ya Watuha, Shule ya Msingi ya Mukarara na Shule ya Msingi ya Kanyenya-ini. Shule za upili tulizozuru ni Shule ya Upili ya Watuha ambayo ni jirani ya Shule ya Msingi ya Watuha, Shule ya Upili ya Muguru na Shule ya Upili ya Wasichana ya Kiangunyi.

Tumeyaainisha makosa haya kutegemea ngeli na upatanisho wa viambishi ngeli katika makundi mengine ya majina. Tuligudua kuwa kulikuwa na makosa yaliyosababishwa na athari za lugha ya kwanza. Mengine yalisababishwa na kutojali mtu anapozungumza hasa walimu na idadi kubwa ya makosa ilisababishwa na kutojua. Wanafunzi wengi walishindwa kujua ni lini walistahili kutumia viambishi vipatanishi fulani katika tungo.

## 5.2 HITIMISHO

Utafiti huu umedhihirisha wazi kwamba lugha ya Kiswahili katika kaunti ndogo ya Kangema imeathiriwa pakubwa na lugha ya kwanza ambayo ni Kikuyu. Kuathiriwa huku kulitokana sana na uchukulizi kwamba lugha zinafanana kimuundo jambo ambalo si la kweli. Uchukulizi huu uliwafanya na baadhi ya wanafunzi na hata walimu ambao waliweza kuhamisha kanuni za lugha ya Kikuyu hadi kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kweli kuna baadhi ya miundo iliyokaribiana. Hii ni kwa sababu lugha hizi mbili zinatokana na lugha mame moja ambayo ni Kibantu. Matatizo yalitokea pale ambapo mzungumzaji alishindwa kuelewa ni miundo ipi inafanana na ile ya lugha ya kwanza na ni ipi haifanani.

Makosa mengine yalitokana na kutojali na kutokuwa makini wakati wa mazungumzo hasa yale yasiyo rasmi. Jambo hili lilidhihirika wazi walimu wa Kiswahili walipoweza kuongea lugha sanifu ya Kiswahili walipokuwa darasani na kukiuka walipokuwa katika mazingira mengine kama vile uwanjani au majilisini. Walimu waliofanya hivyo waliweza kuwasahihisha wanafunzi wao punde tu walipoingia darasani. Kwa hivyo ilikuwa dhahiri kuwa walimu walikuwa wanauwezo wa kuyarekebisha makosa waliyoyafanya na hata yale yaliyofanywa na wanafunzi wao

Idadi iliyo kubwa ya makosa ilitokana na kutokujua. Jambo hilo lilidhihirika bayana kutokana na ukweli kwamba wanafunzi waliokuwa na umilisi mkubwa wa lugha ya Kiswahili walikuwa ni wale wa viwango vya juu vya elimu. Wanafunzi wa shule za upili waliweza kuzungumza bila kufanya makosa mengi tukiwalinganisha na wale wa viwango vya chini vya elimu. Walimu walifanya makosa machache sana na makosa hayo waliweza kuyarekebisha walipoongea wakiwa makini na wakiwa katika miktadha rasmi.

Jambo hilo linaonyesha wazi kwamba kuna uwezo mkubwa wa kuyapunguza makosa ya kimofosintaksia kwa kiwango kikubwa kwani si rahisi kuyarekebisha makosa hayo kwa asilimia mia moja kwa sababu ya athari ya lugha ya kwanza.

## 5.3 Mapendekezo

Katika sehemu hii tumetoa mapendekezo yatakayowasaidia walimu na wanafunzi wao kupunguza makosa yanayojitokeza katika mazungumzo. Kwa kuwa makosa mengi yalitokana na athari za lugha ya kwanza, tungependekeza walimu watumie mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi katika kulinganua lugha zinazohusika. Itakuwa rahisi kutambua ugumu ambao wanafunzi wanakabiliana nao.

Kwanza mwalimu aweze kugundua vipengele vya lugha vinavyomtatiza mwanafunzi ili aweze kumwelekeza mwanafunzi jinsi ya kutatua ugumu huo. Mwalimu amsaidie mwanafunzi kuelewa kuwa lugha hutofautiana kiisimu, kwa hivyo wasifikirie kwanza katika lugha yao ya kwanza, kisha kutafsiri moja kwa moja kwa lugha lengwa. Wanafunzi wanafaa kujifunga katika lugha lengwa na kufuata kanuni zake.

Wanafunzi wahimizwe kutumia Kiswahili sanifu wanapowasiliana kwa sababu lugha ya mazungumzo inaathiri mno lugha andishi, hivyo kuna uwezekano kuwa wakijieleza barabara katika mazungumzo huenda wakapunguza makosa yanayojitokeza katika kazi andishi. Mwalimu abuni njia za kumpa mwanafunzi fursa ya kuzungumza kwa kufuata kanuni za Kiswahili sanifu. Njia hizo ni pamoja na kukariri mashairi, kushiriki katika mijadala na dayalojia, kusoma ufahamu na hadithi kwa sauti, kutega na kutegua vitendawili, kuimba nyimbo zilizotungwa kwa lugha ya Kiswahili na kusikiliza kwa

makini jinsi walimu wao wanavyozungumza na kutamka vitanza ndimi vingi iwezekanavyo. Mapendekezo zaidi ni kwa mwalimu kurudia dhana ambazo wanafunzi hawakuelewa vyema. Uchanganuzi Makosa utamfaa mwalimu kwa sababu atajua vipengele vya lugha ambavyo vinastahili kutiliwa mkazo kulingana na uzito wa makosa na kuamua ni vipi vitashughulikiwa. Urudiaji huu wa kufunza vipengele vinavyowatatiza wanafunzi huwasaidia kuwa na umilisi wa lugha ufaao.

Tungependekeza walimu waweze kuweka msingi thabiti kuanzia madarasa ya chini ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na umilisi mwafaka wa lugha hii mapema. Msingi bora wa fonimu za Kiswahili utawawezesha wanafunzi kuelewa tofauti iliyoko kifonimu baina ya lugha hizi mbili na hili litawawezesha kuimudu lugha hii mapema. Isitoshe, upungufu na ukosefu wa vifaa bora vya mafunzo umechangia matatizo haya; kwa hivyo tunapendekeza kuwepo vifaa vya kutosha vya kufunzia wanafunzi. Vifaa hivi ni kama vile chati zinazoambatanisha picha, sauti na majina ya picha hizo.

Tunawasihi walimu wote wa Kiswahili wawe katika mstari wa mbele katika kuongoza kupiga vita uborongaji wa lugha ya Kiswahili. Tunawahimiza wafanye juhudi za kimakusudi kuzungumza kwa lugha sanifu ya Kiswahili ili wawe vielelezo bora kwa wanafunzi wao na walimu wengine wasiofunza Kiswahili.

Aidha wakuza mitaala hawakuzingatia kuwepo kwa lugha tofauti nchini Kenya. Wao walichukulia kuwa lugha zote ni sawa na wanaojifunza lugha ya pili hutatizika sawa. Mitaala ilikosa kuonyesha tofauti za kiisimu kati ya lugha asilia na jinsi inavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Ingekuwa vyema ikiwa mitaala ingebainisha tofauti hizi na athari za kila lugha asilia katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Utafiti huu haujashughulikia matatizo yote yanayoikumba lugha ya Kiswahili kwa sababu upeo na mipaka ya utafiti wetu haukuruhusu kusema zaidi. Tungependekeza utafiti ufanywe kubainisha kama makosa haya yanafanana katika maeneo yote nchini Kenya.

Tafiti zingine zifanywe kuchanganua matatizo haya kwa kina hasa yale ya kisemantiki.

Utafiti mwingine ufanywe kutafuta njia zingine za kusuluhisha makosa haya na pia uweze kuangazia ni kwa kiwango kipi makosa haya yanaathiri utendaji wa wanafunzi na walimu na umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kuwa wakuza mitaala watayatambua matatizo yanayowakabili wanafunzi wa lugha ya Kiswahili na kutafuta mbinu za kuyatatua.

# MAREJELEO


Corder, S. (1967) *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford: Oxford University Press.

Corder, S.P (1973) *Introducing Applied Linguistics.* Middlesex: Penguin.

Ellis, R. (1985) *Understanding Second Language Acquisition.* Oxford: OUP.

Gass, S.M. na Selinker, L. (2001) *Second Language Acquisition: An Introductory Course* (2 Ed.) N.J Lawrence Erlbaum Associates.

Habwe, J. H. na P. Karanja (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Iribemwangi, P. (2008) *A Synchronic Segmental Morphophonology of Standard Swahili.* Tasnifu ya PhD, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kapufi, O.J. (2008) *Ukiushi wa Viambishi Vipatanishi Unaojitokeza katika Kazi za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kisakwah, B.A (2014) *Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi Sahili za Kiswahili na za Kisuba*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Massamba, D.P. (1990) *Sarufi Miundo ya Kiswahili sanifu*. Dar es Saalam: Tuki.

Matei, A.K (2008) *Darubini ya Sarufi.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Mbaabu, I. (1992) *Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Longman.

Mbaabu, I. (1995) *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili.* Nairobi: Longhorn.

Mghambi, R.S, (1991) *Ukiushi katika lugha ya kimaongezi dhidi ya kanuni za Kiswahili sanifu.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mgullu, R.S. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn.

Mweri, G. (2010) *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: KLB.

Njogu, K. et al (2006) *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foudation.

Obuchi, S.M. na Mukhwana, A (2010) *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele.* Nairobi: A-Frame Publishers.

Rapando, M.M. (2005) *Makosa ya Kimofo-Sintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Selinker, L. (1969) *Language Transfer, General Linguistics.* New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. (RAL).

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Dar es Salaam: Educational Publishers and Distribution LTD.

TUKI (2006) *English- Swahili Dictionary 3rd Edition,* Institute of Kiswahili Research of Dar es Saalam.

## KIAMBATISHO

Haya ni makosa tuliyoyapata kutoka kwa wahusikia wetu wa utafiti. Tuliyaandika tu kama yalivyotamkwa bila kufuata utaratibu wowote. Vile vile hatujaandika waliofanya makosa haya. Huenda ikawa makosa yalikuwa mengi zaidi lakini haya ndiyo tuliyoweza kuyapata na kuyaandika.

1. Darasa lenu lina dirisha nyembamba.
2. Ning'iniza shati ukutani
3. Miti iliokatwa haikuwa mikubwa.
4. Miti ingine iliyopandwa imekauka.
5. Baba aliwanunulia nyanya yangu suka kwa sababu ya kumlea.
6. Chakula zuri kinatamanisha.
7. Darasani huku kuna uchafu.
8. Hatutaki mikutano zenu za ujinga.
9. Blauzi hili ni langu.
10. Darasa nzuri ni lile lililooshwa.
11. Mwalimu alinipa tunda ndogo.
12. Nilirara mapema ili niamke mapema
13. Darasani mwomwote mnafaa.
14. Mwalimu alisema tuimbe wimbo yoyote.
15. Hizo ndizo mifupa za mbwa.
16. Dirisha ndogo haitaingiza mwangaza wa kutosha.
17. Hapa ndiko kwangu.
18. Soko iliyouza matunda zamani iliitwa Gakira.
19. Soko yenu ni ya Gakira?
20. Chura chake kiliruka mtoni.
21. Nilikura chakura changu kabla ya mwarimu kuingia
22. Godoro niliyonunuliwa ndiyo inanifanya nichelewe.
23. Humu ndimo ambako mtakaa.
24. Hatutaki meza ingine.
25. Mwarimu alisema kuwa hamjafagia vizuri
26. Kuku alichakulachakula akitafuta chakula'
27. Hizi ndizo viatu za shule yetu.
28. Choo moja ya wavulana haijaoshwa.
29. Huyu si mamake kamili, mamake alikuwa mtasa.
30. Ludi darasani
31. Jina ya mamangu ni Rosa.
32. Karatasi zuri ndiyo inatakikana.
33. Kata kucha hizi ingine.
34. Hiki ndikio kitabu kiangu.
35. Kiatu yangu ni ya rangi nyeupe.
36. Wasichana ambao wanaokuwa wachafu wanakasirisha.
37. Kijiko ndogo kinatoshea kinywani.
38. Kijiti baya kinaweza kumdhuru mtoto.
39. Hizo ndizo vijiko chafu.
40. Alikuwa anaangalia kipindi radioni

41. Nashukua fulsa hii kuwasukulu warimu na wasasi kwa kuhuthuria mkutano huu,
42. Mlima watoto waliyoupanda.
43. Moyo ya mtoto hupiga mara nyingi kuliko ya mtu mzima.
44. Kioo iliyovunjwa na mtoto ipelekwe ofisini.
45. Kisu ya kukatia maembe.
46. Mashule hayo mengine yametushinda.
47. Fijana wa siku hizi wameharibika.
48. Usifae sale ya shule iliyo na ushafu.
49. Kitanda refu ni cha baba.
50. Nasikia njaa.
51. Ng'ombe anaenda ni wangu.
52. Mahali kwokwote kunafaa.
53. Maji ya kuosha darasa ilitiririka.
54. Kiziwi kilichotajwa kilikuwa kanisani siku ya Jumapili.
55. Kwokwote huko pafagiliwe.
56. Usirarekabla ya kumaliza kasi niliyokupa'.
57. Kuku wanachakulachakula nyuma ya darasa wakitafuta chakula.
58. Madaktari wetu wa Kenya wanawajibika.
59. Machozi yangu ilitiririka.
60. Wanywaji wa pombe watakayeshikwa hawatasamehewa.
61. Mhubiri ambaye aliyehubiri alitufurahisha sana.
62. Nitawaletea shati lililoshorwa sehemu ***'sa'*** mwili'
63. Kuku zile zinataga mayai mengi.
64. Mungu, tuondolee matatizo tuliyokuwa nazo Januari.
65. Kuta ambazo zilizopakwa rangi haziandikiki.
66. Huyu ananing'olea uzi yangu yenye madoadoa.
67. Kuku zao hutaga mayai mengi zikishiba.
68. Fijana wa dalasa la nane wanaandika fisuri sana
69. Mablauzi haya ni yetu.
70. Wavulana wanakunywa sigara
71. Msibebe viti ndogo ya watoto wa chekechea.
72. Kurasa ambazo zilizochafuka zilimkasirisha mwalimu.
73. Madarasa ndio yataoshwa kwanza.
74. Kipindi tuliyopoteza itafunzwa kesho.
75. Mahali kwenyewe ndipo kuliwapendeza.
76. Mbuzi ile iliyo na pembe ndefu.
77. Kiranja aniletee vitabu za insha baadaye.
78. Mbuzi inakula mahindi ya matron.
79. Nilikuja na miguu.
80. Makaratasi ambayo yataandikwa yawe safi.
81. Nunua vijiko sita.
82. Nyufa ya ukuta inapitisha upepo.
83. Nitakula ugali na sukumawiki,
84. Watoto mwendelee vivyo hivyo
85. Manyumba yenu yawe yanafagiliwa.
86. Kuna mkutano ya walimu majilisini.

87. Marafiki wanacheka wanapendana.
88. Lugha mingi za kiafrika si kama Kiswahili.
89. Kifaranga changu kinanenepa.
90. Maziwa hiyo ni tamu.
91. Kitabuni hiki kina picha za kupendeza.
92. Maziwa inafanya mate itiririke.
93. Mbuzi gani hiyo?
94. Likariri shairi nzima, usikariri nusu nusu.
95. Michungwa za jirani zimezaa.
96. Mikeka hizo hazijaoshwa.
97. Sisi ndio walimu wa shule hii.
98. Mwelewane bila kupigana.
99. Mikono zangu zinauma.
100. Mitume inayopatikana katika bibilia ilikuwa na uwezo kuliko binadamu wa kawaida.
101. Mjeledi mwenyewe ulipotea.
102. Mkata uliokuwa msafi tuliupenda.
103. Mkate mwenye utamu utaliwa na mtoto mzuri zaidi.
104. Vipepeo hivyo vinapendeza.
105. Mkija kesho mkiwa mmechelewa nitampiga.
106. Mkipata alama mia nne nitawaandalia kalamu ya kukata na choka.
107. Mpaka huu iliwekwa na mwenyekiti aliyestaafu.
108. Mtayarishaji wa pombe atakaoshikwa ataadhibiwa.
109. Ng'ombe yangu itatoa maziwa mingi kuliko za jirani.
110. Mtoto ya shule asiajiliwe.
111. Mwalimu aendae shuleni mapema huanza kazi yake mapema.
112. Ziyara tunayoitayarisha itakuwa ya kupendeza.
113. Mwalimu mkuu aliingia darasani ambalo halikuwa na watoto.
114. Nchini Kenya ina mamilioni ya watu.
115. Mfupa uliyoutupa bado ulikuwa na nyama.
116. Ndege inayokula nafaka inaweza kuliwa na baadhi ya watu.
117. Marinda zenu zikiraruka zishonwe.
118. Mashini mawili ya kushonea nguo yalipotea.
119. Ndege yake ilitoroka alipokuja shuleni.
120. Mimi ndiye niliyemwona.
121. Ng'ombe yangu imezaa.
122. Majina za wanafunzi ziandikwe vizuri ili ziweze kusomeka baadaye.
123. Ng'ombe hizo ndizo zitakazokamwa.
124. Penga makamasi hiyo.
125. Mikutano ingine haifai wakati wa usiku.
126. Mlima watoto waliyoupanda.
127. Moyo ya mtoto hupiga mara nyingi kuliko ya mtu mzima.
128. Nguruwe hii imenona kwa sababu inakula mabaki ya chakula yetu.
129. Onyesheni vitambaa za kupengea makamasi.
130. Parachichi hii imeiva.
131. Ng'ombe zinaenda mtoni kunywa maji.

132. Peleka parachichi ya mwalimu majilisini.
133. Nilipofagia kulikuwa na uchafu.
134. Pelekeni viti za walimu ukumbini.
135. Ng'ombe ilichinjwa ikaliwa na shule nzima.
136. Vikombe zetu ni safi, labda zenu.
137. Mpaka huu ndiyo wa shule yetu.
138. Wanasiasa walitukanana wataadhibiwa.
139. Mpango hiyo haitafaa kwa hivyo nirudishie mikate zangu.
140. Rais Uhuru Kenyatta ni mshujaa.
141. Njia hio inapitia karibu na kwao.
142. Shati yake imeraruka.
143. Rinda hiyo isije shuleni kesho.
144. Vikombe za walimu zilioshwa na mpishi.
145. Wanafunzi ambao waliochelewa waadhibiwe.
146. Shati mbovu lisivaliwe shuleni.
147. Ukutani ulikuwa na chati za hisabati
148. Shati nyeupe itapata uchavu haraka.
149. Mikebe ndio hii, enda ukachote maji.
150. Maandishi hii ina makosa mengi.
151. Ulikate ua nyeupe uache ile nyekundu.
152. Mate hiyo uliyotema ndiyo iliyomfanya mwenzako akasirike.
153. Shule yetu ni shule ipendwao na wazazi.
154. Ufa mwenyewe utazibwa na mwalimu.
155. Sungura zuri ya kakangu iliuzwa.
156. Tutatumia magari za abiria iwapo hatutapata basi ya shule.
157. Uende ukalete viazi vitamu za kumpa mwalimu wetu.
158. Ufunguo ambao uliotupwa umepatikana.
159. Tunda mbaya halitaliwa.
160. Ukitumie kijiti kiembamba kumpigia mtoto.
161. Tunda lizuri litapewa mtoto mwerevu.
162. Ukuta ilipakwa rangi ikapakika
163. Usimwone akiwa mkulima chafu, amefanikiwa maishani.
164. Samaki zao zimeoza lakini zetu bado.
165. Shati mbovu lisivaliwe shuleni.
166. Tengeneza masiku zako za usoni.
167. Usipitie njiya ya mkato pitiya barabarani.
168. Usiutupe mpira yangu.
169. Tumbo ndiyo sehemu ya mwili muhumu sana kuliko sehemu nyingine.
170. Uzi inayotumiwa inastahili kuwa ngumu.
171. Sitaki excuses enda umlete mzazi.
172. Vifaranga vyao vinapiga kelele.
173. Cucuu hapendi chapoo.
174. Vitendo zenu zimemkasirisha mwalimu wa zamu.
175. Wakati wa mgomo, ni walimu chache tu waliowasili.
176. Usinawe mikono kwa maji hii.
177. Walimu na wazazi hawapendi watoto baya.

178. Usiposoma kwa bidii utapatwa na mashinda kama haya.
179. Ukuta ilipakwa rangi ikapakika.
180. Walivipeleka vile viti ndefu ukumbini.
181. Huyu ndiye boss wangu
182. Usiseme maongo kama hayo.
183. Sungura yako ilikula majani?
184. Watoto hawa ni wasafi.
185. Yai yangu ndiyo kubwa kuliko yako.
186. Soko ndiyo itajengwa kwanza kisha tutengenezewe barabara.
187. Weka kikomo ya kuonyesha mwisho wa sentensi.
188. Akachukua kitabu yangu akaenda nayo.
189. Shule yetu itapewa supervisor yupi?